Hii ni nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

**Kikao cha Pili - Tarehe 5 Novemba, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 16

### Vituo vya Mabasi Nchini

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR (k. n. y. MHE. DR. BATILDA S. BURIAN)** aliuliza: -

Kwa kuwa vituo vikubwa vya mabasi ya abiria ni eneo la umma kama ilivyo kwa eneo la hospitali, masoko na kadhalika na hivyo basi haipaswi mtu anayekwenda kwa miguu kulipa ada ya kuingia kwenye maeneo hayo na hasa kwenye maeneo ya vituo vya mabasi.

Je, kwa nini waenda kwa miguu wanaowasindikiza wasafiri wao katika Kituo Kikuu cha Ubungo Jijini Dar es Salaam wanalipishwa ada ya kuingia kituoni hapo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Batilda S. Burian, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kituo Kikuu cha Mabasi ya Ubungo kilianzishwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam tarehe 06 Desemba, 1999. Madhumuni ya kuanzisha kituo hiki yalikuwa ni pamoja na: -

(i) Kupunguza msongamano wa magari katikati ya Jiji ambao ulikuwa unasababisha misururu mirefu ya magari na hivyo kusababisha watu kuchelewa kazini na kwenye huduma mbalimbali.

(ii) Kupunguza vituo holela vya mabasi yaendayo Mikoani vilivyokuwa vimezagaa katikati ya Jiji ambavyo mara nyingi vilisababisha ajali hasa kwa waendao kwa miguu.

(iii) Kuondoa vibaka na wapiga debe ambao wanaleta kero kwa abiria na mali zao.

(iv) Kuwa na kituo cha mabasi cha kudumu cha kuaminika kwa mabasi yaendayo Mikoani na nchi jirani.

(v) Kuwa na kitega uchumi kwa lengo la kuongeza mapato ya Halmashauri ya Jiji ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutoza ada ya shilingi 200/= kwa kila msindikizaji ulianza mwezi Februari, 2000 na inatozwa kwa mujibu wa sheria ndogo ya Kituo cha Mabasi Ubungo. Lengo la kuanzishwa kwa ada hii ni kuboresha huduma ndani ya kituo ambazo hazikuwepo hapo awali. Huduma hizi ni kama vile ukumbi wa kupumzikia abiria, huduma za matangazo, usafi wa kituo, maji na vyoo vya kulipia. Kabla ya kuanzishwa kwa utaratibu huu Halmashauri ya Jiji ilitangaza sheria ndogo *(By Law)* ya Kituo cha Mabasi Ubungo kupitia Vyombo vya Habari ili kutoa fursa kwa wananchi wote watoe maoni yao. Hadi sheria hiyo inaanza kutumika hakuna maoni yaliyopokelewa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Jiji iliwasilisha ombi maalum kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa barua kumbukumbu nambari *DCC/0.15/30 Vol. IV/3* ya tarehe 24 Juni, 2002 la kuruhusiwa kuendelea kutoza ushuru kwa wanaosindikiza abiria katika Kituo cha Mabasi cha Ubungo ili Halmashauri iendelee kukusanya mapato kwa kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi wa Tanzania na nchi jirani wanaotumia kituo hiki.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa jumla ya shilingi 416,100,000/= zimekusanywa. Vile vile, jumla ya shilingi bilioni 1.4 zimetumika katika kuboresha huduma mbalimbali ndani ya kituo kama nilivyokwishaeleza hapo awali.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuzingatia kwamba Jiji lina njia nyingi za kuweza kupata mapato yake ya kuendesha huduma na kwa mujibu wa agizo la Waziri Mkuu la kuondoa vizuia hasa pale uwanja wa ndege na Muhimbili. Je, ni kwa nini hivi sasa Jiji wasiweze kuondoa ada hasa ya magari? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, maeneo haya yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge kama vile *Airport* na unaweza hata ukatou mfano wa Muhimbili mazingira yake ni tofauti kidogo na tunapozungumzia Kituo cha Mabasi kama cha Ubungo.

Waheshimiwa Wabunge, nina hakika kabisa mnajua kama Halmashauri isingechukua hatua za kujaribu kupunguza *inflow* ya watu wanaoingia pale bila sababu za msingi leo tungekuwa tunailaumu Halmashauri kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, naomba utaratibu uendelee. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa kituo hiki kilijengwa kwa haraka haraka na hivyo mipango mikubwa ilikuwa bado haijafikiwa na kwa kuwa kituo hiki kimekuwa kivutio kikubwa kwa watu hata wanaotoka nje ya nchi. Je, Serikali ina mpango gani wa kukikuza na kukitengeneza kituo hiki kiwe na hadhi ya Kimataifa ukizingatia kina nafasi kubwa ya kufanya hivyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa *very positive* katika suala hili, jambo ambalo nadhani ni jema sana. Kama nilivyosema, tunaendelea kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kujaribu kuboresha kituo hiki kwa kiwango ambacho kitafikia viwango vya juu zaidi kuliko ilivyo sasa.

Kwa hiyo, tuvute subira kidogo, nadhani juhudi zitazaa matunda mema baada ya muda si mrefu. *(Makofi)*

Na. 17

**Mafuta ya Magari ya Wakuu wa Wilaya**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali ilifanya uamuzi wa busara na tunaipongeza kwa kuwanunulia magari ya kusafiri Wakuu wa Wilaya: -

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwapatia fedha ya kutosha ya kununua mafuta ili wakuu hao wasiendelee kutegemea Halmashauri za Wilaya ya Miji na hivyo kuwafanya waonekane omba omba mbele ya Halmashauri hizo za Wilaya?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kurudisha ulinzi kwa Wakuu wa Wilaya katika mazingira haya ya ujambazi?

(c) Je, Serikali haioni madhara yatakayolipa Taifa iwapo Wakuu hawa watadhurika kutokana na uamuzi wake wa kufanya wasilindwe na Polisi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, magari ya Wakuu wa Wilaya yako chini ya Serikali Kuu kama yalivyo magari mengine ya Viongozi wa Serikali. Upo utaratibu mahsusi wa Serikali kuyapatia mafuta pamoja na matengenezo magari yote yaliyo chini ya Ofisi za Wakuu wa Wilaya kwa kutumia fedha za matumizi ya kawaida ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Aidha, ni kweli kuwa Wakuu wa Wilaya kwa miaka ya nyuma walikuwa wakikabiliwa na uhaba wa fedha za kuendeshea ofisi zao na hivyo kwa kiasi fulani kuzitegemea Halmashauri, lakini kwa sasa tatizo hilo limedhibitiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, hatua iliyochukuliwa na Serikali kuhakikisha kuwa magari ya Wakuu wa Wilaya hayategemei mafuta kutoka kwa Wakurugenzi wa Miji na Halmashauri za Wilaya hizo ni pamoja na kutuma fedha za kutosha za matumizi ya kawaida moja kwa moja kwa Makatibu Tawala wa Wilaya.

Kuanzia mwaka huu wa fedha jumla ya shilingi 3,396,144,200/= zimetengwa kwa ajili ya ofisi zote za Wakuu wa Wilaya. Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo kwa kila Wilaya unategemea kipaumbele kwa wakati unaohusika. Mfano mzuri ni Wilaya ya Njombe ambao kati ya shilingi 28,613,200/= walizotenga shilingi 4,634,000/= zimewekwa kwa ajili ya mafuta kwa mwaka mzima.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu ulinzi, naomba tu kumjulisha Mheshimiwa Mbunge wa Njombe Kaskazini kuwa, Serikali haijaondoa ulinzi kwa Wakuu wa Wilaya. Mkuu wa Wilaya ni Kiongozi wa Serikali na Mlinzi wa Amani katika ngazi ya Wilaya. Kulingana na masharti yao ya kazi Wakuu wa Wilaya wanastahili kupewa walinzi kwenye nyumba zao. Hivi sasa nyumba za Wakuu wa Wilaya zinalindwa na walinzi waliopitia mafunzo ya Mgambo.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua dhamana kubwa waliyonayo Wakuu wa Wilaya katika Taifa hili. Aidha, Serikali ingependa sana kuwapa ulinzi wa Polisi, lakini kwa sasa bado haina uwezo wa kuwapatia ulinzi huo kutokana na uchache wa Askari waliopo.

Kuhusu utaratibu wa Wakuu wa Wilaya kulindwa na Polisi napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa sasa Serikali imeainisha baadhi ya viongozi ambao watalindwa na Polisi. Viongozi hao ni Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri na Wakuu wa Mikoa. Hapo baadaye Serikali inaweza kufikiria kuwapatia ulinzi wa Polisi Wakuu wa Wilaya kufuatana na uwezo wa Serikali wa kuajiri Polisi wa kutosha.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa niipongeze Serikali kwa hatua hizo ambazo imechukua, lakini kwa upande wa ulinzi Mkuu wa Wilaya ndiye kielelezo cha Serikali katika ngazi ya Wilaya.

Pale Njombe Polisi wapo ½ kilomita kutoka nyumba ya Mkuu wa Wilaya, lakini Mkuu wa Wilaya huyo analindwa na mgambo akiwa na kirungu cha mti wa mwanzi, kiusalama ni hatari sana. Bado ninapendekeza Serikali ichukue hatua za haraka kwa sababu ya madhara yanayoweza kujitokeza kwani mazingira yamebadilika. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ulinzi wa mgambo tusiudharau na unaongozwa huko huko mikoani. Mgambo wanaweza wakatumia silaha kama maombi ya ruhusa yatatolewa na kukubaliwa.

Lakini vile vile kuhusiana na Polisi ni kwamba, pamoja na kuwa Wakuu wa Wilaya hawamo kwenye orodha ya kupatiwa ulinzi wa Polisi, lakini Mkuu wa Wilaya na hata kiongozi mwingine yeyote anapohisi kwamba ana tishio la kiusalama la kweli kweli anayo haki ya kuomba dharura ya ulinzi na akapatiwa. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwa kuwa Mkuu wa Wilaya ni msimamizi wa shughuli zote za Serikali katika eneo lote linalohusika na kwa kuwa Mkuu wa Wilaya anafanya maamuzi makubwa na mazito ambayo yanaudhi hasa maadui. Je, ni kwa nini katika suala hili la kumpa Mkuu wa Wilaya ulinzi wa Polisi lisitamkwe wazi wazi kuliko kukaa tukaanza kufikiria habari ya Mgambo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi imeelezwa kwamba miongoni mwa matatizo tuliyonayo yaliyosababisha uamuzi wa kuwa Wakuu wa Wilaya kutoorodheshwa katika viongozi wanaopata ulinzi wa Polisi ni kwa sababu ya upungufu wa Askari tulionao.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Ndiyo.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge siku zote hapa wanatuomba: "Katika kituo changu nina upungufu wa Askari, nileteeni Askari." Hicho ni kielelezo cha kutosha kwamba hatujawa na Askari wa kutosha, lakini juhudi za kuongeza Askari zinaendelea na tutakapofika mahali hali ikaruhusu wataingizwa kwenye orodha.

Na. 18

**Dhahabu - Iramba Mashariki**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza: -

Kwa kuwa ukanda mzima wa Iramba Mashariki yaani maeneo ya Singa, Mwanga, Nkungi, Madirika, Kidarafa, Kinampanda, Singida Kaskazini maeneo ya Mudida, Hannang, Mbulu maeneo ya Mwanga, Hillbador Basutu, Hydom yana dhahabu nyingi na nzuri sana.

(a) Je, Serikali inasemaje juu ya ukweli huo?

(b) Kwa kuwa inasemekana kwamba maeneo haya yameshachukuliwa na Makampuni makubwa; je, Serikali haioni kwamba kutakuwa na mwingiliano mkubwa na wakulima hasa ikizingatiwa kwamba maeneo hayo yanatumika zaidi kwa kilimo cha ngano?

(c) Je, Serikali itawasaidiaje wachimbaji wadogo wadogo wa maeneo hayo ili wapate vifaa vya kuchimbia dhahabu hiyo na pia kujikinga na zebaki?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Sehemu kubwa ya maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge ndiyo sasa yanafanyiwa utafiti wa kina wa kijiolojia wa kuthibitisha wingi wa dhahabu iliyopo. Utafiti huo unafanywa na Kampuni ya kigeni inayojulikana kama *Barrick Exploration Africa Ltd.* Shughuli zinazoendelea ni pamoja na uchorongaji wa miamba ama kwa lugha ya kigeni *drilling* katika baadhi ya maeneo ili kujua miamba yenye dhahabu inaenda chini kiasi gani.

(b) Mheshimiwa Spika, sheria ya Madini ya mwaka 1998 katika kifungu Na. 95 (1) (b), (ii) na (iii) inamzuia mtu ama Kampuni yenye leseni ya madini kufanya kazi katika eneo lolote la kilimo isipokuwa kwa kibali kutoka kwa mmiliki wa eneo husika. Hivyo, hatutegemei kuwa utatokea mwingiliano kati ya watafiti wa madini na wakulima usio na ridhaa.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara ina Ofisi ya Madini Mjini Singida. Kati ya majukumu ya Maafisa wa Madini katika ofisi hiyo ni pamoja na kuwatembelea wachimbaji wadogo mkoani humo na kutoa ushauri kuhusu vifaa ambavyo vinafaa kununuliwa na wachimbaji wadogo vinavyolingana na hali ya miamba ya maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwasaidia wachimbaji wadogo kujikinga na zebaki linahusu mambo mawili ambayo yamekuwa yakifanyika katika Ofisi za Madini kuwaelimisha madhara ya zebaki na jinsi ya kujikinga kwa kutenga maeneo maalum mbali ya mito na vijito vya kusafishia mchanga wenye zebaki na kuwahamasisha kukunua na kutumia vigida *(retors).* Mbinu zinazotumika ni pamoja na kutembelea maeneo husika na kuonyesha filamu za video na kusambaza vipeperushi na mabango.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nichukue nafasi hii kwa kweli kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada zake za kufuatilia suala la wachimbaji wadogo katika eneo lake.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa wachimbaji wengi wadogo wadogo sasa hivi wana uwezo wa kununua vifaa vya kuwasaidia, lakini hawajui wavipate wapi. Je, Serikali inaweza kusaidia kutafuta makampuni ambayo yanauza hivi vifaa na kuvileta kwa wachimbaji wadogo wadogo wa Iramba na maeneo mengine yote wanaohitaji?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kutafuta au kuwaelekeza wachimbaji wadogo mahali ambapo vifaa vinapatikana na tuko tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo wadogo wa Iramba na sehemu nyingine nchini wanaelekezwa wapi pa kupata vifaa hivyo vya uchimbaji.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa vile Kampuni ya *Barrick* imekuwa na leseni ya kutafiti dhahabu katika maeneo hayo kwa muda mrefu na haionyeshi jitihada zozote za kuendeleza uchimbaji wa dhahabu hasa katika ka Kijiji cha Endarhadat katika Wilaya ya Mbulu. Je, Wizara iatakuwa tayari kufuta leseni hii hasa katika maeneo ya Hydom na Endarhadat ili watu wengine waweze kutumia fursa hii kufanya utafiti na kuchimba dhahabu ambayo wazi inaonekana iko katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, utafiti wa madini unachukua muda mrefu na gharama kubwa. Lakini pia katika utafiti wa madini Serikali inao utaratibu wa utoaji leseni ambao unazingatia muda na muda ukiisha wale wanaoomba leseni inabidi waonyeshe kama wana uwezo wa kuendelea kutafuta madini katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi ningependa kumwomba Mheshimiwa Mbunge akubali kwamba kwa kweli tuwaachie watafiti hao waendelee na kazi hiyo na hapo itakapoonekana kwamba wameshindwa, leseni yao itakapofikia muda wa kuisha hawatapewa tena, watatafuta watu wengine.

Na. 19

**Umeme - Kigoma**

**MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU** aliuliza: -

Kwa kuwa wananchi wengi wa Kigoma wanaamini kuwa kutokuwepo na umeme wa uhakika kumechangia kwa kiwango kikubwa kuongezeka kwa umaskini, kutokana na kutokuwa na wawekezaji mkoani humo.

(a) Je, Serikali itakubaliana na tathmini ya wananchi wa Mkoa huo?

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa uhakika Kigoma na ni utaratibu gani utakaotumika?

(b) Je, kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kutoa umeme toka Burundi?
(c)
**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Amani W. A. Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Kwanza kabisa, pamoja na kwamba uwekezaji una mambo mengi, Serikali inatambua na kwa kweli ni dhahiri kuwa umeme ni nyenzo muhimu ya kuvutia wawekezaji na kuleta maendeleo. Hivyo, Serikali inakubaliana na tathmini kuwa umeme wa uhakika ni nyenzo muhimu ya kuleta maendeleo.

Katika kushughulikia suala la umeme wa Mkoa wa Kigoma katika miaka michache iliyopita, Serikali imekuwa na mpango wa muda mfupi wa kuhakikisha kuwa umeme kwa mji wa Kigoma unapatikana na mpango wa kudumu wa kuupatia Mkoa mzima wa Kigoma umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza wakati najibu maswali ya Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou tarehe 31 Julai, 2001 na Mheshimiwa Magayane tarehe 01 Novemba, 2002, katika hatua za muda mfupi Serikali iliahidi kupeleka Mjini Kigoma mashine mbili za dizeli kutoka Kihansi, zenye uwezo wa kutoa zaidi ya *MW 1.0* kujenga nyumba ya kuzalishia umeme *(Power House)* na kufanya ukarabati wa mashine za zamani. Kazi hizo zote zilifanyika na ilipofika Mei, 2003 hali ya umeme Mjini Kigoma ilikuwa imeboreshwa.

Kwa bahati mbaya mashine hizo zilipata hitilafu ya kiufundi na *TANESCO* kulazimika kuzisimamisha kwa matengenezo ambayo baadhi yake yanatarajiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa wiki hii. Kusimama kwa mashine hizi kumesababisha mgao mkubwa wa umeme Mjini Kigoma na napenda kuchukua nafasi hii kuwapa pole wananchi wa Kigoma Mjini na kusema kuwa Serikali inajitahidi kushughulikia suala hili ili kero hii ya mgano iondoke.

Mheshimiwa Spika, juu ya hatua za kudumu za kuupatia Mkoa wa Kigoma umeme wa uhakika, Serikali ilifanya tathmini ya awali ya kupeleka umeme wa gridi ya Taifa, wa msongo wa kilovolti 132 kutoka Tabora kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 36 na hata sasa kazi ya kupeleka umeme Urambo na Kaliua inafanyiwa

marekebisho ili msongo wa umeme utakaofika Urambo/Kaliua uwe wa kilovolti 132 badala ya kilovolti 33 za awali, ili iwe rahisi kufikisha umeme mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Spika, njia nyingine ya kuupatia Mkoa wa Kigoma umeme wa uhakika ni ile ya kujenga kituo cha umeme wa nguvu za maji kwenye maporomoko ya Mto Malagarasi na kufikisha umeme Uvinza, Kasulu, Kigoma na Kibondo. Chanzo hiki cha umeme kingegharimu zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 30 na kwa *MW 10* za umeme kwa mfano. Ndio maana kutokana na gharama za uzalishaji na matatizo mengine ya kiufundi katika Mto Malagarasi kuwa kubwa ikilinganishwa na umeme utakaopatikana. Serikali inatazama zaidi uwezekano wa kuupatia Mkoa wa Kigoma umeme kutoka kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya majadiliano na wahisani, wakiwemo Benki ya Dunia na Serikali ya Sweden katika jitihada za kuupatia Mkoa wa Kigoma umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme wa Burundi, mawasiliano yamefanyika baina ya Serikali ya Burundi na Tanzania. Aidha, Mashirika ya umeme ya nchi hizi mbili pia yalifanya majadiliano yaliyobainisha kuwa mfumo wa umeme wa gridi wa Burundi hauna uwezo wa kukidhi mahitaji ya umeme wa Mkoa wa Kigoma.

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Majibu aliyotoa Mheshimiwa Waziri hayo ndiyo majibu ya siku zote hata viongozi Wakuu wanapofika Mkoani Kigoma, wanakuwa na maelezo hayo hayo. Hivi tutaendelea kukaa gizani na kuombwa msamaha bila matumaini! Hebu tuambie, umeme utapatikana lini katika kipindi hiki kabla ya uchaguzi wa 2005? Hapo ndiyo tunataka majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, inaeleweka kwa sehemu ambayo umeme ni kero kubwa hata pale yanapotolewa maelezo ya kuonyesha maendeleo yanaweza yakaonekana kama ni majibu ya aina ile ile.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ina dhamira thabiti ya kuhakikisha kwamba Mkoa wa Kigoma unaunganishwa au unapata umeme wa uhakika na ndiyo maana nilichukua muda katika kuelezea hatua ambazo Serikali imechukua hadi sasa na kuelezea kwa mfano hatua ya majadiliano ambayo tunayo hivi sasa. Ni nia ya Serikali na ni matarajio yetu kwamba, umeme utapatikana Mjini Kigoma na Kigoma kwa ujumla mara fedha hizi zitakapopatikana.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunpatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwenye jibu la msingi la Mheshimiwa Waziri ametamka kwamba, wanafanya mabadiliko ya msongo wa umeme ambao ulikuwa uende Urambo. Kwa sababu

amesema wata *step-up* kwenda *132 KV,* sasa napenda kufahamu hayo mabadiliko ni lini yameanza kufanywa na yataisha lini na yataongeza gharama kwa kiasi gani na kwa nini tulikuwa hatujaambiwa hilo sisi wadau?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Dr. Msekela, kwamba haya mabadiliko au marekebisho ya kiufundi yanayotathminiwa sasa hivi hayataathiri ratiba ya upelekaji umeme Urambo na Kaliua.

Pili, gharama halisi ndiyo zinafanyiwa tathmini sasa hivi. Kwa hiyo, siwezi kutoa gharama hizo sasa hivi na majadiliano na wahisani kwa ajili ya kuongeza gharama hizo yanafanyika hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie kwamba ahadi ya Serikali ya kufikisha umeme Urambo na Kaliua, ambao inaweza kuwa ndiyo wasiwasi mkubwa ipo pale pale. Lakini ni muhimu wakati ninafanya kazi hii hivi sasa ni bora kuchukua hatua hizi za tahadhari ili hapo baadaye iwe rahisi zaidi kwa Serikali kufikisha umeme Mkoa wa Kigoma.

Na. 20

**Wachezaji wetu Kuiga Mitindo ya Wachezaji wa Nje**

**MHE. RAMADHANI NYONJE PANDU** aliuliza: -

Kwa kuwa siku hizi kumekuwa na mtindo kwa wachezaji wetu hasa wa mpira wa miguu kuiga tabia na mitindo ya wachezaji wa mchezo huo wa nje kama vile kusuka nywele, kusuka rasta, kuvaa kipuli (herini sikio moja la kushoto), kuvaa mikufu, bangili na kadhalika wanapokuwa michezoni.

(a) Katika jitihada za kukuza mpira wa miguu nchini, je, kuiga mitindo na tabia kama hizo kunasaidia vipi kuinua kiwango cha mchezaji huyo na kiwango cha mpira wa miguu kwa ujumla?

(b) Kwa kuwa Chama cha Mpira wa Miguu *(FAT)* kimefumbia macho tabia na mienendo hiyo, je, ndiyo kusema kwamba hizo ni miongoni mwa sheria mpya za *FIFA* na *FAT?*

(c) Kama ikitokea kwamba mwamuzi wa mpira wa miguu naye ameiga tabia na mitindo hiyo na akaingia uwanjani kuchezesha mpira; je, Chama cha Marefarii Tanzania *(FRAT)* na Serikali kwa ujumla itasema nini juu ya hali hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI k. n. y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Nyonje Pandu, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Wachezaji wa mpira wa miguu kuiga mitindo ya wachezaji wa nje kama vile kusuka nywele, kusuka rasta, kuvaa kipini na kadhalika ni utashi wa mchezaji katika kujitambulisha miongoni mwa wananchi ili kujipatia umaarufu. Hivyo, tendo hili halisaidii chochote katika kuinua au kushusha kiwango cha mchezaji.

(b) Chama cha Mpira wa Miguu *(FAT)* hakijafumbia macho tabia na mienendo hiyo, kwa kuwa mienendo na tabia hizo si sheria 17 za mpira wa miguu ambapo mienendo na tabia hizo hazikuelezwa. Huu ni utawala na utashi wa mchezaji mwenyewe. *(Makofi)*

(c) Kama ikitokea kwamba mwamuzi wa mpira wa miguu naye anaiga tabia na mitindo hiyo ya nje na akaingia uwanjani kuchezesha mpira, huo ni utawala binafsi na utashi wake. Hakuna sheria inayombana asifanye hivyo. *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa vile Mheshimiwa Waziri amesema ni utashi tu wa mchezaji mwenyewe, lakini hakuna kanuni wala sheria inayombana mchezaji; je, kiutamaduni, mila na silka za Tanzania hii inakubalika? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI k. n. y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO):** Mheshimiwa Spika, kwa haya yaliyotokea Tanzania, binafsi sidhani kama tumeyaona mambo ambayo yanaathiri mila na desturi za Tanzania hasa yanayohusu wachezaji wa mpira wa miguu, maana swali lenyewe lilikuwa linahusu mchezo wa mpira wa miguu. Yale ambayo yanafanywa kinyume cha utaratibu wa mpira wa miguu ambayo yameainishwa katika zile sheria 17 za mpira wa miguu yanadhibitiwa na vyombo vinavyohusika kwa mujibu wa utaratibu wa soka.

Na. 21

**Uwezeshaji wa Watu Wenye Ulemavu Kujitegemea**

**MHE. MARGARETH A. MKANGA** aliuliza: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali walio wengi hapa nchini ni maskini na wanaishi maisha duni sana kiasi kwamba wanashindwa kuendesha maisha yao hata ya kujikimu.

Je, Serikali ina mikakati gani thabiti ya kuiwezesha jamii hiyo ya wananchi ili nayo iweze kujitegemea katika maisha badala ya wengi wao kuwa ombaomba?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI k.n.y WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mbunge Vitu Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba watu wenye ulemavu ni miongoni mwa wananchi wengi wenye maisha duni.

Serikali kupitia mkakati wa Taifa wa kuondoa umaskini inajenga mazingara yanayohakikisha kwamba wananchi wanawezesha kuinua hali zao za kiuchumi. Mazingira hayo ni pamoja na kuhamasisha wananchi kujiunga katika vikundi vya uzalishaji mali na kujipatia mikopo kupitia asasi za kijamii kama vile benki, kata na vyama vya kuweka na kukopa.

Mheshimiwa Spika, hatua mahsusi zinazochukuliwa kwa ajili ya kuinua hali za kiuchumi za watu wenye ulemavu ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Sheria ya ajira kwa watu wenye ulemavu namba 2 ya mwaka 1982. Pamoja na ukweli kwamba utekelezaji wa sheria hii umekuwa na mapungufu bado imeweza kutumika kwa kuwapatia ajira watu wenye ulemavu. Aidha, sheria hii inatumika sana kuwarejesha kazini watu wenye ulemavu walioachishwa na waajiri kwa kigezo cha ulemavu wao.

(ii) Mikopo au Misaada kwa ajili ya wazalishaji mali. Kupitia idara ya Ustawi wa Jamii (Mradi wa *SHIA)* Wizara imekuwa inatoa mikopo kwa watu wenye ulemavu kuwawezesha kuendesha biashara ndogo ndogo. Aidha, Idara ya Ustawi wa Jamii inatoa fedha za miradi midogo kwa mwombaji mmoja mmoja.

(iii) Sera ya Maendeleo na Huduma kwa watu wenye ulemavu. Wizara ipo katika hatua ya mwisho ya kupitisha Sera ya Maendeleo ya huduma kwa watu wenye ulemavu. Sera hii itaimarisha mikakati mbalimbali inayolenga katika kuboresha maisha ya watu wenye ulemavu kwa kuhusisha sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo Wizara kupitia Idara ya Vijana inasimamia uendeshaji wa Mfuko wa Vijana ambao fedha zake hutumwa Wilayani. Napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, wenzangu tuwahamasishe vijana wenye ulemavu ili kuomba mikopo kupitia mfuko huu na asasi nyinginezo.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Je, ni kwa kiasi gani watu wenye ulemavu walishirikishwa wiki ya mkakati wa kuondoa umaskini ili nao waweze kutoa mawazo yao na kurekebisha mikakati hiyo, kuendana na matatizo yao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI k.n.y WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Mkanga, kama ifuatayo:-

Kongamano lililofanyika hivi karibuni nina uhakika lilihusisha taasisi zote na *NGOs* zote ikiwemo za vyama vyenye ulemavu. Zipo taasisi ambazo japo si za walemavu, lakini waliohudhuria walikuwa walemavu. Kwa hiyo, walikuwa na nafasi zote mbili. Lakini watu wenyewe kupitia vyama vyao walipitishwa katika maandalizi ya sera niliyoitaja, lakini hata katika wiki ya maadhimisho ya kuondoa umaskini.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, vile vile namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake lakini nina swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa sheria namba 2 ya mwaka 1982 aliyoitaja Mheshimiwa Waziri imekuwa na matatizo makubwa na hasa katika Idara za Serikali imeshindikana kuitekeleza na kwa kuwa walemavu wengi hasa waliofundishwa taalum kama *telephone operator* yaani *operation* ya simu wamepaswa kuondolewa na hivi kuna walemavu zaidi 200 waliojifunza kozi hizo kwenye taasisi zilizokuwepo.

Je, Serikali itafanya jitihada gani ili kuwapa angalau upendeleo maalum katika Idara za Serikali angalau hawa waliofundishwa kwa gharama kubwa waweze kubaki katika kazi yao? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI k.n.y WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, kama ifuatavyo:-

Pamoja na sababu nyingine lakini kuondolewa kwa watendaji siyo walemavu tu lakini wengi katika ajira ya kazi *operator* wa simu yametokana zaidi na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia kwa sababu zamani tulikuwa na mitambo mikubwa inayoendeshwa na watu, lakini sasa *automation* kuna mitambo ambayo inajiendesha yenyewe. Kwa hiyo, maeneo kama haya watu waliokuwa wanafanya kazi hizi wameondoshwa bila ubaguzi. Sasa kama kulikuwa na mlemavu ameajiriwa katika eneo hili anaweza kuguswa lakini ni kwamba sababu ya maendeleo ya teknolojia.

Mheshimiwa Spika, lakini sheria hii nakiri kwamba ina matatizo tangu ilipoanzishwa ilikuwa ngumu kutekelezwa hata ndani ya Serikali, baadhi ya taasisi chache sana kama kile Kiwanda cha Moshi cha Shah cha yule bwana anayetengeneza vitu vya ngozi, yeye alikuwa anapenda kuajiri walemavu kwa sababu alikuwa anaona anapata tija zaidi kwa kuwachukua walemavu kuliko watu wa kawaida kwa sababu mlemavu akikaa hakuna *movement* za chai, anazalisha saa 8 kama alivyo.

Kwa hiyo, yeye binafsi alikuwa ameamua, yeye ndiyo mfano katika nchi hii wa kuajiri na kutekeleza ile sheria. Lakini sehemu nyingi katika nchi hii walishindwa na ndiyo maana Wizara inakuja kufanya mapitio ya sheria hii ili angalau ziendane na wakati. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Taifa lolote lenye kulenga kupata maendeleo moja ya dhamira zake ni kupunguza idadi ya walemavu. Je, Taifa letu kwa miaka 10 iliyopita tumepunguza idadi hii ya walemavu kwa kiasi gani? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI k.n.y WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kahumbi, kama ifuatavyo:-

Kwa hesabu za uwiano wa Umoja wa Mataifa katika kila idadi fulani ya watu asilimia 10 inahesabika kwamba ni ya walemavu. Lakini ulemavu huu uko wa aina nyingi na aina nyingi ya ulemavu ni ya kuzaliwa, hasa ulemavu usio wa viungo lakini sehemu kubwa ya ulemavu kama *Maalbino* na wengine wasioona huwa ni ya kuzaliwa.

Kwa hiyo, Serikali inafanya jitihada ya kupunguza athari siyo kupunguza walemavu, kupunguza athari zinazoweza kusababishwa na ulemavu unaoweza kutokea. Hizo jitihada zinafanywa kupitia sekta mbalimbali hasa Wizara ya Mambo ya Ndani kupunguza ajali, afya ya mama na mtoto na mengineyo. *(Makofi)*

Na. 22

**Viwanda vya Mvinyo**

**MHE. WILLIAM J. KUSILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kilimo cha Zabibu katika Mkoa wa Dodoma kilififia sana katika miaka ya hivi karibuni baada ya soko pekee lililokuwepo la zao hilo yaani Kiwanda cha Mvinyo cha Dodoma kufa na kwa kuwa kilimo hicho kimeanza kufufuka baada ya viwanda vidogo vya watu binafsi kuanza tena kutengeneza mvinyo.

(a) Je, kuna viwanda vingapi sasa katika Mkoa wa Dodoma vinavyotengeneza mvinyo?

(b) Je, Mvinyo unaotengenezwa na viwanda hivyo unafikia viwango vya ubora wa kimataifa na unauzwa wapi?

(c) Je, uwezo wa viwanda hivyo unatosheleza uzalishaji wa zabibu Mkoani Dodoma hivi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Kusila, Mbunge wa Bahi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mkoani Dodoma kuna viwanda sita vinavyotengeneza mvinyo ambavyo ni kama ifuatavyo, *Bihawana Mission, Tanganyika Vine Yards, Hombolo Mission, Alko Enterprises, Makutupora Viticulture Research Centre* na *Tan Wine.*

(b) Mvinyo unaotengenezwa na viwanda hivi haujafanyiwa uhakiki kuthibitisha ubora wa bidhaa zinazozalishwa kama zinakidhi viwango vya Kimataifa. Hata hivyo Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* wako katika harakati za kuwasiliana na viwanda husika ili ukaguzi ufanyike kwa lengo la kuhakikisha kuwa ubora wa bidhaa husika unafikia kiwango kinachotakiwa.

(c) Uwezo wa viwanda hivi hautoshelezi uzalishaji wa zabibu Mkoani Dodoma kwani kwa mwaka 2002 Mkoa ulizalisha jumla ya tani 944 wakati matumizi halisi viwandani yalikuwa tani 170 tu. Kiasi kilichobaki cha zabibu kiliuzwa ndani na nje ya Mkoa kwa matumizi kama matunda.

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza kama ifuatavyo:-

Zao la zabibu ni tegemeo kubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma katika kuinua uchumi wao. Kuanzishwa kwa viwanda hivi vya kutengeneza Mvinyo ni matumaini makubwa sana kwa wananchi hawa ili waweze kufufua kilimo cha zao la Zabibu.

(a) Kwa nini imechukua muda mrefu kiasi hicho kuhakiki ubora wa Mvinyo unaotumiwa na viwanda hivi na Shirika la *TBS* kwa sababu vimeanza kuzalisha muda mrefu? *(Makofi)*

(b) Serikali inachukua hatua gani kuvilinda viwanda hivi ili viweze kujiimarisha dhidi ya ushindani mkubwa kutoka mvinyo unaoingizwa kutoka nchi za nje na hatua iliyochukuliwa na Serikali katika bajeti iliyopita ya kupunguza ushuru wa mvinyo unaoingizwa kutoka nchi za nje, ulikuwa ni kwa manufaa ya nani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa William Kusila, kama ifuatavyo:-

Kuhakiki ili kuweza kujua kwamba mvinyo wa kiwanda sita nilivyovitaja hapa unafikia kiwango cha Kimataifa, unapaswa kufanywa na *Bureau of Standard* lakini kwa matakwa ya mwenye kiwanda. Mwenye kiwanda anapozalisha bidhaa zake anapoona

sasa yuko tayari kuleta katika soko anafanya maombi ya kupewa nembo ya *Bureau of Standard.*

Binafsi nimefika *Makutopora Research Centre* kuona kama *wine* tunayozalisha inafikia kiwango na wakasema wako tayari kwenda kuhakiki na *Bureau of Standard,* tumewasiliana na *Bureau of Sandards* na wakasema wanataka maombi yatoke kwa wale watu, lakini hatimaye baada ya kuona muda unazidi kuwa mrefu *wine* nyingi zinatengenezwa mitaani na zile ambazo tumefundisha watu wa *SIDO* sasa hivi maandalizi yanafanyika na Shirika la Viwango kuhakikisha kwamba tunawapatia nembo ya *TBS* kama itakidhi matakwa ya Kimataifa.

La pili, ningependa kumjibu kuwa Serikali kwa sasa hivi tuko katika soko huria au soko huru. Hatuwezi kupiga marufuku mvinyo unaotoka nje ambapo hapa ndani bado hatujaweza kujitoshereza kwa mvinyo ambao upo. Pamoja na hayo pale ambapo viwanda hivi 6 vitakapofikia uwezo wa kuzalisha lita zinazohitajika hapa nchi nchini kwa walaji, tutajitahidi kwa njia yoyote ile kuweza kuhakikisha tunavilinda viwanda. Kwa sasa hivi bado tunahitaji sana *wine* kutoka nje kwa sababu lita ambazo tunazalisha hapa nchini ni lita 119,000 ambapo tunahitaji zaidi ya lita milioni 1,000,000 kwa mwaka.

La mwisho ameuliza kwa nini Serikali imepunguza kodi? Tumepunguza kodi ili tuweze kupata wine na kuleta ushindani zaidi, lakini bado nia ya Serikali ya kulinda viwanda vyake na kuvisaidia vingine viweze kuanza bado iko pale pale. *(Makofi)*

**MHE. HASHIM A. Z. SAGGAF:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii niulize swali moja kama ifuatavyo:-

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, je, anaelewa kuwa zabibu ambazo zinatumiwa kutengeneza mvinyo hapa Dodoma, hazikidhi haja za kuweza kutengeneza mvinyo wa kuweza kushindana na mvinyo unaotengenezwa nchi zingine kwa maana ya Kimataifa? Kwa sababu zabibu hizi mvinyo wake hauwezi kuishi zaidi ya miaka 4 na mvinyo lazima uive ndiyo unakuwa mzuri. Zabibu zetu za Dodoma baada ya miaka 4 zabibu hizi zinageuka *sickly,* je, Mheshimiwa Waziri ana mpango gani wa kuweza kusaidia kupata mbegu nyingine za zabibu ili tuweze kushindana na nchi za kimataifa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Hashim Saggaf, Mbunge wa Dodoma Mjini, swali lake kama ifuatavyo:-

Sina hakika kabisa kwamba zabibu zetu tukiziboresha zile zile zilizopo sasa hivi tutashindwa kutoa *wine* ya kufikia kiwango cha Kimataifa. *Wine* hii inayotoka katika zabibu zetu hapa Dodoma ni nzuri sana kwa wale mnaokunywa *wine.* Isipokuwa kwa ushauri wako mzuri tutawasiliana na Wizara ya Kilimo kwa kufuatilia kile Kituo cha *Makutupora Research Centre* kutazama kama tunaweza tukapata uwezekano wa mbegu nzuri tutengeneze *wine* bora ili tuweze kuuza nje na kuweza kutosheleza soko la nyumbani. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na.23

**Baiskeli zinazofaa kwa Wanawake**

**MHE. MARGARETH J. BWANA (k.n.y.MHE. ROSEMARY H. K. NYEREYE)** aliuliza:-

Kwa kuwa baiskeli ni miongoni mwa nyenzo muhimu za usafiri hususan Vijijini na kwa kuwa akina mama wengi hasa wale wa Mkoa wa Mara hutumia baiskeli hizo kwa shughuli zao mbalimbali za kiuchumi na kijamii:-

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba baiskeli nyingi zilizopo hapa nchini hazikubaliki kwa maumbile na mavazi ya akina mama walio wengi?

(b) Kama hivyo ndivyo je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa umefika wakati wa kuhakikisha kuwa baiskeli zinazotengezwa hapa nchini au zinazoagizwa kutoka nje zinazingatia maumbile na mavazi ya akina mama yaani baiskeli za kike?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kukubalika au kutokubalika kwa bidhaa yeyote ile ikiwa ni pamoja na baiskeli hutegemea matakwa ya soko. Wazalishaji na wafanyabiashara wanapoagiza bidhaa, huvutiwa zaidi kuagiza bidhaa ambazo wana uhakika wa kupata soko kubwa ili kupata faida.

Taarifa tulizonazo ni kuwa baiskeli za wanawake hazina soko kubwa nchini, ikiwa ni pamoja na katika Mkoa wa Mara. Hii inadhihirisha kwamba baiskeli za wanaume zina soko kubwa kuliko baiskeli za wanawake licha ya bei nafuu kwa baiskeli za wanawake. Utafiti unaonyesha kuwa familia nyingi, katika kuokoa gharama, hununua baiskeli moja ya kiume ambayo hutumiwa na wanaume na wanawake kuliko baiskeli ya kike ambayo wanaume hawapendelei kuitumia. Taarifa za Kiwanda cha Baiskeli cha *NABICO* kinachotengeza baiskeli za *AVON* ni kwamba kwa mwaka, kiwanda kimekuwa kikipokea oda za baiskeli za kiume kwa wingi na siyo baiskeli za kike.

(b) Pamoja na kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuhusu haja ya kuzingatia masuala ya maumbile wakati wa utengenezaji au wakati wa uagizaji wa baiskeli, hii itategemea kuwepo kwa soko la aina hizo za baiskeli. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge anashauriwa kuwahamasisha wafanyabiashara wa mkoa wake kuagiza baiskeli hizo kama lipo ili akina mama mkoani kwake wanaopendelea baiskeli za kike waweze kufaidika na huduma hii. Aidha, ningependa kutumia fursa hii kutoa wito kwa wafanyabiashara na kwa kiwanda cha *NABICO* kutafiti juu ya soko la baiskeli za wanawake na kuchukua

hatua za kuzalisha na au kuagiza baiskeli hizo iwapo soko la uhakika litathibitika kuwepo.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kutokana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mji wa Bukoba unaonekana kwamba wananchi wa pale wameridhika na wanapenda sana kupanda na kutumia usafiri wa baiskeli na kwa kuwa baiskeli zinazofaa kwa usafiri wa abiria zimedhihirika kutumika sana katika miji mikubwa ya Ujerumani: Colon, pamoja na Bonn na Berlin.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atasaidiaje kuweza kuwashawishi wafanyabiashara wanaoagiza baiskeli waweze kuagiza baiskeli ambazo ni sawa na zile zinazotumika huko Ujerumani ili ziweze kutumika hapa na kukubalika katika *system* ya Serikali ya usafiri wa baiskeli. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, kama ifuatayo:-

Tunashukuru kwa ushauri, tutawashauri wafanyabiashara waagize baiskeli za Ujerumani kama zitapata soko ili ziweze kutumika hasa Mji wa Bukoba ambapo kweli wako tayari. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 24

**Ukosefu wa Nyumba za Walimu - Siha**

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa walimu wengi wanaopangiwa kufundisha katika shule ya msingi zilizoko katika Jimbo la Siha wamekuwa wakikatisha tamaa na kutokuwepo kwa nyumba za walimu hususan katika vijijini vya Lekrimuni, Magadini, Karansi, Naibilie, Makiwaru, Donyomoruak, Ngumbaru, Olkolili mbalimbali katika kati ya Siha Magharibi vinavyokaliwa na wafugaji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za walimu kwenye maeneo niliyoyataja hasa ikizingatiwa kuwa upo mpango wa kuendeleza na kuboresha elimu ya Msingi *(MMEM)* na kwamba maeneo hayo yako nyuma sana kielimu?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge Siha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mpango wa *MMEM* 2002/2006 umeweka malengo mbalimbali ya kuboresha elimu ya msingi ikiwa ni pamoja na kuboresha na kujenga aina zote za majengo ya shule yakiwemo madarasa, nyumba za walimu, ofisi na maliwato pamoja na kununua aina zote za samani. Anayeamua umuhimu wa aina ya majengo kati ya madarasa, nyumba za walimu na ofisi ni Halmashauri husika wakati wa kuandaa mpango wake wa mwaka kwa kuzingatia hali halisi ya mahitaji ya kila shule. Serikali hutoa Ruzuku ya Maendeleo *(Development Grant)* kwa kila jengo lililopangwa kujengwa shuleni.

Katika hotuba yangu ya Bajeti niliyoitoa hapa Bungeni Julai, 2003 ukurasa wa 11, niliainisha bayana kiasi cha ruzuku kilichotolewa kwa kila Halmashauri kwa ajili ya Ujenzi wa Nyumba za walimu. Jukumu la kuamua wapi nyumba zijengwe ni la Halmashauri husika ambamo, Waheshimiwa Wabunge ni wajumbe wa Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kusisitiza Halmashauri kujenga nyumba za walimu za kutosha hasa kuanzia katika maeneo ya vijiji vya mbali ikiwa ni pamoja na maeneo ya wafugaji ili ziwe vivutio kwa walimu wanaopangiwa kwenda kufundisha katika maeneo hayo. Serikali kwa kushirikiana na wahisani itaendelea kusaidia katika ujenzi huo kwa kutoa ruzuku ya maendeleo kwa Wilaya na shule zote ili ifikapo mwaka 2006 kila shule iwe na majengo ya shule ya kutosha kwa vigezo vya utoaji wa elimu bora ambavyo ni :-

(a) Wingi darasani wasizidi wanafunzi 40 wa umri sawa.

(b) Ukubwa wa shule usizidi wanafunzi 560 vijijini (mikondo 2 x 40 x 70= 560 na 840 Mijini (mikondo 3 x 40 x 70= 840).

(c) Kila chumba cha darasa kiwe na mwalimu mwenye nyumba.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo mkao sahihi wa kulisha elimu darasani na shuleni.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali. Naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na naomba pia nichukue nafasi hii kumshukuru kwa kufanya ziara katika jimbo langu la Siha mahali ambapo alijionea matatizo haya ambayo nimeyazungumzia.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameainisha hapa na kuonyesha kwamba Halmashauri ndizo zinazotakiwa kutoa kipaumbele na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri mwenyewe alifika katika jimbo langu na kujionea matatizo hasa katika maeneo haya ya wafugaji, je, Mheshimiwa Waziri pamoja na maelekezo aliyoyatoa hapa yuko tayari kunipa barua ambayo mimi nitaipeleka katika Halmashauri yangu, ili hivi vijiji nilivyovitaja viweze kupewa kipaumbele?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Aggrey Mwanri, swali lake kama ifuatavyo:-

Kwanza namshukuru sana kwa kushukuru kwamba nilitembelea Jimbo lake, *Wabheja Kulumbha.* Hii ni kwa lugha wenye utamaduni huo. Lakini napenda na mimi nishukuru kwa ratiba nzuri niliyoandaliwa na mapokezi mazuri niliyoyapata na nitakuwa tayari kutoa barua ya maelezo ambayo Mheshimiwa Mbunge anaamini itasaidia. *(Makofi)*

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Pamoja na juhudi ambazo Serikali inajitahidi sana kujenga nyumba za walimu, lakini lipo tatizo sugu ambalo naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kulipatia ufumbuzi ni tatizo la posho za walimu ambao wanaajiriwa sasa hivi pamoja na mishahara. Tatizo hili mpaka leo ni tatizo sugu. Je, Wizara ina utaratibu gani kuondoa tatizo hilo kwa walimu kwa sababu ni matatizo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Joel Bendera, kwa kuuliza swali hili na nakushukuru pia kwa kunipa nafasi.

Napenda kukiri kwamba Serikali tunalifahamu tatizo hili ambapo walimu wapya ambao wameajiriwa moja kwa moja kutoka katika Vyuo vya Ualimu na wamepangwa katika Wilaya mbalimbali, kumekuwa na ucheleweshwaji wa kulipwa posho. Jambo hili tunajitahidi kushughulikia kwa kushirikiana na Wizara tatu husika ikiwemo Wizara yangu ambayo imetoa mafunzo kwa walimu hawa na kuwapanga katika mikoa husika, Wizara ya TAMISEMI ambao ndiyo *Vote 56* inayolipa mishahara ya walimu pamoja na Idara Kuu ya Utumishi ambao lazima uajiri wao ukamilishwe katika Wizara hiyo.

Sasa zipo taratibu ambazo ningependa kwa haraka niseme kwamba walimu hawa wakishapangwa kwenye Wilaya kunahitajika uhakika kwamba wamefika, wameripoti pale Wilayani na pia wameripoti kule shuleni. Ili utaratibu huo ukamilishwe na uhakika huo upatikane ni lazima ngazi ya Wilaya zijazwe fomu za aina tatu ambazo zinahitajika kujazwa mojawapo ni *date sheet* na nyingine kwa *Head teacher* kusema yule mwalimu ameripoti pale. Inabidi zirudishwe Idara Kuu ya Utumishi, ilinganishwe na ile orodha mama kwamba kweli walimu ni wale wenye vyeti.

Mheshimiwa Spika, sasa yamejitokeza matatizo kutoka katika baadhi ya Wilaya, majina yaliyorudishwa kutoka Wilayani siyo yale yaliyo katika orodha mama. Inabidi jambo hili lifanyiwe uchambuzi wa kina ili kuepukana na walimu ambao walimu hewa *(ghost teachers)* tunataka kuepukana na tatizo hilo kwa hiyo imebidi tuchunguze kwa ukamilifu.

Katika baadhi ya Wilaya walijikuta hawana *stationary* ya hizo *date sheet* na kadhalika. Lakini Wizara yangu ili kupunguza tatizo hilo tumeamua kwamba walimu hawa ambao wako katika walimu tarajali wakiwa kwenye vyuo kabla hawajapangwa watajaza hizi fomu tunahakikisha *stationary* zipo kwenye *TTC* watakwenda nazo kule Wilayani kinachohitajika ni kuweka sahihi na kupiga muhuri.

Kwa hiyo, tunaamini mwaka unaokuja jambo hili litasimamiwa kwa ufanisi zaidi. Kwa matatizo yaliyopo tunaendelea kushughulikia kila bidii inayowezekana. *(Makofi)*

Na. 25

**Uvujaji wa Mitihani**

**MHE. MASOUD ABDULLA SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa suala la kuvuja kwa Mitihani ya Taifa hapa Tanzania hasa ya darasa la kumi na mbili *(Form Four)* limekuwa likiendelea na kuathiri sana kushuka kwa kiwango cha Elimu na kwa kuwa uvujaji huo hatimaye kusababisha kufutwa kwa mitihani hiyo katika baadhi ya mikoa na mingine kuachwa kuendelea na mtihani wa awali:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kukomesha kero hiyo?

(b) Je, ni matukio mangapi ya namna hiyo yamejitokeza kuanzia mwaka 1995 - 2002 na kati ya hayo ni mangapi ambayo wahusika wamechukuliwa hatua?

(c) Je, Serikali ina mkakati gani wa ziada wa kudhibiti hali hiyo kwa mwaka 2003 na kuendelea?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mbunge wa Mtambile, naomba nitoe ufafanuzi ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taratibu za uendeshaji wa mitihani maana ya uvujaji wa mitihani ni kuonekana kwa karatasi ya maswali au baadhi ya maswali ya mitihani au majibu yake kwa watahiniwa au kwa watu wasiohusika kabla ya muda uliopangwa kufanyika kwa mtihani huo. Hivyo mtihani unakuwa umefanywa kwa njia za udanganyifu na baadhi ya watahiniwa. Hali hiyo inapobainika ama mitihani hiyo hufutwa yote au mitihani hufutwa tu maeneo yalioathirika na pengine matokeo ya watahiniwa waliobainika kujihusisha na udanganyifu huo hufutwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kukomesha kero hiyo, Wizara yangu kupitia Baraza la Mitihani ka Tanzania *(BAMITA)* imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

- Kuimarisha kitengo cha Uchapishaji wa *BAMITA* kwa kufanyia ukarabati mkubwa na kusimika mitambo mipya yenye uwezo wa kuchapa mitihani kwa ufanisi na usalama wa hali ya juu.

- Kuimarishwa ulinzi ndani na nje ya jengo la uchapishaji na uhifadhi wa mitihani kwa kufunga vifaa vya kisasa vyenye uwezo wa kuangalia nyendo za wafanyakazi na wageni wanaofika Ofisi za *BAMITA.*

- Kuimarisha zaidi mfumo mzima wa uchapaji, ufungaji, usambazaji na usimamizi wa mitihani kwa kushirikisha kikamilifu Vyombo vya Dola. Aidha, zimeundwa Kamati za Uendeshaji wa Mitihani ya Taifa za Mikoa na Wilaya zenye jukumu la kusimamia masuala yote yanayohusu Mitihani ya Taifa.

(b) Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 1995 hadi 2002 kumekuwepo na matukio manne ya uvujaji wa mitihani ya Kidato cha Nne katika miaka ya 1995, 1996,1997 na 1998. Waliodhihirika kuhusika walitiwa Mbaroni na Polisi na hatua za kisheria zilichukuliwa dhidi yao na watahiniwa waliogundulika kuona mtihani kabla ya wakati walifutiwa matokeo yao. Aidha, Walimu na Watumishi waliobainika kuhusika na matukio hayo walifukuzwa kazi.

(c) Mheshimiwa Spika, kufuatia uvujaji wa kupita kiasi wa mwaka 1998 na Serikali kulazimika kufuta mtihani wote wa Kidato cha Nne, hatua kali kama nilizozieleza katika sehemu (a) hapo juu zilichukuliwa. Kwa hiyo kati ya mwaka 1999 hadi 2002 halikuwepo tena tukio lolote la uvujaji wa mitihani. *(Makofi)*

**MHE. MASOUD ABDULLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Je, Serikali ina mpango wowote wa kuwasilisha Muswada Bungeni kuweka sheria ya kudhibiti kero hii? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli mpaka sasa tunaona sheria iliyopo inatosha kwa sababu kama nilivyosema baada ya hatua kali zilizochukuliwa, kosa lile halijarudiwa tena. Endapo itaonekana kuna mapungufu ya kisheria hatutasita kuchukua hatua anayoshauri Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara nyingine. Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan.

Na.26

**Ukaguzi wa Silaha za Maangamizi**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa miongoni mwa kazi kubwa ya Umoja wa Mataifa ni pamoja na Ukaguzi wa Silaha za Maangamizi zinazomilikiwa na nchi mbalimbali duniani:-

(a) Katika ukaguzi uliofanyika huko nchini Iraq, je, kuna silaha zozote za maangamizi ambazo zimegunduliwa hadi leo hii?

(b) Je, ni lini Umoja wa Mataifa utafanya ukaguzi kama huo kwa nchi ya Marekani na washirika wake?

(c) Je, ni vigezo gani vinavyotumika ili nchi iwe na kura ya *Veto?*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Tangu kuanza ukaguzi wa Umoja wa Mataifa huko Iraq mara tu baada ya Iraq kuondolewa kwa nguvu kule Kuwait mwaka 1991 na ukaguzi huo kuendelea baadaye hakuna taarifa yoyote iliyotolewa na Wakaguzi hao wa Umoja wa Mataifa inayoonesha kugunduliwa kwa silaha za maangamizi ya halaiki nchini Iraq ambazo ni pamoja na silaha za kunyuklia, silaha za kemikali na silaha za kibaolojia.

Aidha, hata baada ya Marekani na Washirika wake kuivamia Kijeshi Iraq, mwezi Mei, 2003 na kujipa jukumu la kutafuta silaha za maangamizi ya halaiki huko Iraq na kuendelea kuzitafuta silaha hizo hadi leo, bado Marekani haijatoa taaria yoyote ya upatikanaji wa silaha zozote za maangamizi huko Iraq.

(b) Marekani na washirika wake ikiwemo Uingereza, hawako chini ya vikwazo vyovyote vya Umoja wa Mataifa ambavyo huwekewe nchi pale inapokiuka mikataba ya Umoja wa Mataifa, kama vile ilivyoikuka Iraq, kwanza kwa kuivamia kijeshi Kuwait mwaka 1990 na kukataa kuondoka hadi kuondolewa kwa nguvu mwaka 1991.

Pili, kuwahi kutumia silaha za maangamizi ya halaiki kwa raia wake wenyewe miaka ya nyuma na pia kutumia silaha hizo wakati wa vita vyake na Iran. Hivyo, Marekani na washirika wake haziwezi kukaguliwa na Umoja wa Mataifa, kwa vile hazijashutumiwa kukiuka mikataba ya Umoja wa Mataifa. Nchi kama India na Pakistan zina mpango wa kutengeneza silaha za nyuklia na zinakiri kuwa na silaha hizo, lakini nchi hizo hazipo chini ya mpango wa ukaguzi kwa sababu hazikuwekewa vikwazo vyovyote na Umoja wa Mataifa.

(c) Mheshimiwa Spika, kura ya *Veto* waliyonayo wananchama wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa iliwekwa na wanzilishi wa Umoja huo na ambao ndio waliokuwa washindi wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia.

Umoja wa Mataifa uliundwa mwaka 1945 baada ya makubaliano ya Dola zilizoshinda vita ya pili vya dunia na kupendekeza kuundwa kwa chombo hicho cha Umoja wa Mataifa mwaka 1943. Dola hizo ni Marekani, Urusi, Uingereza na Uchina ambazo ndizo zilizotoa pendekezo la kuundwa kwa Umoja wa Mataifa na pia kupendekeza na kuipitisha Katiba ya Umoja wa Mataifa ambayo ilizipa Dola hizo pekee kura ya *Veto.*

Jamhuri ya Watu wa China iliiingizwa kwenye kundi la Mataifa yenye kura za *Veto* mwaka 1971 baada ya kukubaliwa kuwa mwanachama kamili wa Umoja wa Mataifa na hivyo kuiengua iliyokuwa inaitwa Jamhuri ya Taifa la Uchina ambayo sasa

inaitwa Taiwan na ambayo ilipewa nafasi ya kushika kiti hicho kwa muda tu. Nchi nyingine zote zilizotia saini Mkataba wa kuundwa kwa Umoja huo zilikubali Katiba hiyo. Hakuna vigezo vingine isipokuwa vile vilivyowekwa vya kujiunga tu na Umoja wa Mataifa na cha muhimu ni kukubali Katiba hiyo.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Spika, lakini nchi kama Marekani, imeshatumia silaha kama hizo Hiroshima na Vietnam. Je, Mheshimiwa Waziri anazungumza nini kuhusu hilo? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Anza vizuri Mheshimiwa Parmukh Singh, sikukusikia vizuri.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko)*

Lakini nchi kama Marekani, imeshatumia silaha kama hizo huko Vietnam na Hiroshima. Je, Mheshimiwa Waziri anazungumza nini kuhusu hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Marekani ilitumia bomu la nuklia kule Hiroshima, lakini bomu hilo lilitumiwa kabla ya kuundwa Umoja wa Mataifa. Lilitumiwa katika Vita vya Kwanza vya Dunia na kwa kweli lilikuwa kabla vita vya pili vya dunia.

**SPIKA:** Waziri, zungumza na Spika, usizungumze na watu wengine. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Samahani Mheshimiwa Spika, lakini wakati huo bado mikataba hii ilikuwa haijawekwa. Ni kweli lilikuwa ni janga kubwa, limeangamiza watu wengi, athari zake zimebakia mpaka sasa vizazi, vijukuu na vitukuu.

Kwa hiyo, Umoja wa Mataifa haukuweza kwenda kukagua au kuwekea vikwazo Marekani. Lakini pamoja na hiyo Marekani kwa sababu ya kura ya *Veto* iliyojipa na kura walizojipa wengine wale, azimio lolote lile ambalo litataka kuiwekea vikwazo litapingwa. Ndiyo maana sasa hivi kuna juhudi kubwa ya kutaka kwenda mbio kurekebisha Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ili kura hii ya *Veto* ama iondolewe au ipunguzwe nguvu zake au wapewe Wajumbe wengine zaidi. Lakini kwa sababu ya nguvu hizo walizojiwekea Marekani, hata ufanye nini siku zote watapinga na haitaweza kukaguliwa au kuwekewa vikwazo na swali hilo hilo kuhusu Vietnam.

**SPIKA:** Msemaji Mkuu wa Upinzaji kuhusu Mambo ya Nchi za Nje, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, swali la nyongeza.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, katika majibu yake ya msingi amesema kuwa Marekani mpaka sasa haijashutumiwa kuwa inavunja mikataba ya Umoja

wa Mataifa, kitendo cha kuandamana watu karibu dunia nzima kupinga vita vile vya Iraq, haoni yeye kuwa sasa hizo pekee ni shutuma za kufanya Marekani na washirika wake waweze kushutumiwa na kama inawezekana wachukuliwe hatua za Kimataifa juu ya jambo hili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Malizia kujibu swali la mwisho la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NCHI NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mataifa mengi duniani ikiwemo Tanzania yanapinga kabisa vita vilivyofanywa na Marekani kushambulia Iraq kwa sababu havikuwa halali, havikufuata taratibu za Umoja wa Mataifa, vimekiuka utaratibu.

Lakini nadhani tunachozungumzia hapa ni Umoja wa Mataifa kuiwekea vikwazo Marekani, siyo dunia na watu wengine. Ndiyo maana nikasema kwa sababu Marekani ina nguvu ya kura ya *Veto,* siku zote ikitaka kuwekewa kikwazo chochote itatumia kura hiyo. Lakini hiyo haina maana kwamba dunia nzima na watu wakiandamana barabarani, kila mahali kupinga, haina maana kwamba Marekani haishurumiwi, Marekani inashutumiwa na nchi nyingi zinashutumu, zimo ndani ya Umoja wa Mataifa vile vile.

**SPIKA:** Maswali kwa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Talala Mbise.

Na.27

**Huduma ya Benki - Wilaya ya Arumeru**

**MHE. TALALA B. MBISE** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Jimbo la Arumeru Mashariki kulikuwa na huduma za Benki ya Biashara *Usa River* - Mji Mkuu wa Wilaya ya Arumeru:-

(a) Je, ni lini huduma hiyo iliondolewa na ilikuwa ni kwa sababu zipi na Serikali imewawekea wananchi utaratibu gani wa kupata huduma hiyo hasa baada ya kuondoa Benki iliyokuwepo?

Kwa kuwa Mji wa *Usa River* na Miji mingine midogo kama vile Ngarenanyuki, Leguruki, King'ori Madukani, Kikatiti, Tengeru na Mbuguni inakua kwa kasi kubwa, je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka huduma za Kibenki kwenye maeneo hayo ili kupunguza adha wanayopata wananchi ya kufuata huduma hiyo Mjini Arusha?

(b) Je, Sera ya Huduma za Kifedha au Kibenki inasema nini juu ya *Mobile Banking Services* na je, ni taratibu zipi zinatakiwa zifuatwe ili kutoa huduma hiyo na ni sheria gani zinazohusika na kulinda biashara kama hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mbunge wa Arumeru Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Tawi la ilivyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara *(NBC), Usa River* lilifungwa mwaka 1996 katika kuitayarisha Benki hiyo kubinafsishwa.

Katika kipindi hiki, Matawi yote ambayo yalionekana dhahiri kuwa yanapata hasara yalifungwa. Hali iliendelea kuwa hivyo hata baada ya kubinafsishwa. Kufuatia kujitoa kwa Serikali katika biashara ya mabenki, uendeshaji na utoaji wa huduma za kibenki katika sehemu mbalimbali sasa unafanywa na mabenki binafsi ambayo uwekezaji wake hutegemea mazingira yanayowezesha na uwepo wa biashara katika maeneo husika.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Benki Kuu imewaweka wananchi utaratibu wa kujianzishia Benki zao wenyewe chini ya mpango wa Benki za Wananchi. Huduma hii ni muhimu hasa kwenye zile sehemu ambazo hazijaweza kuwavutia wawekezaji wakubwa. Tayari wananchi katika sehemu mbalimbali wameshajianzishia Benki zao chini ya mpango huu, zikiwemo zile za Beni ya wananchi wa Mwanga, Benki ya Wananchi Mufindi, Benki ya Wananchi ya Dar es Salaam na nyinginezo. Mheshimiwa Mbunge anashauriwa atumie utaratibu huu kuanzisha Benki huko *Usa River* na sehemu nyingine za Wilaya ya Arumeru.

(c) Mheshimiwa Spika, kimsingi sheria ya mabenki na Taasisi za fedha haizuii huduma za *Mobile Banking* na mabenki kupitia matawi yao yanaruhusiwa kutoa huduma hizo ilimradi tu usalama wa wateja na mali zao na ia mali za Benki utazingatiwa wakati wote wa utoaji wa huduma hizo.

Ukuaji wa huduma za *Mobile Banking Services* haujakuwa na mafanikio mazuri hata hivyo na hii ni kutokana na wawekezaji katika sekta ya kibenki kutoona manufaa ya kibiashara katika utoaji wa huduma hizo. Serikali itaendelea kushawishi mabenki yaliyopo kutoa huduma za *Mobile Banking Services* katika maeneo mbalimbali ili kuziba pengo la huduma za kibenki katika maeneo ya Vijijini.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu. Kwanza kuhusu mazingira ambayo tunawekewa ili tuweze kupata huduma za kibenki, mojawapo ni kwamba wananchi wa Arumeru na hasa kwenye Jimbo langu wangetazamia kwamba Benki ya Wananchi *National Microfinance Bank (NMB)* ingekuwa tayari kutuanzishia Tawi hilo *Usa River.* Je, Benki hiyo ya *NMB* ambayo mpaka sasa haijapata leseni ya kujiendesha kama Benki kamili, itapata lini leseni hiyo ili ipate motisha ya kuja kuanzisha hilo tawi la huduma za kibenki huko *Usa River? (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, *NMB* kwa yale matawi ambayo imeshayafungua bila shaka mwote humo imeangalia mzunguko wa fedha na hali ya biashara katika sehemu mbalimbali hizo. Hata hivi sasa hata kama haina leseni, bado itakapotaka kufungua tawi la *NMB* -

Arumeru, itafanya hivyo kutokana na leseni iliyokuwanayo hivi sasa pale tu itakapoona kwamba kuna mzunguko wa fedha wa kutosha na kuna biashara ya kutosha katika Wilaya ya Arumeru.

**SPIKA:** Bado nina maswali matatu na muda uliobaki ni kidogo. Tunaendelea Mheshimiwa Estherina Kilasi.

Na.28

**Sheria ya Pensheni ya Mashirika ya Umma**

**MHE. ESTHERINA KILASI** aliuliza:-

Kwa kuwa Bunge lilipitisha mabadiliko kadhaa katika Sheria ya Pensheni ya Mashirika ya Umma (Sheria Na.14 ya 1978) kikiwemo kifungu cha 44 kinachositisha malipo ya kila mwezi ya mwanachama aliyestaafu kabla ya muda wa kustaafu kisheria; na kwa kuwa kuna wanachama ambao ajira zao zilikoma kabla ya umri wa kustaafu na walikuwa wanalipwa malipo ya kila mwezi na kwa kuwa sheria hiyo inamruhusu mwanachama kuendeleza michango ya kila mwezi mpaka atakapofikia umri wa kustaafu kisheria (miaka 55):-

(a) Je, kuna wanachama wangapi walioathirika na kusitishwa malipo ya kila mwezi na ni taratibu zipi zilitumika kuwajulisha wanachama ili wajue kiasi ambacho watalipwa iwapo wataendeleza michango hiyo?

(b) Je, Serikali inasema nini kuhusu wanachama waliostaafu chini ya miaka 55 na wameshindwa kuendeleza michango kwa kukosa ajira nyingine?

(c) Je, tangu sheria hiyo ianze kutekelezwa kuna malalamiko yoyote yaliyojitokeza kutoka kwa wanachama wa *PPF* na kama yapo ni yapi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Kutokana na mabadiliko makubwa ya kiuchumi, yaliyoikumba Tanzania kuanzia mwishoni mwa miaka ya themanini, Sheria nyingi nazo zilihitajika kurekebishwa zikiwemo zile za pensheni ili kukidhi mabadiliko hayo. Ilikuwa ni jambo lisiloepukika kuifanyia marekebisho Sheria ya *PPF* Na.14 ya mwaka 1978 ili kuwezesha Mfuko huu kujiendesha katika mazingira yanayobadlika kwa kasi. Hata hivyo mabadiliko haya yamekuwa ni ya kitaalam zaidi kwa kuzingatia misingi ya Mifuko ya Mafao ya uzeeni ya kuchangia *(contribution schemes).* Kwa kutambua dhamana ambayo Mfuko huu unabeba katika jamii, Serikali iliamua kuleta Muswada wa marekebisho ya sheria iliyounda mfuko

huu ili kuunusuru kwenye hatari ya kufilisika na kusababisha hasara kubwa sana kwa wanachama wote na Serikali ambayo ni mdhamini wa *PPF*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wanachama waliohusika na mabadiliko hayo ni wale waliokuwa hawajafikia umri wa miaka 55 toka zoezi hilo lianze tarehe 01 Novemba, 2002. Usitishwaji huo uligusa wanachama 21,487 lakini hadi kufikia Septemba, 2003 kiasi cha wanachama 1,429 zaidi walianza kulipwa pensheni zao baada ya kufikisha umri wa miaka 55. Hadi kufikia Desemba, 2003 idadi ya watakaokuwa wametimiza umri wa kisheria wa kulipwa pensheni wataongezeka na kufikia idadi ya 11,291.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kabla ya utekelezaji wa mabadiliko hayo *PPF* ilihakikisha kuwa wanachama walitumiwa na kupata barua kupitia matawi yao ya Benki zikieleza kuwa malipo yao yangesimamishwa kutokana na marekebisho ya Sheria Na.25 ya 2001 ambayo pamoja na mambo mengine ilifanya marekebisho ya kifungu cha 26 ambacho kimesitisha ulipwaji wa mafao ya uzeeni yaani pensheni ya kila mwezi kwa wanachama ambao hawajafikia umri wa miaka 55.

Mheshimiwa Spika, kuhusu taratibu zilizotumika kuwataarifu wanachama kiasi ambacho watalipwa endapo wangeendeleza uanachama, Mfuko hauwezi kutoa takwimu halisi kwa sasa. Ili kujua kasi ambacho mwanachama atapata inabidi kuangalia muda ambao mwanachama amechangia katika mfuko pamoja na mshahara atakaokuwa nao wakati wa kustaafu. Kiasi cha mafao ya mwanachama kitajulikana baada ya kufanya mahesabu kwa kutumia kanuni maalum ukizingatia muda na mshahara wa mwanachama atakaokuwa nao wakati anastaafu baada ya kuendeleza uanachama wake.

(b) Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma *(PPF)* ulianzishwa ili kutoa mafao ya pensheni kwa watumishi watakaostaafu baada ya kutimiza umri wa kustaafu kisheria. Aidha, pensheni tafsiri yake ni mafao alipwayo mwanachama kwa kutokuwa na uwezo wa kufanya kazi ama kwa umri au kwa ugonjwa. Kabla ya mabadiliko ya Sheria ya *PPF* kufanyika, Mfuko ulijkuta ukilipa mafao ya uzeeni kwa kundi lingine la wanachama wake kinyume na misingi ya pensheni. Kundi hili ni la wananchama wenye uwezo wa kufanya kazi, lakini hawana kazi.

Kimsingi watu wa jinsi hii hupaswa kushughulikiwa na Serikali na mafao yao hujulikana kwa jina la mafao ya kutokuwa na kazi *(unemployment benefit)*. Hata hivyo, ni nchi zilizoendelea duniani ambazo zimeweza kutoa mafao ya aina hii.

(c) Mheshimiwa Spika, malalamiko mbalimbali yameletwa kutoka kwa wanachama kuhoji uhalali wa Serikali kusitisha ulipwaji wa mafao ya uzeeni kwa wanachama vijana ambao hawajafikisha umri wa kustaafu, kupitia kwenye barua na hata kwenye vyombo vya sheria. Lakini kwa kuwa suala hili liko Mahakamani haitakuwa busara kulizungumzia kwa undani zaidi, ila mfuko unaendelea kutoa elimu ya pensheni kwa wanachama na wadau mbalimbali kupitia Semina ambazo zinaelimisha jamii kuhusu maana halisi ya pensheni ukizingatia kuwa hata katika mifumo mingine ya pensheni

duniani kote mwanachama halipwi mafao ya uzeeni mpaka awe amefikia umri wa uzee kisheria. Aidha, wengi wa wadau wanapoelimishwa huelewa vizuri kuhusu dhana hii ya pensheni.

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kutokana na mawasiliano kuwa yana matatizo, mifuko ambayo inatumika hasa baada ya kubadilishwa Benki na wastaafu wengi kwenda sehemu ambazo siyo rahisi kuwafikishia taarifa.

Je, Waziri haoni kwamba kunatakiwa kufanywe utaratibu wa kufuatilia kupitia *record* zao kujua wale wastaafu ambao mpaka sasa hawajawasilisha mawasiliano yao au hawajatoa taarifa ya madai yao ili waweze kuwafikia na wajue ni kiasi gani wanadai na lini wanatakiwa kulipwa? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa Serikali wakati wa kipindi cha Bajeti iliahidi kuwafikiria wale wastaafu ambao walichukua malipo kwa mkupuo; je, ni lini wastaafu hawa wataanza kulipwa hasa hawa wazee ambao bado wanaishi mpaka sasa na kama wameanza kulipwa ni utaratibu gani wa kufuata ili waweze kulipwa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, tutawashauri *PPF* wafanye hivyo ili kuhakikisha kwamba wananchi au wadau wao wanapata huduma kama inavyostahili na taarifa zote zinazowahusu zinapatikana kwa wakati ili wasiwe na shida ya kupata pensheni zao.

Kuhusu mkupuo, kama tulivyokuwa tumeeleza wakati wa Bajeti kwamba Serikali inafikiria kuangalia na hali ya mfuko ilivyo na kama utakumbuka Mheshimiwa Mbunge, tulitaja idadi inayohusika na fedha ambazo zinahitajika ili taratibu hizi ziweze kufanyika. Kwa hiyo, hili bado tunalifikiria na limo katika fikra zetu kuhakikisha kwamba hawa wastaafu hapo baadaye hali yao vile vile inazingatiwa na inakuwa bora. Ahsante.

Na.29

**Uchakavu wa Reli ya Kati**

**MHE. ALLY A. KARAVINA** aliuliza:-

Kwa kuwa miundombinu ya Reli, hususan Reli ya Kati ni muhimu sana kwa uchumi wa Tanzania na nchi za Maziwa Makuu; lakini kuna uchakavu mkubwa hasa wa reli yenyewe na madaraja ambayo mengi yalijengwa tangu enzi ya utawala wa Mjerumani:-

(a) Je, ni lini Serikali itabadilisha reli hiyo na kuweka reli mpya yenye uzito mkubwa?

(b) Je, ni lini Serikali itajenga upya na kukarabati madaraja yaliyopo ili yaweze kuhimili injini na treni zenye uzito mkubwa zaidi hasa zile za mizigo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Amani Karavina, Mbunge wa Urambo Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa miundombinu ya reli, hususani Reli ya Kati kwa uchumi wa nchi. Kutokana na umuhimu huo, kumekuwepo na mkakati maalum wa kuboresha njia hii pamoja na nyenzo nyingine zikiwemo injini na mabehewa. Reli ya Kati inayoanzia Dar es Salaam hadi Kigoma ina umbali wa Kilomita 1,252. Katika jitihada za muda mfupi na mrefu wa kuboresha njia hii, baadhi ya maeneo ya reli yaliyokuwa mabaya zaidi kutokana na uchakavu yalikwishakarabatiwa kwa kubadilisha reli za uzito mdogo wa paundi 56 kwa yadi na kuweka zilizo na uzito mkubwa za paundi 80 kwa yadi.

Sehemu ambazo zimekwishabadilishwa na kutandikwa reli za uzito wa paundi themanini *(80lb)* kwa yadi ni kama zifuatazo:-

Pugu - Mpiji kilomita 22; Mzaganza - Kintinku kilomita 225; Makutupora - Itigi kilomita 79 na Malongwe - Igalula kilomita 73. Jumla ya Reli ya Kati iliyokarabatiwa ni kilomita 399

Katika malengo ya muda mrefu, Serikali inatarajia kuimarisha Reli ya Kati kwa kutandika reli nzito zaidi ya paundi 110 kwa yadi kati ya Dar es Salaam na Morogoro ambazo ni urefu wa kilomita 202 zenye sehemu ambayo hupitisha reli nyingi zaidi. Fedha zinazohitajika kwa kazi hiyo ni Dola za Marekani milioni 69. Umbali utakaobaki ambao haujakarabatiwa, wenye urefu wa kilomita 650 unatarajiwa kutandikwa reli za uzito wa paundi 80 kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 65. Uimarishaji huu wa Reli ya Kati utafanywa kwa awamu kutegemea na upatikanaji wa fedha.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli madaraja mengi yaliyoko kwenye njia ya reli yalijengwa wakati wa utawala wa Mjerumani kati ya mwaka 1905 na 1914 yakiwa na uwezo wa kubeba mzigo-tairi wa tani kumi. Baadaye madaraja haya yaliimarishwa na kuyawezesha kubega mzigo-tairi *(axle load)* kati ya tani 12 na tani 18. Katika Reli ya Kati kuna jumla ya madaraja 1,271 ambapo 1,166 yana uwezo wa kupitisha mzigo-tairi kati ya 12 na tani 18 na yaliyobaki 105 yaliimarishwa kuweza kupitisha mzito-tairi 25. Ili kuyaimarisha madaraja 1,166 yaliyobaki kufikia kiwango cha kupitisha mzigo-tairi tani 25 zinahitajika Dola za Marekani milioni 66.4. Fedha hizi ni nyingi na upatikanaji wake ni mgumu hivyo uimarishaji wa madaraja haya pia utafanyika kwa awamu kutegemea na upatikanaji wa fedha hizi.

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili mafupi tu ya nyongeza.

Wakati Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, akihutubia Taifa mwishoni mwa mwezi Agosti, alizungumzia pia jinsi ambavyo nchi yetu iko katika *position* nzuri sana kuvuna uchumi wa jiografia. Je, Serikali ina mikakati gani katika *vision* hiyo ya *central corridor* na kama alivyoelezea Rais katika kuimarisha miundombinu huo na mingine katika kutimiza azma hiyo ambayo alieleza?

Swali la pili, kwa kuwa uchakavu huo wa madaraja unafanya Shirika la Reli liweze kununua injini ghali sana ambayo ni *special* badala ya kununua zile ambazo ni *axle load* tani 25; Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa ukarabati wa madaraja hayo kabla ya ubinafsishaji kufanywa?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Ally Karavina, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba pesa zitakapopatikana ukarabati utafanywa na ukarabati tumekusudia kuufanya kwa awamu kutokana na hali ya fedha ilivyo.

Pili, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Ally Karavina, kwamba katika masuala ya *Central Corridor* ni suala zima la kurekebisha Reli ya Kati iweze kuhimili uchukuzi wa ubebaji wa mizigo na pia ni pamoja na kuboresha barabara ambayo kutakuwa na *linkages* na kufanya uchumi wa eneo hili uwe ni wa kuaminika zaidi na hivi sasa juhudi zinavanywa kuona hili linatekelezwa.

Na.30

**Usafiri wa Abiria Kati ya Tanga na Pemba**

**MHE. KHAMIS ALI SALEH** aliuliza:-

Kwa kuwa shida inayowapata wasafiri (abiria) wanaotoka na kurudi Pemba kwenda Tanga kwa kutumia Bandari zote mbili za Mkoani na Wete ni vyombo vya usafirishaji na kwa kuwa imekuwa kero kubwa sana kwa kulazimika kusafiria vyombo vya mbao (jahazi na mashua) visivyo na uhakika ambavyo huwasababishia wasafiri/wafanyabiashara kupoteza mizigo na hata maisha yao:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha usafiri wa kutumia boti za mashine zenye uhakika na safari?

(b) Je, ni ajali ngapi (maafa) zinazotambulika zimetokana na vyombo hivyo vya mbao (jahazi na mashua) visivyo na uhakika wa usalama wa abiria na ni fidia gani imetolewa kwa walioathirika?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khamis Ali Saleh, Mbunge wa Mgogoni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kuwa usafiri kati ya Bandari ya Tanga na Pemba umekuwa siyo wa kuridhisha kutokana na kukosekana kwa vyombo vya uhakika na salama. Hata hivyo, Sera ya Serikali kwa sasa ni kuwezesha watu binafsi au makampuni kutoa huduma za biashara ikiwa ni pamoja na uchukuzi baharini. Hivyo Serikali itaendelea kuwashawishi wawekezaji kutambua kuwa upo umuhimu wa kuwa na boti salama za mashine kati ya Pemba na Tanga ili kuimarisha usalama wa watumiaji wa vyombo hivyo.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge, kuwa juhudi za Serikali kuwashawishi wawekezaji binafsi kuboresha usafiri kati ya Tanga na Pemba zimeanza kuzaa matunda kwa upande wa usafiri wa safari za ndege. Hivi sasa kampuni ya Ndege ya *Coastal Travel* inatoa huduma kati ya Tanga na Pemba kila siku na ndege hiyo huanza safari yake kutoka Dar es Salaam, Zanzibar, Pemba na Tanga na kurudi.

Kwa hiyo, kwa njia hiyo tena Tanga na Pemba na Dar es Salaam kwa sasa napenda nikiri kuwa baada ya meli ya *Ms SEPIDEH* kujitoa katika utoaji huduma kwenye njia hii, hali ya usafiri imekuwa si ya kuridhisha kama alivyobaini Mheshimiwa Mbunge na tunaahidi kuendelea kuwashawishi wawekezaji ili waweze kuona umuhimu wa kuboresha usafiri kati ya Tanga na Pemba.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda pia nikiri kuwa hakuna kumbukumbu sahihi za idadi ya ajali zilizowahi kutokea kutokana na vyombo kusafiri bila kutoa taarifa na kutokana na kutokuwepo kwa mawasiliano ya kuaminika kati ya vyombo hivyo na bandari zetu. Hata hivyo, Wizara yangu itaendelea kufanya mawasiliano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa lengo la kuhakikisha kuwa vyombo vidogo vya majini vinakaguliwa na katika ubora unaotakiwa na vile vinavyosafirisha abiria kuwa na redio kwa ajili ya kutoa taarifa za maendeleo ya safari zao wakiwa baharini.

**MHE. KHAMIS ALI SALEHE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa hivi sasa kuna utaratibu wa Boti ya *Sea Star* kutoka Unguja kwenda Pemba. Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kuitaka kampuni hiyo kupeleka boti hiyo Pemba-Tanga angalau mara moja kwa wiki ili kuwapunguzia kero wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli hivi sasa Kampuni ya *Sea Star* imeanza kutoa huduma kutoka Zanzibar kwenda Pemba na ipo Kampuni moja ilitoa tu ahadi ya kufanya hivyo lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba tutaendelea kuwasiliana nao kuwaomba waweze kuona umuhimu wa kupeleka meli hii iwapo *qualification* ya meli ile itaweza kuhimili mawimbi ya kwenda Tanga. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamemalizika. Matangazo ya vikao vya Kamati vilivyopangwa leo ni kama ifuatavyo:-

Kwanza wageni waliopo kwenye *Gallery* ni wale wale niliowatambulisha jana, bado tunaendelea mazungumzo nao. *(Makofi)*

Pili, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo, anaomba Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo Jumatano tarehe 5 Novemba, 2003, mara baada ya kipindi cha maswali na majibu. Kikao kitafanyika kwenye chumba cha Kamati Namba 231 ghorofa ya pili kwa lengo la kukamilisha Muswada wa Sheria wa Vyama vya Ushirika. Hiyo ni Kamati ya Uwekezaji na Biashara.

Kamati ya Miundombinu, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, anaomba Wajumbe wakutane leo saa 5 katika ukumbi Namba 216, ghorofa ya pili kwa madhumuni ya kukutana na ujumbe wa *TTCL,* kama hizo mbili, baada ya hapo tunapenda kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba kile kikosi kinachoshughulikia ujenzi wa Ukumbi wetu mpya kimeshawasili Dodoma kwa ajili ya *Soil Testing* na mambo mengine yanayotakiwa kufanyika kabla ya kuweka jiwe la msingi.

Kwa ajili hiyo, kuanzia kesho tarehe 6 Novemba, 2003 wataanza kazi. Kwa ajili hiyo, tutawatengenezea Waheshimiwa Wabunge mahala pengine pa ku-*park* magari hapo sasa hapafai tena ku-*park* magari. Kwa hiyo tutawaelekeza, ma-*staff* wetu watawaelekeza baadaye. Kuanzia kesho magari yata-*park* wapi.

La mwisho kama Waheshimiwa Wabunge mtakavyokumbuka, nimeshajenga mazoea ya kutambua Wabunge miongoni mwetu, wanaojiendeleza kitaaluma, kielimu na kupata mafanikio. Sasa leo napenda kuwatambua Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu ambaye hivi majuzi ametunukiwa Shahada ya Sheria *(LLB)* ya Chuo Kikuu Huria cha Dar es Salaam. Amekuwa *learned brother. (Makofi/Kicheko)*

Wa pili ambaye napenda kumtambua leo na amewasilisha cheti chake kwangu kuwa kinatoka nje ni Mheshimiwa Mzindakaya. Cheti chake kinasema hivi: *"Califonia Church Christian University, has conferred upon Christian, Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, the Honorary Degree of Doctor of Humanity. (Makofi)*

*In formal recognition of his outstanding achievement and influence in his hosted service to humanity."* Kwa hiyo, amepewa *Honorary Degree* ya *Doctor of Humanity.* Sasa hata wanaopewa *Honorary Degree* wanaitwa ma-*Doctor* kama tunavyomwita Dr. Malecela. Dr. Mzindakaya, kuanzia leo. *(Makofi/Kicheko)*

Mwisho wa matangazo.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Viwango vya Mbegu wa Mwaka 2003
### *(The Seeds Bill, 2003)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Subiri kidogo, sasa namwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Mbegu ya mwaka 2003 iitwayo *The Seeds Act, 2003* sasa usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi pamoja na Wajumbe wa Kamati yake kwa uchambuzi wao wa kina wa Muswada na kwa mapendekezo ambayo nimeyazingatia katika kuboresha Muswada huu.

Mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika nyongeza ya marekebisho ya Muswada ambayo Waheshimiwa Wabunge wamekwishakugaiwa.

Aidha, napenda kuwashukuru wadau mbalimbali wakiwemo wawakilishi wa wakulima, watafiti, wazalishaji na wafanyabiashara wa mbegu kwa michango yao waliyoitoa ya kuunga mkono Muswada huu wakati walipokutana na Kamati ya Bunge ya Ardhi na Kilimo tarehe 20 Oktoba, 2003.

Mwisho, naomba kwa ruhusa yako, nichukue nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala na Katibu wa Wizara, Ndugu Wilfred Ngirwa na watumishi wote wa Wizara ya Kilimo na Chakula na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambao wameshiriki kikamilifu katika kuandaa Muswada huu hadi kuufikisha katika hali yake ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Muswada ulioko mbele ya Bunge lako Tukufu unakusudia kufuta Sheria ya Mbegu ya mwaka 1973, *The Seeds (Regulation of Standards) Act, of 1973.* Ili kuondoa mapungufu makubwa yaliyopo kwenye sheria hii.

Aidha, Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria mpya itakayokidhi matakwa ya soko huru na kuweka mfumo wa udhibiti wa ubora wa mbegu utakaotambulika kisheria na ambao utasimamia uzalishaji, uingizaji kutoka nje ya nchi, usambazaji wa mbegu za kilimo ndani ya nchi na uuzaji nje ya nchi wa mbegu zilizozalishwa hapa nchini. Kwa kifupi Muswada huu utasimamia masuala yote yanayohusiana na biashara ya mbegu.

Mheshimiwa Spika, ulazima wa kutunga sheria mpya ya mbegu unatokana na Serikali kuruhusu sekta binafsi kujihusisha na biashara ya mbegu mwaka wa 1993. Kabla ya mwaka huo shughuli za uzalishaji, ununuzi, uuzaji na usambazaji wa mbegu zilikuwa zikifanywa na Serikali kupitia kwenye Kampuni pekee ya mbegu inayojulikana kama *The Tanzania Seed Company* ama *TANSEED* ambayo ilikuwa na ukiritimba wa kushughulikia masuala yote ya mbegu hapa nchini.

Katika kipindi chote cha uhai wake *TANSEED* haikuweza kukidhi mahitaji ya mbegu ya nchi na mwaka wa 2001 *TANSEED* ilifikia hali mbaya ya kushindwa kabisa kutekeleza majukumu yake kutokana na udhaifu katika uendeshaji uliosababisha kampuni hiyo ipate hasara kubwa na kuifanya ishindwe kubeba madeni ya wazalishaji wa mbegu kwa mkataba.

Hatua ya kuruhusu sekta ya binafsi kujishughulisha na biashara ya mbegu haikuambatana na mabadiliko katika Sheria ya Mbegu ya mwaka 1973. Idadi ya makampuni binafsi yaliyojitokeza na yanayoendelea kujitokeza kufanya biashara ya mbegu hapa nchini imekuwa ikiongezeka na kumekuwepo na matatizo katika udhibiti wa ubora wa mbegu yanayotokana na upungufu katika sheria, Kanuni na taratibu zilizowekwa na Serikali za kusimamia na kudhibiti ubora wa mbegu hizo.

Kwa mfano, kumekuwepo na uingizaji wa mbegu kiholela ambao umesababisha kuingizwa nchini kwa magonjwa mbalimbali ya mimea. Kuna mbegu nzuri sana ya Songea ilikuwa inaitwa *Songea Select* ambayo sasa hivi haifai kwa sababu imeshambuliwa na ukungu.

Mheshimiwa Spika, Sheria itakayotokana na Muswada huu, itaweka utaratibu utakaoiwezesha Sekta ya binafsi kufanya shughuli za kuagiza kutoka nje, kuzalisha, kuandaa, kuuza, kununua na kusambaza mbegu bora hapa nchini. Muswada huu pia utaweka utaratibu wa kusajili mbegu na wazalishaji na uuzaji wa mbegu na hivyo kuwezesha kufahamika na kudhibitiwa kwa ubora wa aina za mbegu zitakazosambazwa na kuuzwa hapa nchini.

Madhumuni ya Muswada huu ni kufuta Sheria ya Mbegu ya Mwaka 1973 na kutunga Sheria mpya itakayoitwa *The Seeds Act, 2003* itakayokidhi mabadiliko ya kijamii na kiuchumi wa soko huria la uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa mbegu nchini. Sheria hii itadhibiti biashara ya mbegu baada ya makampuni yanayojihusisha na mbegu hapa nchini kuruhusiwa kushiriki katika kuzalisha, kuandaa na kuuza mbegu ndani na nje. Aidha, Sheria mpya itaipa Serikali pamoja na Taasisi zake uwezo wa kudhibiti ubora wa mbegu hizo.

Muundo wa Muswada, Muswada huu umegawanyika katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza inaeleza mambo ya kiutangulizi yaani jina fupi la Sheria na tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hiyo na tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyotumika katika Muswada.

Sehemu ya pili, inayojumuisha vifungu vya 3 hadi 12 inahusu uanzishaji au uteuzi wa watekelezaji wa Sheria. Kifungu cha tatu cha Muswada kinaanzisha Kamati ya Mbegu ya Taifa ambayo itakuwa na Wajumbe 10. Wajumbe hao ni pamoja na Wataalam kutoka Taasisi za Serikali zinazohusika na masuala ya mbegu na wajumbe wengine wa Kamati watateuliwa na Waziri wakiwawakilisha wafanyabiashara na wauzaji wa mbegu.

Jukumu kuu la Kamati hii ni kukutanisha wadau wa Sekta ya mbegu ili kujadili masuala muhimu yanayostahiki uzalishaji na usambazaji wa mbegu na kuishauri Serikali ipasavyo. Kamati pia itatoa maoni na ushauri wake juu ya masuala ya utekelezaji na urekebishaji wa sera ya mbegu. Utajiri wa mbegu na masuala yoyote ya jumla yanayohusiana na Sekta ndogo ya mbegu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili vile vile inahusu uundaji wa Kamati ndogo ndogo za Kamati ya Mbegu ya Taifa kushughulikia masuala maalum yanayohusu mbegu. Uteuzi wa watendaji mbalimbali watakaosimamia sheria ya mbegu wakiwemo Wakaguzi na Wahakiki wa Mbegu, ubora wa mbegu yaani *Seed Inspectors* nao pia utafanyika chini ya kifungu cha nane cha sehemu hii.

Aidha, sehemu hii inaanzisha kisheria taasisi ya Mbegu ya Taifa itakayojulikana kama *The Tanzania Official Seed Certification* na kuipa majukumu ya kusimamia ubora wa mbegu ambao ni pamoja na kufanya ukaguzi wa mashamba ya mbegu, kufanya ukaguzi wa maabara na kuthibitisha ubora wa mbegu zinazofaa kupandwa hapa nchini. Taasisi ya Mbegu ya Taifa yaani *TOSCA* ilianzishwa mwaka 1973 na Makao yake Makuu yako Morogoro. Taasisi hiyo ina matawi Iringa na Arusha.

Hata hivyo, Taasisi hii haijawahi kuanzishwa kisheria. Kuna mkanganyiko uliotokea, Sheria ilimtaka Waziri aanzishe Taasisi hii kupitia kwenye kanuni. Kanuni zikatungwa bila kuianzisha *TOSCA*. Sheria ya Mbegu ya mwaka 1973 ilionyesha kwamba Taasisi hii ingeanzishwa na Waziri katika Kanuni na Kanuni za mbegu zilizotoka mwaka 1975 hazikuianzisha Taasisi hiyo.

Sehemu ya pili pia inampa Waziri uwezo wa kutangaza kwenye gazeti la Serikali aina za mbegu hatari. Kwa mfano, mbegu za magugu ambazo hazitaruhusiwa kuwa miongoni mwa mbegu zitakazouzwa ama kuingizwa humu nchini.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu, ambayo inajumuisha vifungu viwili cha 13 na cha 14 inaweka utaratibu wa kudhibiti uingizaji, uuzaji na usambazaji wa mbegu ndani ya nchi. Aidha, sehemu hii inaweka utaratibu wa kuuza mbegu nje ya nchi. Chini ya sehemu hii uagizaji wa mbegu kutoka nje ya nchi na wauzaji wa mbegu nje ya nchi, wazalishaji wa mbegu wa ndani na wauzaji na wasambazaji wa mbegu wanatakiwa kupata kibali au leseni kwa ajili hiyo.

Kwa mfano, kifungu kidogo cha pili cha kifungu cha 13 kinamtaka Mkurugenzi wa Maendeleo wa Mazao kabla hajatoa leseni, kuhakikisha kwamba viwango vya uingizaji nchini, uzalishaji, uandaaji, uuzaji na usambazaji kwa ajili ya kuuza mbegu vinakubaliana na viwango vilivyowekwa katika Sheria ya kudhibiti viumbe waharibifu wa mimea na mazao yaani *The Plant Protection Act, 1997* na vile vile na Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kile kifungu cha 14 wauzaji wa mbegu nje na ndani ya nchi wanatakiwa kuuza mbegu zinazowiana na viwango vilivyotolewa katika sheria au katika Kanuni. Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha tatu cha kifungu cha 14 ni kosa la jinai kukiuka utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ya Muswada inajumuisha vifungu kuanzia cha 17 mpaka cha 25. Sehemu hii ina vipengele vinavyowataka wazalishaji, wauzaji na wasambazaji wa mbegu kujisajili na kupewa leseni. Aidha sehemu hii inatoa utaratibu wa kufuta leseni hizo. Haki na utaratibu wa kukata rufaa kwa wale ambao hawataridhika na uamuzi wa kukataliwa au kufutiwa leseni zao pia umetolewa katika kifungu cha 18 cha sehemu hii.

Sehemu hii pia inapiga marufuku biashara ya mbegu kufanyika bila kuanza kufanyiwa usajili. Chini ya kifungu kidogo cha pili cha kifungu cha 19 wakulima wanaozalisha mbegu za ubora uliohakikiwa kuwa *quality declared seeds* wanaruhusiwa kutumia kwenye mashamba yao au kuuza au kugawa mbegu zilizozalishwa kwa majirani zao. Mbegu za aina ya ubora uliohakikiwa huzalishwa na wakulima chini ya usimamizi wa wataalam na huruhusiwa kutumika kama mbegu baada ya kukaguliwa na *TOSCA.*

Sehemu ya nne, ina vipengele vinavyotoa mamlaka kwa wakaguzi na wahakiki wa mbegu ya kutekeleza Sheria hii. Chini ya kifungu cha 23 ni kosa la jinai kumkatalia mkaguzi kufanya kazi yake au kutoa taarifa za uwongo kwa mkaguzi. Sehemu ya tano na ya mwisho ina vifungu kuanzia kifungu cha 26 mpaka 35. Sehemu hii inaainisha makosa na adhabu kwa makosa mbalimbali yatakayotokana na ukiukaji wa sheria hii.

Chini ya kifungu kidogo cha 4 cha kifungu cha 29, Mahakama inaweza kuamuru mtu aliyetiwa hatiani kulipa fidia kwa watu walioathirika kutokana na ukiukwaji wa Sheria hii. Hiki kifungu kina lengo la kumlinda mkulima kwamba mtu anayesema kwa mfano ameingiza mbegu ya aina fulani akagawa mbegu ambao haikufikia kiwango kile na akapatikana na hatia Mahakamani, Mahakama inaweza kumtaka mtu huyo awalipe wakulima fidia.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 5 pia inampa Waziri uwezo wa kisheria wa kutunga Kanuni mbalimbali zitakazotumika katika utekelezaji wa sheria hii. Aina na viwango vya ubora wa mbegu vitawekwa kwenye kanuni zitakazotungwa chini ya sheria hii. Aidha, chini ya kifungu cha 32 cha Sheria ya Mbegu ya mwaka 1973, *The Seeds (Regulation of Standards) Act,* inafutwa.

Hata hivyo, kwa mujibu wa kifungu kidogo cha 2 cha kifungu hicho Kanuni, amri na matangazo yaliyotolewa kwenye Gazeti la Serikali chini ya Sheria ya Mbegu Na. 29 ya mwaka 1973 yaani ile *The Seeds (Regulations of Standards) Act, 1973* iliyofutwa yataendelea kufanyika mpaka hapo yatakapotungwa chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamliwe)*

**SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua Muswada huu, namwomba Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, aje anipokee kiti ili nikafanye kazi nyingine.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**MHE. MUSA A. LUPATU (k.n.y. MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Mbegu *(The Seeds Bill 2003)* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kifungu cha 70(ii) Toleo la 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa maoni ya Kamati, ningependa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam kwa jinsi walivyowasilisha kwa ufasaha mkubwa Muswada huu wa mbegu. Maelezo yao yaliwapa uwelewa mkubwa Wajumbe wa Kamati na hivyo kuwarahisishia kazi yao katika kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi, ilichambua Muswada wa Mbegu *(The Seeds Bill, 2003)* tarehe 29 Oktoba, 2003 na kabla ya kuchambua Muswada huu Kamati ilikutana kwa siku nzima na wadau mbalimbali kwa lengo la kupokea maoni yao juu ya Muswada huu wa mbegu. Kamati ilinufaika sana na uhodari na utaalam wa wadau pamoja na wataalam kutoka Wizara ya Kilimo na Chakula kwa maelezo ya kitaalam waliyoyapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kutoa maoni naomba kutumia nafasi hii kuwataja na kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii ambao walihusika katika kuchambua na kuboresha Muswada huu kama ifuatavyo:-

Wa kwanza ni Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mwenyekiti, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Makamu Mwenyekiti na wafuatao walikuwa ni Wajumbe:-

Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Robert Mashala, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Masoud Abdulla Salum, Mheshimiwa Ali Said Salum, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Salama Khamis Islam, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha na Mheshimiwa Philip Magani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Kamati ilikubaliana na Serikali juu ya kuleta Muswada wa Mbegu *(The Seeds Bill, 2003)* ikiwa ni juhudi za Serikali za kuinua na kuendeleza sekta ya mbegu hapa nchini kwa kuzingatia mabadiliko ya sera hasa sera ya uzalishaji, utafiti na usambazaji wa pembejeo za kilimo kufanywa na sekta binafsi.

Muswada ambao sasa unazingatia mabadiliko ya kiuchumi ambapo huduma za pembejeo za kilimo kwa sasa zinatolewa na Sekta binafsi.

Muswada huu ndio msingi wa kilimo hapa nchini na hasa tukiweka mikakati mizuri ya uzalishaji, tafiti, usimamizi na usambazaji wa mbegu. Kamati imefarijika kuona kuwa kutakuwa na chombo ambacho kitasimamia ubora wa mbegu zinazozalishwa hapa nchini na zinazoagizwa toka nje ya nchi yaani *TOSCA.* Chombo hiki ni cha muhimu sana kwa ajili ya kukidhi ubora, kudhibiti ubora wa mbegu, pamoja na kulinda mbegu ambazo zimeonyesha ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama chombo hiki hakitafanya kazi zake vizuri basi mbegu bora zilizopo na zitakazofanyiwa utafiti zitapotea kwa hivyo ni vyema chombo hiki kikaimarishwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijadili Muswada wa Mbegu kwa kina nataarifu mapendekezo yote yalikubaliwa na Mheshimiwa Waziri. Kamati imependekeza kuwa Wizara iandae utaratibu wa kuweka msukumo kwa wananchi wetu kuhamasika kupanda mbegu bora zilizoandaliwa na wataalam badala ya utaratibu waliouzoea wa kupanda mbegu zilizozalishwa nao wenyewe kutoka kwenye mavuno yao. Juhudi zifanywe na Serikali ili hamasa hiyo ya kutumia mbegu bora iweze kuwafikia wakulima walio wengi huko vijijini. Hamasa hiyo hiyo iende sambamba na Serikali kutoa ruzuku ya bei ya mbegu ili wananchi wengi zaidi waweze kununua mbegu hizo badala ya mbegu za kienyeji au mbegu za kuokoteza tu. Kilimo ndiyo msingi wa maendeleo ya nchi yetu na wananchi kwa jumla, hivyo basi msingi wa kilimo bora lazima ianze na upandaji wa mbegu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikubaliana na Muswada katika kuanzisha Kamati ya Kitaifa ya Mbegu yaani *The National Seeds Committee,* kwa lengo la kusimamia masuala ya kitaifa ya mbegu. Muswada pia umeweka utaratibu wa Kamati ya Kitaifa kuwafutia leseni ama usajili wafanyabiashara au makampuni ambayo watakiuka taratibu za uagizaji, uzalishaji na usambazaji wa mbegu.

Muswada pia umeweka utaratibu wa kukata rufaa kwa Waziri kama mtu yeyote ataona uamuzi wa Kamati ya Kitaifa ya Mbegu haujamtendea haki. Katika Muswada huu pia umeweka kipengele kwamba Waziri atatoa uamuzi baada ya kushauriwa na Kamati ya Kitaifa ya Mbegu.

Wajumbe walionyesha wasiwasi kwamba Kamati ambayo tayari imemfutia leseni, ikiwa ndiyo itamshauri Mheshimiwa Waziri kutoa uamuzi kwenye rufaa ya mlalamikaji hapo Kamati iliona kuwa ni vema kuwe na chombo kingine cha kumshauri Mheshimiwa Waziri juu ya maamuzi ya rufani, vinginevyo mlalamikaji atakosa imani juu ya uamzi wowote hususan ule utakaokwenda kinyume na mategemeo ama matarajio yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliona kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuweka utaratibu wa kutunza mbegu na mimea yetu ya asili ili isitoweke. Sasa kuna haja

ya kuanzisha makumbusho yaani *Museum* ya kilimo kwa lengo la kuonyesha mbegu, kuonyesha na kuhifadhi mbegu, mimea na vifaa vya zamani ili watoto wetu wakajifunze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 26, kifungu cha nne, kunaelezwa utaratibu wa kulipa fidia kwa hasara ya kutumia mbegu isiyofaa. Kamati ilikubaliana kuwa lazima kipengele hiki kifafanuliwe kwa uwazi zaidi ili kujua fidia itakayotolewa kufidia hasara inayosababishwa kwa mkulima kununua mbegu zisizofaa itakuwa ni ya namna gani? Je, fidia hiyo itakuwa ni gharama ya mbegu au gharama ya mbegu pamoja na mazao ambayo yangepatikana kutokana na mbegu hizo? Kwa sababu mbegu ndiyo msingi wa kwanza wa mavuno endapo msingi huo utakosewa mkulima atapata hasara. Kwa hiyo, lazima sasa fidia ilenge kumpatia mkulima huyo wa mbegu pamoja na mavuno ambayo yangepatikana kutokana na mbegu hizo.

Aidha, Muswada pia uweke wazi ni nani atalipa fidia hiyo, je, ni mfanyabiashara aliyemwuzia mkulima mbegu, mtafiti aliyeshughulikia mbegu hizo au chombo kinachothibitisha ubora wa mbegu yaani *TOSCA* au ni Serikali? Jambo la msingi zaidi kwa maoni ya Kamati ni kwamba sheria inayokusudiwa kutungwa kwa Muswada huu itakuwa na manufaa kama itasimamiwa na kutekelezwa kwa makini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati walielezwa kwamba Serikali imeanza kuwaelimisha wataalam Wilayani namna ya kukagua mbegu bora zilizozalishwa. Lakini Kamati ilionyesha wasiwasi kuwa wataalam hao hawataweza kufanya kazi hiyo kikamilifu kwa sababu hata sasa Mabwana

Shamba waliopo kwenye Kata zilizopo wanashindwa kutembelea Vijiji vilivyopo kikamilifu katika Kata zao, je, huyo mtaalam kutoka Wilayani atawezaje kuhudumia Vijiji vyote katika Wilaya yake?

Aidha, baadhi ya Wilaya karibu 68 hapa nchini hazina Mabwana Shamba wa Wilaya, je, hawa Maafisa wa kukagua mbegu watatendaje kazi yao katika Wilaya ambazo hazina Mabwana Shamba? Kamati kwa kuzingatia umuhimu wa jambo hili inaishauri Serikali iharakishe na ihakikishe ya kwamba kila Wilaya inampata Bwana Shamba aliyesomea na kuhitimu utaalam huo kabla ya kuanza shughuli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la muundo wa Serikali katika uwajibikaji wa Mabwana Shamba bado hauna nguvu za Kisheria kwa Wizara ya Kilimo na Chakula kwani kwa utaratibu wa sasa Mabwana Shamba wanawajibika kwa Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya. Huu ni utaratibu unaoleta kasoro kubwa sana katika ufanisi wa Sekta ya Kilimo hapa nchini kuna umuhimu mkubwa sana, Mabwana Shamba na Maafisa wa Mifugo waliopo katika Wilaya zetu wawe wanawajibika moja kwa moja Wizarani kwa majukumu yao ya kitaalam ili pawepo na mtiririko mzuri wa utoaji wa taarifa, ufuatiliaji na utekelezaji muafaka wa maamuzi ya Wizara Kitaifa kuhusu sekta hizi nyeti za kilimo na mifugo. Mfumo uangaliwe upya ili kuona nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya na wajibu wake katika usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati walikubaliana kimsingi kuwa, kuna umuhimu mkubwa kwa wakulima wetu kuelimishwa kuhusu utaratibu mzima katika kununua mbegu zilizo bora. Kwa kawaida mbegu bora ni ghali kidogo ukilinganisha na mbegu zinazouzwa bila ubora. Hivyo wakiona mbegu zinauzwa kwa bei ya chini wachukue tahadhari juu ya ubora wake, pia wakulima washauriwe kutunza mifuko waliyonunulia mbegu hizo ili matatizo yakitokea mifuko hiyo iwe kumbukumbu muhimu katika kufuatilia uhalali wa mbegu hizo. Inaaminika ya kwamba mifuko inayowekewa mbegu bora haiharibiki kwa muda mrefu.

Aidha, Waheshimiwa Wabunge wawahamasishe wananchi katika suala zima la kutumia mbegu bora zilizozalishwa kwani suala la mbegu bora ni muhimu kama suala la mbolea. Mbolea bila mbegu bora ni kazi bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilibaini kimsingi kuwa Muswada huu haukuweka kipengele kinachoshughulikia *genetically modified organisms* ambapo baadhi ya wafanyabiashara wa mahindi, ngano, mchele na kadhalika wanaweza kuingiza nafaka hizo kwa ajili ya chakula lakini nafaka hizo zikiachwa zipandwe zitaathiri sana mazao yetu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu kutoka nchi za India na Amerika unaonyesha ya kuwa *GMOs* zinaathiri sana mazao asilia. Kamati inaishauri Serikali kuwa iweke umuhimu mkubwa wa kuwaelimisha wananchi wetu juu ya matumizi ya nafaka za *GMOs* kuwa ni kwa ajili ya chakula tu na siyo kwa ajili ya kupanda. Inashauriwa pia kwamba uanzishwe utaratibu wa kuleta nafaka hizo katika hali ya unga na siyo mbegu. Kipengele kiongezwe kwenye Muswada huu cha namna ya kudhibiti *GMOs* na matumizi yake kwa msisitizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Kamati ilishauri Wizara itayarishe mapema kanuni zitakazosaidia kutekeleza Sheria hii badala ya kuendelea kutumia kanuni zinazotawala Sheria inayofutwa ya mwaka 1973. Kanuni hizo zieleze kwa uwazi kabisa utaratibu wa Mabwana Shamba kuwajibika Kisheria kwa kupeleka taarifa Wizarani ili tuwe na takwimu kamili katika Wizara ya Kilimo na Chakula. Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya awajibike kuratibu shughuli za kiutendaji za Mabwana Shamba pamoja na kuhakikisha wanapeleka taarifa zao Wizarani kama inavyopendekezwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ingependa kuunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri na kuliomba Bunge lako Tukufu pia liunge mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Uanzishwaji wa Sheria ya Mbegu ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda niseme ya kwamba mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati hii ya Kilimo na Chakula, nilikuwa kwenye Kamati kwa hiyo, nitakayokuwa nayasema hapa ni kukazia tu ushauri na siyo kupinga hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inatambua umuhimu wa Sheria hii ya Mbegu kwani ni moja ya mihimili mikuu ya Sekta ya Kilimo. Tunaamini Sheria hii ikiangaliwa kwa makini na kuwapa uwezo wadau wote wanaoendesha sekta nzima ya kilimo pato la wananchi na Taifa kwa jumla navyo vitaongezeka, Taifa litajitosheleza kwa chakula na kuuza mazao mengi nje ya nchi na hatimaye kujinasua katika lindi la umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kilimo nchini ni duni lakini haina maana kuwa wakulima hawalimi ila moja ya matatizo makubwa ni kuwa hawapati mbegu zenye ubora unaoendana na hali ya hewa kwenye maeneo husika. Pia haina maana kuwa mbegu hizo hazipo bali Sheria zinazotawala biashara nzima ya mbegu hazitoi nafasi kwa wadau kwani kuandaa mbegu siyo mchezo na Serikali ijue hilo kwamba hawa wanatakiwa wapewe maandalizi mazuri kimazingira na kihuduma *(environmental and good infrastructures)* kama vile upatikanaji wa maji na mashamba mazuri kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Taifa ya Mbegu ukizingatia muundo wake katika Sheria hii mpya, muundo uliopendekezwa ni wa Kiserikali mno, kati ya Wajumbe kumi, watano ni watumishi wakuu wa Wizara ya Kilimo na Chakula wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ambao kwa Sheria ya 1973 ni hao hao walikuwa Wasimamizi wa Sheria ya Mbegu ambayo imeshindikana kutekelezeka na hivyo kusababisha kutungwa kwa Sheria hii leo, kwa mtazamo wetu ni sawa na mvinyo wa zamani katika chupa mpya.

Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa, Kamati hii iwe na mtu mmoja tu kutoka Wizarani na wengine wote wawe ni watu wa nje ya Wizara ya Kilimo na Chakula ambao ni wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapendekeza kuwa mwakilishi wa *Seed Trades Association* awe mmojawapo, pili, *either* Mwakilishi kutoka *Tanzania Plant Association,* tatu, mwakilishi kutoka Vyuo Vikuu viwe vyenye kuhusika na kilimo na nne, mwakilishi kutoka Umoja wa Wakulima. Ukifanya hivyo, kwanza utapunguza ukubwa wa Kamati na pili utaondoa urasimu, *bureaucracy* ya Kiserikali na Kamati hiyo ichague Mwenyekiti wake na siyo Katibu Mkuu wa Wizara.

Tunapendekeza Katibu Mkuu wa Wizara awe ndiye Katibu wa Kamati hiyo. Katika muundo uliopendekezwa Katibu Mkuu ni Mwenyekiti wa Kamati na wafanyakazi wa chini yake yaani *subordinates* ni Wajumbe wa Kamati hiyo, kiutendaji hawatakuwa na sauti mbele ya bosi wao. Kama Serikali inaona pendekezo la kubadili muundo wa

Kamati hauwezekani, basi Serikali iunde Mamlaka ya Mbegu *(Seed Authority)* ambayo itakuwa na bodi yake na mamlaka zaidi ya kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa kazi ya Kamati tunapendekeza kwamba muundo huo uendane na kazi zitakazofanywa na Kamati. Kambi ya Upinzani inaona Kamati itakuwa na nafasi nzuri ya kuishauri Wizara kama Wajumbe wake hawatakuwa watumishi wa Wizara hiyo hiyo.

Kwa mfano, moja ya kazi za Kamati na napenda ninanukuu: *"The functions of the National Seed Committee shall include:- (a) To advise the Ministry on formulation and implementation of the seed industry policy and implementation of guidelines;"* kifungu kidogo cha *"(d) To give general advice in the co-ordination and supervision of the seed industry."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ni kwamba Kamati itaishauri Wizara na Wizara ni Katibu Mkuu na wale waliotajwa katika Muswada. Haiingii akilini wewe uwe ndiyo Msimamizi Mkuu na ndiyo mpokea ushauri na vile vile uwe ni mshauri, mtu huyo huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi zilizotajwa, bado ushauri wa Kamati hautakuwa na maana kama Wajumbe wake wako chini ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo. Ningependa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wasome sehemu ya pili ya Muswada, *The functions of the Committee,* kifungu cha tano (a) mpaka (e) wanaweza wakaona haya ninayojaribu kuyafanunua hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utafiti uliofanywa na Profesa Kalunde P. Sibuga wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, *on harmonization of Seed Policies and Regulations in East Africa* kuhusu matumizi ya mbegu bora, ni kwamba umeshuka sana hapa Tanzania na kwamba kutoka asilimia 15 ya miaka ya nyuma hadi asilimia 4 tu kwa sasa. Kama takwimu zinavyoonyesha hapa chini ukilinganisha na matumizi ya mbegu bora katika nchi nyingine za Afrika utafiti wake unaonyesha kama ifuatavyo:-

Tanzania kwa sasa inatumia tani 5,000 tu, Kenya wanatumia tani 25,000, Zambia wanatumia tani 30,000, Zimbabwe wanatumia tani 50,000 na *South Africa* wanatumia tani 100,000, sasa ukiangalia matumizi ya mbegu bora Tanzania ni 5,000 tu, ni asilimia kidogo sana. Kwa hiyo, tunahitaji kuhamasisha zaidi na kutumia mawazo tunayoyatoa hapa sisi Waheshimiwa Wabunge ili yaweze kwenda sambamba kwa kufanikisha katika utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwelekeo huo hatuendi, hivyo Tanzania itakuwa inatakiwa itumie ushauri nasaha wa Kamati madhubuti ili kuongeza matumizi ya mbegu zenye ubora. Ikumbukwe kuwa tulikuwa na *TANSEED Company* ambayo ilifanya kazi yake vizuri hasa kwa sababu ilikuwa ikipewa ruzuku, *subsidy* kwa mbegu zilizozalishwa, kampuni hiyo ilifilisika kwa sababu ya kukosa ruzuku.

Tunaishauri Serikali itoe ruzuku kwa wazalishaji wa mbegu bora ili wazalishe zaidi. Nataka ieleweke kuwa ruzuku siyo ili mradi ruzuku, tuangalie mfano ambao

nitausema hapa chini, kwamba ongezeko la tija siyo tu kupunguza bei, bali wakulima wetu ambao uwezo wao ni mdogo wapate kuzinunua kwa wingi na siyo hiyo tu na hata wale wababaishaji wanaotumia mbegu za mahindi au nafaka za kawaida, kuweka rangi na kuuza kwa bei kubwa kama mbegu bora kwa ulaghai, hawataweza kufanya hivyo ikiwa kwa mfano gunia moja la mahindi ni shilingi 10,000/= na gunia la mahindi ya mbegu bora yaliyotiwa dawa ni shilingi 8,000/=, hakuna mtu atakayeshawishika au kuhangaika na ulaghai ambao yeye atapata hasara. Hivyo kukomesha uhalifu wowote ni kuweka ruzuku ya kutosha, siyo kwamba ruzuku mradi ruzuku maana labda gunia la mbegu linaweza kuwa shilingi 25,000/= na gunia la mahindi ya kawaida likawa shilingi 10,000/=, na Serikali ikatoa shilingi 5,000/= kama ruzuku sisi tunaona si jawabu, jawabu ni kwamba zile mbegu bora tuhakikishe kwamba bei inakuwa chini ya bei ya soko ya nafaka za kawaida, ili kukomesha mambo mengi sana ambayo labda tungehangaika Mahakamani, kuwashtaki watu na ma-*inspectors,* sasa hayo yatajikomesha yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia nzima na hasa nchi zilizoendelea hutoa ruzuku kwa wakulima wake na hata nchi maskini kama Bangladesh hutoa ruzuku kwa wakulima wake na sisi Tanzania tunafahamu hilo, ni vipi tunakuwa na kigugumizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu aya iliyoandikwa kwa lugha ya kiingereza kama walivyoshauri wataalam tangu mwaka 1980: *"Registration should be the last step in the development, in the greatest seed programs rather than control and should all be affected when the seed industry in operation."*

Kuna mazao ambayo huwa hayaoteshwi kama nafaka, mkulima anaweza kukaa na mbegu zake kwa miaka mingi kwa mfano mazao kama mihogo, viazi vitamu, viazi vikuu, migomba, miwa na kadhalika. Mazao kama haya kila mkulima vijijini ni mzalishaji wa mbegu hiyo hivyo Sheria ya Mbegu inasema nini kwa hawa wananchi pindi akiamua kufanya biashara itakuwaje? Nadhani Mheshimiwa Waziri katika Muswada huu amesahau umuhimu wa Sekta hii ya Mbegu isiyo rasmi *(Informal Seed Sector).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na marekebisho *schedule of amendments* bado haijasema kuhusu hawa wenye mbegu hizi za asili na wenyewe wanaziamini, je, watalindwaje na Sheria hii kibiashara? Aidha, katika mapendekezo ya watafiti wa mbegu ni kuwa na Sheria ya Uanzishaji wa Mfuko wa Mbegu *(Seed Revolving Fund).* Mfuko huu utasaidia hasa *contract pharmacy* ili waweze kuzalisha mbegu na wasishawishike kuharibu mbegu kwa ajili ya soko nzuri la biashara ya chakula. Vile vile, mfuko utasaidia usambazaji na kuongeza upatikanaji wa pembejeo kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tunashauri kuhusu Mabwana Shamba kuwa chini ya Halmashauri au Mkurugenzi wa Wilayani kwani wanatumika vibaya huko waliko, utakuta Bwana Shamba anatumwa na Mkurugenzi kwenda kukusanya kodi za maendeleo, sasa hivi haipo lakini walifanya hivyo, sasa sijui watapewa kazi gani. Hili limeturudisha nyuma sana kwani sisi tunatunga Sheria hapa, Sheria zinatumika lakini wale watekelezaji wa Sheria ni Mabwana Shamba ambao ndiyo wako karibu na wananchi hawapati taarifa moja kwa moja kutoka Wizarani na hawarudishi majibu, aidha, matokeo

ya kule chini moja kwa moja mpaka Wizarani wanakwenda kwa Mkurugenzi ambaye labda hajui chochote kuhusu kilimo wala labda hana hata *interest* kwa hiyo hawezi akaisaidia sana Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunashauri kama yalivyo mashirika mengine kama ardhi na kadhalika, yapo mashirika ya namna nyingi ambayo yameishia pale, tunapenda kuiomba Serikali iliwekee umuhimu hilo kwamba kwa kweli tunahitaji ile channel kuanzia juu kwenye Wizara mpaka kwa *Extensional Officers* ambao ndiyo Mabwana Shamba ndiyo wanaoweza kuwafikia wakulima vizuri ili shughuli hii iweze kwenda sambamba kwa manufaa ya Taifa la Tanzania. Tanzania itaneemeka kwa Muswada huu kama ushauri huu utazingatiwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Muswada huu muhimu wa Mbegu wa mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea ningependa niseme ya kwamba, nauunga mkono Muswada huu moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nianze kwa kweli na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wao wote. Kwanza, kwa kazi nzuri ambayo Wizara inafanya na pili kwa kuuleta Muswada huu kwa wakati muafaka. Ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba pamekuwa na mabadiliko mengi, *Tan Seed* ilipoelemewa na kushindwa kukidhi haja ikafa na Serikali mwaka 1995 ikaruhusu wauzaji wa mbegu binafsi.

Kwa hiyo, matokeo yake wakulima wetu wamekuwa wakipata mbegu ambazo nyingine kwa kweli si nzuri, mbovu na matokeo yake mavuno yanakuwa hafifu na mbegu nyingine zimekuwa mara kwa mara zina magonjwa, wadudu wengi, nikichukulia mfano, wakulima wangu kule Kisarawe wanaponunua mbegu za mahindi wakienda kupanda utakuta pengine asilimia 10 tu ya mbegu waliyopanda ndiyo inaweza kuzalisha. Kwa hiyo, hali hii imefanya Wizara kuleta Muswada huu, tuipongeze ili kuweza kuwanusuru wakulima na mbegu mbovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nina maoni machache tu juu ya Muswada huu. Ningeomba nikiri kwamba nilikuwa na maoni mengine ambayo baada ya kuona marekebisho yaliyotolewa hivi sasa imebidi sehemu nyingine nibadilishe maoni yangu. Sasa nakiri muda haukutosha, inawezekana pengine nikarudia mambo ambayo tayari yamekwisha rekebishwa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri anisamehe kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nianze na kifungu cha 11, kifungu kidogo cha kwanza ambacho kinasema, Mheshimiwa Waziri anaweza kukasimu baadhi ya madaraka yake lakini vile vile kinasema au madaraka yake yote.

Mimi nadhani pengine Mheshimiwa Waziri hangependa kukasimu madaraka yake yote, kwa hiyo lile neno *or all* pengine angependa kuliondoa kwa sababu yapo madaraka ambayo mimi nadhani si rahisi kuyakasimu. Kwa mfano, pale anapopewa madaraka na Sheria hii kuteua *National Committee,* sidhani kama angependa ku-*delegate,* kutunga *regulations* au ukitazama katika sehemu ya kwanza, Ibara ya kwanza inayosema, lini Muswada huu utaanza, ni kwamba amepewa madaraka kuutangaza yeye. Sasa nisingependa kuona Mheshimiwa Waziri anakasimu madaraka hayo kwa mtu mwingine autangaze. Hilo ni rekebisho ambalo pengine akilizingatia linaweza likasaidia huu Muswada kumpa madaraka yake kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, maoni yangu yanahusu sehemu ya tatu, kifungu cha 13, Ibara ndogo ya kwanza. Pale wameonyeshwa watu ambao watakuwa wanashughulika na kuingiza mbegu nchini, kupeleka nje, usambazaji na kadhalika lakini pale mwisho kuna maneno yanasema, *sale or advertisement for sale of seeds.*

Mimi nafikiri kwa wale wanaotangaza, kama mtu aliyezalisha mbegu, amesambaza, ameingiza nchini au amepeleka nje amekwishapata *Certificate,* sioni kwa nini anayetangaza lazima atakiwe ku-*register* kwa sababu tayari anatangaza kitu ambacho mbegu hiyo ama ni yeye mwenyewe tayari amekwishapata *certificate* au anamtangazia mtu ambaye amekwishapata *certificate.* Hili siyo jambo nzito lakini nafikiri ingebidi liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu ya nne, *registration of seed dealers* kwenye ile Ibara ya 15, Ibara ndogo ya tatu, kumeelezwa pale kwamba kutakuwa na *registration fee.* Lakini nilipoangalia katika Muswada huu sikuona mahala gani pametamkwa hiyo ada ya usajili itakuwa ni kiasi gani. Sijui kama inaachiwa mpaka iwe chini ya kanuni ambazo Mheshimiwa Waziri atafanya au ingekuwa vizuri ingetajwa ndani ya Sheria hii ili kusudi kila anayeshughulika na uuzaji, ununuzi na kadhalika ajue kwamba *registration fee* ni kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 18, Ibara ndogo ya pili, Sheria inasema ya kwamba Mheshimiwa Waziri kabla hajaamua kushughulika na *appeal* angependa kupata ushauri kutoka kwa Kamati ya Taifa ya Mbegu. Wasiwasi wangu ni kwamba pakitokea *appeals* nyingi, hivi Kamati hiyo itakuwa inaitwa kila mara inakutana ili kumshauri Mheshimiwa Waziri?

Mimi nafikiri kungekuwa na utaratibu ambao utamfanya Mheshimiwa Waziri apate ushauri moja kwa moja bila ya kuitisha Kamati ile ili kusudi maamuzi yake yasije yakachelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *section* hiyo hiyo, Ibara ya 22, Ibara ndogo ya nne inasema kwamba, *"provided that any seed or package seized or placed under stop*

*sale pursuant to this subsection shall not be detained after."* Sasa ameendelea kuweka (a) na (b), sasa pale (b) kumewekwa kipindi cha miezi sita. Nahofia ya kwamba kwa mtu ambaye mbegu zake zimezuiliwa na kama mbegu zenyewe haziwezi kudumu kwa muda mrefu, baada ya miezi sita mbegu hizi akiachiwa yule mtu zitakuwa si mbegu tena, je, nani atafidia hasara ambayo ataipata? Nafikiri kingewekwa kipindi kifupi ili kusudi maamuzi yatoke upesi na kama mbegu zile zikitolewa bado ziwe zinaweza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sehemu ya Tano, Kifungu cha 26(1) kinatoa adhabu ambayo inasema: *"Conviction to a fine of not less than one million shillings."* Ni sawa kwa wale wanaoshughulika na uuzaji wa mbegu kwa wingi, lakini namfikiria yule mtu aliyechukua kijisehemu pale Kariakoo anauza mbegu zake kidogo sana, mapato yake yeye mwenyewe hayafiki hata laki mbili. Unapompiga faini ya shilingi milioni moja, akishindwa kulipa maana yake ni kwamba hayupo katika biashara na kama hayupo katika biashara maana yake ni kwamba wale wakulima wetu wadogo wadogo wanaotoka kule Kisarawe ambao mahali wanapopata mbegu ni pale Kariakoo watakuwa hawana mahali pa kupata mbegu kwa sababu hawana *access* kwa wauzaji wakubwa. Kwa hiyo, nafikiri ingekuwa bora hiki kiwango cha chini kikashushwa chini ya milioni moja ili wale wakubwa basi wanaweza wakatozwa hata hizo milioni zinazosemwa milioni 5 kwa sababu wana-*deal* na *volumes* kubwa. Hii itatuwezesha kuwa na wafanyabiashara wa mbegu wadogo wadogo wengi ambao ndio wanaowafikia wakulima wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 26(4), naipongeza Serikali imeamua kwamba yule ambaye amepatishwa hasara na mfanyabiashara ambaye amemuuzia mbegu mbovu, apate kufidiwa. Lakini sheria haionyeshi wakulima wadogo wana fursa gani ya kufidiwa pale ambapo wanapouziwa kwa mfano na huyu mfanyabiashara mdogo.

Sasa sheria hii jinsi ilivyo inaonyesha kana kwamba wale wakaguzi watakuwa wanakwenda kwenye mabohari ya watu wakubwa lakini mimi nimenunua kwa mtu mdogo ambapo nimekwenda kule shamba nikaharibikiwa, je, kuna fursa gani ya mkulima wa kawaida kuweza kupata fidia kwa hasara ambayo ameipata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri basi Mheshimiwa Waziri labda ile idadi ya wakaguzi iende mpaka kule vijijini hata kwa kuwafanya Maafisa Kilimo kuwa ndio wakaguzi pale ambapo mkulima mdogo ameuziwa mbegu ambazo ni mbovu aweze kutaarifu na wao wachukue hatua ili wauzaji hawa na wao waweze kutoa fidia kwa wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabla ya kengele ya mwisho haijagonga, nina jambo dogo tu ambalo liko katika kifungu cha 33 ni mpangilio tu. Katika kifungu cha 33 kuna kifungu kidogo cha kwanza na cha pili katika ukurasa wa 34, ukienda ukurasa wa 35 kifungu cha pili kimerudiwa tena kwa maneno yanayosema: *"The Minister may restrict the application of any of the regulations..."* nafikiri kuna haja ya kukifanya kiwe kifungu cha tatu na vilivyobaki vikasahihishwa katika mpangilio huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, narudia kusema tena naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nichangie katika Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Viwango vya Mbegu wa mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wizara nzima kwa kazi wanayoifanya na hasa kwa kuleta Muswada huu kwa wakati muafaka kuhusu masuala ya mbegu katika soko huria ambalo sasa hivi tunapambana nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya au bahati nzuri naweza kusema kwa upande mwingine upande mmoja bahati mbaya upande mwingine bahati nzuri masuala ya mbegu kwa Tanzania ni moja ya tatizo linalosababisha tuwe na mazao machache katika mashamba hasa hasa wakulima wadogo wadogo. Mbegu zinazotolewa ikiwa hazina ubora unaotakiwa basi ndio itakuwa balaa zaidi pengine matatizo yatakuwa makubwa kwa sababu moja hawa wakulima wadogo wadogo wanalima vijishamba vidogo vidogo na ikiwa mbegu zenyewe si bora maana yake hali ya mavuno itakuwa mbaya zaidi. Sasa naipongeza Wizara kwa kuliona hili suala ni muhimu sana wakati ambapo tumeingia katika soko huria ambapo kila mmoja alikuwa anaingiza mbegu anavyotaka, huyu anazalisha mbegu baada ya *Tan Seeds* kama ilivyosemeka mwaka 1995 kuwa hoi bin taaban basi akawa tena kila mmoja anaona amepata nafasi ya kufanya anavyotaka, hili moja Wizara imefanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande mwingine pengine nilikuwa nataka kuuliza masuala ya utafiti, matokeo ya utafiti, mbegu zile ambazo zimefanyiwa utafiti na hatimaye kupatikana matokeo ya utafiti huo je, ulikuwa umewafikia vipi wakulima hasa hasa wakulima wadogo wadogo?

Mara nyingi tafiti zinazofanywa kwa mbegu zinazozalishwa hapa hapa Tanzania matokeo ya tafiti hizi yanachelewa sana kuwafikia wakulima. Sasa sijui kwa sababu naona kazi hapa za Kamati ya Taifa ya Mbegu itakuwa ni kumshauri Waziri kuhusu mambo ya sera tu lakini kuhusu matatizo ya upatikanaji wa mbegu bora ili mkulima azipate na hatimaye aweze kupata mazao mengi au mazao bora, hilo naona halipo na tukizingatia mambo ya ugani katika sehemu mbalimbali ya nchi hii ni hafifu Mabwana Shamba kuwafikia wakulima wanawafikia wachache mno.

Sasa nilidhani tu pengine moja katika kazi ya Kamati ya Taifa ingawa ni *grade* ya Taifa pengine ishuke mpaka katika Wilaya ikiwa na Kamati ndogo ndogo huko kuona jinsi gani matokeo ya utafiti wa mbegu yanamfikia mkulima na mbegu bora hasa zinamfikia mkulima huyu mdogo ili aweze kuzalisha kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Pwani tumekuwa na utafiti wa zao la minazi, tafiti hizi zimefanywa kwa muda mrefu sana aina karibu 79 hasa katika Jimbo langu aina hizi 79 zimepandwa lakini hakuna hata mmoja uliokuwa umefaulu. Mbegu hizi ziliingizwa katika utaratibu mzuri tu na *TANSEED* ndiyo ambayo ilikuwa inashughulikia lakini ilikuwa chini ya msaada wa Ujerumani ndio walikuwa wanaendesha utafiti huo lakini

mpaka sasa hivi karibu mradi ule utamalizika muda wake nafikiri mwakani au mwaka unaofuata lakini mpaka sasa tunaona zao la minazi linaendelea kuathirika.

Sasa, je, kitu kama hicho ili kupata mbegu bora maana yake ni kwamba watu binafsi wataendelea au itakuwa ni masuala ya mtu binafsi atafute yeye mwenyewe au pengine kuwe na utaratibu maalum wa Kitaifa kama zao fulani linaathirika basi kuwe na mpango ambao utaweza ukasaidia kupata mbegu bora kwa ajili ya kuokoa zao ambalo linateketea. Kwa hiyo, nadhani katika moja ya *functions* za hii *National Seeds Committee* ingekuwa ni kuangalia lile zao ambalo limeathirika sana basi kuwe na utaratibu hata kuwekea sera ya kuona jinsi gani panaweza kupatikana mbegu ya kufaa ili zao lile liendelee au lifufuliwe kama limekufa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ninaloliona linahusu fidia ambalo Mheshimiwa Janguo, amelianza hapa hawa wauzaji wadogo wadogo. Je, mkulima ikiwa atapata hasara kwa mfano Mwanza kwa wajukuu zetu Wasukuma kule kumetokea mwaka 2002 mbegu za Pamba zilizotolewa kule zilikuwa mbaya au pengine mbovu au hazikufaa wakapata hasara wamepanda lakini hazikuota na nyingine zimeota hovyo hovyo tu na walipodaiwa fidia wakasema kwamba aah sisi hatujui habari hizo sasa nani anaweza kuwalipa fidia wakulima wale kwa hasara waliyoipata kutengeneza mashamba yao kisha baada ya hapo mbegu zisiote je, Wizara inasemaje kuhusu suala hili? Hapa nadhani jambo la kuangalia Kamati hiyo ikiundwa moja katika majukumu yake ni kuangalia haya masuala panapopatikana hasara kuhusu mbegu ambayo imeonekana kwamba mbegu hiyo ina kasoro nani anayehusika au atakayehusika kuwalipa wakulima fidia ya gharama ambayo wameitumia kwa ajili ya kutayarisha mashamba pamoja na mbegu ambayo haikuota na ununuzi walioufanya nani atawalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande wa marekebisho ya vifungu, nashukuru Mheshimiwa Waziri amerekebisha mengi ambayo nilikuwa nataka kuyatolea mfano na Mheshimiwa Janguo amezungumza kwa hiyo, sina haja ya kurudia kabisa katika masahihisho ya vifungu na natosheka kama alivyoyaleta Waziri katika *schedule of amendments* ambayo ametoa kule katika Kamati naridhika kabisa hakuna matatizo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hii *TOSCA* hivi ikiwa taasisi imeanzishwa kinyume cha utaratibu wa sheria na ambapo ilikuwa ianzishwe na Waziri haikuanzishwa na Waziri imeota kama uyoga tu na nini hiyo taasisi inaruhusiwa ku-*operate* vipi mpaka mwisho inaonekana kuna tatizo la kuweza kumudu kuendesha kazi zake na hatimaye inakuja kulalamikiwa baada ya kuonekana kwamba kazi zile zilizokuwa zifanywe na taasisi hiyo hazikufanywa, kwa nini kitu hicho kinatokea?

Mimi nimeshangaa kwamba inalalamikiwa taasisi wakati ambapo taasisi hiyo ingeweza kusimamishwa tu pale ilipoonekana kwamba haiendeshwi kisheria. Kwa hiyo, nadhani katika vitu kama hivi ambavyo vinaathiri uchumi wa nchi yetu kwa sababu mambo ya mbegu ndio yanaathiri kilimo chetu na yanaathiri hatimaye uchumi ambao unatokana na kilimo ambapo kilimo kinachochukua sehemu kubwa sana ya uchumi wetu.

Kwa hiyo, nadhani hili suala la kuanzishwa taasisi au kitu chochote kile kinachohusu uzalishaji na hatimaye kikaonekana kwamba hakikuanzishwa au kilikuwa kimeanzishwa bila utaratibu hicho kitu lazima kipigwe marufuku, kisimamishwe haraka iwezekanavyo kianzishwe kitu ambacho kinakwenda kwa utaratibu unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, namshukuru Waziri, Naibu Waziri wake na Wizara kwa kuleta Muswada huu na upande wa wenzetu wa Upinzani wameunga mkono na kwa maana hiyo upite ili mambo yaende kama kawaida na hatimaye tupate mbegu nzuri ziwafikie wakulima wetu wadogo wadogo na kazi iwe nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuongea katika Muswada huu wa *The Seeds Act, 2003.* Pia napenda niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja, Profesa Pius Mbawala na wataalam ndugu zangu katika Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kutuletea Muswada huu wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unataka kuwa na kilimo bora na kama unataka kilimo kiendelee basi sharti uwe na mbegu bora. Huna mbegu bora hakuna kilimo bora. Kwa hiyo, suala hili la udhibiti wa ubora wa mbegu ni suala muhimu sana. Nikitoa mfano katika zao tunalolima sana, zao la mahindi, kama una mbegu bora ya mahindi na ukafuata taratibu zote za kulima mahindi basi unaweza kuzalisha tani sita mpaka kumi kwenye hekta moja ya shamba. Lakini kama hukutumia mbegu bora hata ungeweka mbolea namna gani, uzalishaji wako utakuwa kuanzia nusu tani mpaka tani mbili. Kwa hiyo, umuhimu wa mbegu bora ni mkubwa sana katika kuleta maendeleo ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kwetu Tanzania ni muhimu zaidi kwa sababu *productivity* katika kilimo chetu kwa mazao mengi ni chini ya asilimia 15. Kwa mahindi kama nilivyotoa takwimu hizi ni chini ya asilimia 10, na ukienda kwa nafaka nyingine ni chini ya asilimia 15. Kwa hiyo, tunahitaji mbegu bora kwa kiwango kikubwa sana. Ukitaka kujua tatizo letu liko wapi, ujue tu kuwa mahitaji yetu ya mbegu bora kwa mwaka kama yalivyotolewa kwenye hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri ni kama tani 33,000 za mbegu bora, lakini sisi wenyewe tunazalisha tani 2,000. Kwa hiyo, unaona matatizo yetu ni makubwa kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetegemea Muswada huu ungejikita kwenye maeneo matatu muhimu. Eneo la kwanza ni hili hapa lililoelezwa kwa ufasaha kweli kweli namna ya kupata mbegu bora na kuhakikisha kwamba mbegu zinazouzwa na kulimwa na wananchi zinakuwa nzuri, hiyo ni sehemu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, katika mwaka wa 2003 pia Muswada huu ungetuletea ni jinsi gani tutaweza kuratibu *Vegitatively propagated materials* kama *tissue culture* na maeneo ya *genetically modified foods. Tissue culture* ya kawaida inatumiwa kuzalisha mazao mengi hata viazi hivi vya mviringo ni lazima yafuate utaratibu huo kwa wakati huu ya uzalishaji. Kwa hiyo, namna ya kudhibiti hivyo vimelea hivyo ni kitu

muhimu katika kuendeleza kilimo na katika kuratibu mbegu kwa maana ya chanzo cha mmea. Hiyo ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kutokana na uzalishaji mdogo wa mbegu hapa nchini na kutokana na kilimo kutokuwa bora kwa sababu hakuna mbegu bora basi Muswada huu ungelenga ni jinsi gani tutaweza kuzalisha mbegu ya kutosha ambayo ni mbegu ya hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi sehemu tatu ni muhimu sana na Muswada huu una sehemu moja tu kwa hiyo kwa mawazo yangu ningeshauri kabisa kwamba Muswada huu labda ungengoja kidogo hizo sehemu zote ziangaliwe kinaganaga ili tuweze kuwa na mpango kamili wa kudhibiti ubora wa mbegu, wa kudhibiti njia mpya za kuzalisha mbegu na wa kuhakikisha kwamba tunapata mbegu ya kutosha katika kuendeleza kilimo cha Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mawazo hayo, mwanzoni nilipokuwa nimesoma sheria hii nilisema ile *section ten,* ibadilishwe kabisa ili tuanzishe taasisi. Sasa katika marekebisho yaliyoletwa leo kumeanzishwa taasisi lakini kwa maoni yangu marekebisho haya hayaendi *deep enough* kuweza kukidhi matatizo ya upatikanaji, ubora na aina za mbegu ambazo zinafaa kwa wakati huu tulionao wa karne ya 21.

Kwa hiyo, nashauri kwamba taasisi hii ambayo tunaianzisha lazima iwe ni taasisi ambayo inaweza kusimamia sekta nzima ya mbegu ikiwa ni pamoja na kuhimiza uzalishaji wa mbegu bora, kusimamia na kutoa vibali vya uzalishaji wa mbegu kwa wakulima wakubwa, wakulima wadogo kwa maana ya *on farm seed production* na kwa makampuni ambayo yangezalisha mbegu.

Pia kukagua ubora wa mbegu kama ilivyoelezwa katika sheria ilivyo sasa na kufanya utafiti wa mbegu na kutoa maelekezo kwa maabara na mawakala wanaozalisha mbegu na kusimamia biashara ya mbegu ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja na kuratibu utafiti na uingizaji, majaribio, usambazaji na ufuatiliaji wa *genetically modified foods.* Hiki ni kitu muhimu sana katika kuendeleza kilimo. Mwisho, iweze kuratibu uzalishaji na usambazaji (sasa sijui unasemaje kwa Kiswahili) *vegetatively propagated materials* na *micro propagation* kwa maana ya *tissue culture* na *genetic engineering.* Bila kufika hapo tunafanya vitu nusu nusu tu. Kwa wakati huu na hali yetu ya kilimo ilivyo mbaya hatuwezi kungoja, hatuwezi kufanya vitu nusu nusu kwa sababu tunatakiwa tukimbie wakati wenzetu wanatembea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, taasisi hii ya uongozi wa mbegu ambayo imewekwa chini ya Ibara ya 10 na ambayo imeletwa kama marekebisho ya sheria hii inatakiwa irekebishwe zaidi, ili viongozi wake watendaji waelezwe vizuri kwamba hawa viongozi watendaji wa taasisi hii watakuwa akina nani, wateteuliwa namna gani na watafanya kazi yao namna gani. Kwa sasa kilichoelezwa hapa ni Kamati ndogo na Kamati kwa tatizo kubwa la nchi lilivyo sasa haiwezi kazi hii. Kazi hii lazima ifanywe na Bodi na sio Kamati na kwa umuhimu wa tatizo hili la mbegu ingetakiwa Bodi hii Mwenyekiti wake ateuliwe na Rais kwa sababu hiki ni kitu muhimu sana kinakwenda

kwenye *foundation* ya uchumi wa Tanzania. Hakiweza kuongozwa kakamati tu kanaundwaundwa huko ndani ya Wizara, haiwezekani. Ni lazima Bodi hii iteuliwe kama Bodi ambayo ni *serious* ambayo itafanya kazi kubwa ya kuratibu uzalishaji wa mbegu. Pia ni lazima sheria hii itueleze na Mwenyekiti wa Bodi hii atateuliwa namna gani, Makamu wake atateuliwa namna gani, wajumbe watakuwa akina nani na majukumu yake. Kama nilivyoeleza majukumu yake yaorodheshwe vizuri kabisa na jinsi gani yatatekelezwa.

Katika hali ambayo tunayo sasa hii ya soko huria na mbegu kwamba itaingia kwenye soko huria chombo hiki lazima kipewe nguvu nyingi zaidi ya hapa ili kiweze kusimamia msingi huu wa kilimo. Huu ndio msingi wenyewe, hakuna. Hivyo kilimo bila mbegu bora, hakuna, ni lazima chombo hiki kielezwe vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Bunge lako Tukufu linadhani kwamba kwa utaratibu wa marekebisho haya inatosha sina tatizo. Suala langu mimi ni kulieleza Bunge lako Tukufu, kitaalam ni kitu gani kinatakiwa kifanywe katika sheria hii.

Nadhani kwa jinsi ilivyo sasa sio kama napinga ni kitu kizuri sana kuwa na sheria hii lakini nadhani sheria hii haitoshi. Kwa hiyo, nadhani ingekwenda kurekebishwa halafu ikaletwa tena tarehe 10, 12 tukaipitisha ikiwa vitu hivi vya msingi vimewekwa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nimefurahishwa sana sheria hii kuja kwenye Bunge lakini nashauri Bunge kwamba lisiwe na haraka ya kuupitisha leo. Twendeni tubadilishe tena Muswada huu ili uweze kukidhi majukumu ambayo tunataka kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana mimi nataka Muswada huu ubadilishwe kwa kuuboresha kwa sababu nadhani msingi wake ni mzuri. Kwa hiyo, sina tatizo na Muswada wenyewe ile mantiki yake, lakini *content* yake ninayo matatizo nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Muswada uliopo mbele yetu.

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na wataalam kwa kutuletea Muswada huu mbele yetu ili na sisi tuweze kuchangia kidogo na kuboresha pale panapohitajika kutokana na maoni yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Tanzania toka Uhuru sijui tumefanikiwa kwa kiasi gani katika utafiti na udhibiti wa mbegu. Kwa sababu hatupewi maelezo ya takwimu na mafanikio katika upande huu. Hakuna maelezo ya kutosha kuturidhisha kwamba utafiti wa mbegu umeleta mafanikio fulani ndio maana mpaka hii leo inadhihirisha wazi kwamba utafiti au mafanikio ya utafiti hayakuleta tija kubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili ni jambo muhimu katika suala zima la utafiti wa mbegu tunapata matatizo mengi na hasa Serikali inakuwa na jukumu kubwa la kuongeza gharama panapotokea matatizo ndani ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunajadili Muswada huu hapa nashukuru na Waziri wa Fedha yupo ili aweze kuliona hili ni muhimu sana kwa sababu Wizara ya Kilimo na Chakula katika Bajeti yake na sisi tunapopiga kelele juu ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula ina matatizo, hii Wizara inahitaji ipate Bajeti ya kutosha ili kuweza kukidhi haja, mambo ya kilimo ni mengi na ni mapana kwa maana ya mahitaji ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazotolewa katika utafiti ni pesa ambazo huwezi ukazihesabu kwamba tunataka tulete mapinduzi ya kilimo katika nchi yetu ya Tanzania. Ni vema Serikali sasa ikasisitiza na kuona kwamba inatoa Bajeti ya kutosha kwa ajili ya utafiti wa mbegu kwa ajili ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi nina tahadhari na wasiwasi mkubwa katika suala zima la hii biashara huru au huria. Sasa hivi nchi kama Amerika, Canada na Uingereza wanatoa *pressure* kubwa kwa nchi nyingine ili wao nchi hizo waweze kusambaza mbegu duniani ili mbegu hizo zikizalisha mazao basi wawe wanadhibiti hali ya mbegu duniani.

Sasa natahadharisha Serikali kwamba kuna hatari ya sisi kuuawa kiuchumi na nchi hizi iwe wao ni kama silaha watakayoitumia kwa upande wetu na hasa nazungumzia *third world countries.* Tukikubaliana na jambo kama hilo basi Tanzania tumekwisha kwa sababu watakuwa na masharti yao na tukikubaliana na masharti hayo, tukikataa basi hatua ya kwanza ni kutunyima mbegu na hatimaye ni kuuwawa kisiasa na kichumi.

Sasa hilo vile vile napenda nitahadharishe kwa sababu Amerika sasa hivi wana utaratibu wa kuzalisha hizi mbegu ambazo zina majina mengi zinaitwa *Genetically Engineered Seeds* au wengine wanasema ni *GMO.*

Sasa vitu kama hivi vimethibitisha kwamba, hizi *genetically engineer seeds* zina madhara, kwanza, kwa binadamu na wao watakuwa na masharti kwamba, usiweke akiba ya mbegu ila wao ndiyo watakao-*supply.* Kuna nchi ambazo kuna makampuni yamefilisika kwa kukataa masharti ambayo tayari walishakubaliana nayo toka mwanzo. Kwa hiyo, naitahadharisha Serikali katika kuweka Mikataba au kuingia kuridhia mambo kama hayo bila kuwa na uangalifu. Wizara imeweka *organs* mbalimbali au *delegations* mbalimbali za kuweza kusimamia mambo kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna hili suala lingine linatia wasiwasi katika ibara ya 11 kwamba, zile *delegation of powers* alizopewa Waziri kwamba, anaweza akakasimu madaraka haya ama baadhi au yote, Mheshimiwa Mbunge mmoja, alizungumza hapa, mimi nikubaliane naye kwamba, Mheshimiwa Waziri hawezi kukasimu madaraka yote katika masuala kama haya kwa sababu kukasimu madaraka yote haya hakuna sababu kwa nini basi iingizwe katika Muswada. Iachwe wazi, sisi tunataka

Waziri mwenye dhamana, pakitokea jambo lolote basi awe ndiye anawajibika moja kwa moja na suala hili badala ya kutupiana mpira kwamba, ahaa siyo mimi ni fulani. Kwa hiyo, hili tuliepuke kwa sababu tunachotaka ni kuhakikisha kwamba, mwenye dhamana ya mambo kama haya ni Mheshimiwa Waziri basi tujue kwamba, ni yeye awe na uhakika kabisa kwamba, maamuzi yanayofanywa awajibike Waziri moja kwa moja badala ya kutupiana mpira kwa watu ambao pengine hawana madaraka ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui Serikali ina mpango gani wa kudhibiti uingizaji wa mbegu za nje ambazo zitaua au kuondoa zile mbegu za asili ambazo zinavumilia hali ya hewa na ardhi yetu na itazilinda vipi mbegu hizi za asili, kwa sababu haya makampuni ambayo yanauza mbegu hayapendi kuuza zile mbegu za jamii ya kunde kwa sababu uzalishaji wake siyo wa *volume* kubwa. Wao watauza mbegu ambazo zitakuwa na *volume* kubwa ya biashara, lakini mbegu hizi za jamii ya kunde ambazo wananchi wetu huwa wanaweka akiba na kuzalisha kila wakati na ni mbegu ambazo ni chakula ambacho kinapendwa na wananchi wetu kama vile kunde, maharage na mbaazi na vitu kama hivyo. Sasa utaona wazi kwamba, wao wame-*concentrate* na mbegu ambazo *volume* ya uzalishaji ni kubwa na hatimaye mkulima akipata faida anajua atakwenda tena kununua mbegu zile kwa sababu atapata faida. Hapendi mkulima apande mbegu hizi za jamii ya kunde kunde.

Sasa mimi naiomba Serikali ihakikishe kwamba, inawapa maelezo mazuri na kuwahamasisha wakulima wahakikishe kwamba, wanaweka mbegu za aina hii ili ziweze kuwasaidia panapokuwa na matatizo na tusikubali kupewa mbegu za aina hii zinazotoka nje kwa sababu hatimaye hazitakuwa na faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo mengi yamekwishaelezwa na Wabunge wenzangu, sina haja ya kuyarudia lakini nilikuwa na haya machache ya kutaka kuyasisitiza. La mwisho, nizungumzie suala la hii Kamati au Tume ambayo inasimamiwa na Katibu Mkuu wa Wizara. Mimi niko katika kukubaliana kwamba, Katibu Mkuu asiwe Mwenyekiti wa Chombo hiki na wale wanaofuata chini yake wote wapo katika Wizara hiyo hiyo, ni vema chombo hiki kikasimamiwa na Mwenyekiti ambaye hatokani na Wizara hiyo. Sina tatizo nani atamteua Mwenyekiti huyo aidha Rais au Waziri, mimi sina tatizo, lakini suala la Katibu Mkuu kuwa ndiyo Mwenyekiti na wale wote wanaofuata chini yake wanatokana na Wizara hiyo hiyo, mimi hiyo hainipi mantiki kama hicho chombo kitafanya kazi ipasavyo. Kwa hiyo, naomba mzingatie hilo ili tuweze kuboresha hali hii ya mbegu na kuleta manufaa na uchumi wa nchi yetu ili tuendelee vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru na ahsante sana.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia kidogo. Nichukue nafasi hii nimpongeze sana Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Keenja, Naibu Waziri, Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala, pamoja na wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu kwa kweli umekuja wakati muafaka, umekuja wakati ambapo Watanzania tunatakiwa tuufanyie kazi ili tusiendelee kulima kilimo duni, ambacho kinasababishwa na uduni wa mbegu. Hivi sasa tunakabiliwa na njaa katika sehemu nyingi, lakini katika nchi yetu tulikuwa hatuna sababu kabisa ya kukabiliana na njaa kwa sababu nchi yetu imekuwa na mvua ambazo ni nzuri, lakini tatizo lipo kwenye utafiti

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani kuna sehemu kama Ismani na nyingine kwa mfano, Mbeya na sehemu nyingine, tulikuwa tunatoa mahindi ya kutosha. Lakini tatizo watafiti hawakufanya utafiti mzuri hasa wa matumizi ya mbolea, unakuta mbolea ambayo inapelekwa Ismani haikupaswa mara nyingine kwenda Ismani kwa sababu tayari kuna chumvi, lakini unauziwa mbolea yenye chumvi sasa matokeo yake unaua ardhi, sasa unapoleta mbegu na mvua zikawa siyo za kutosha basi hupati kitu. Kwa hiyo, ningeomba utafiti wa kina ufanyike kwenye hili suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna udhibiti wa uingizaji wa mbegu, sasa hivi Serikali imeacha soko huria, tutadhibiti vipi au tumejipanga vipi. Mfano mwingine kwa sababu ya udhibiti mbovu wa mbegu zile ambazo zilikuwepo, sasa hivi kuna sehemu ya Kilolo wameingiza nzige. Nzige wale waliingia Kijiji kimoja tu cha Uluti, sasa hivi wameshaingia Kata nzima na wanatishia amani. Sasa ningeomba Mheshimiwa Waziri, hiyo ni moja ya kazi ambayo angeifanya, atume timu yake iende haraka sana kule Kilolo ikaangalie, *otherwise* nchi nzima wataenea wale nzige halafu litakuwa ni tatizo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia nizungumzie habari ya mbegu bora. Mbegu bora haiwezi kuwa bora mpaka iote, ikiota ndipo unapojua kwamba, ile mbegu ni bora na haiwezi kuota kama hakuna maji. Sasa hivi kuna tatizo la mvua, sasa tumejipanga vipi kuwafundisha Watanzania uvunaji wa maji ya mvua. Kuna mabonde mazuri ya umwagiliaji kwa mfano, Ruaha, Mbuyuni, Mahenge na kule Nyanzwa, yale mabonde maji yanapotea, je, Serikali inasema nini na tutakuwa ombaomba wa chakula mpaka lini?

Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri, tulenge zaidi kwenye utafiti, Maafisa Kilimo wanatakiwa wakae sehemu yenye kilimo lakini kama wataendelea kukaa Mjini kwa sababu ya uduni wa maisha, hatutafika popote. Kwa hiyo, tupunguze siasa tufanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri, pamoja na kuwa njaa ipo lakini usambazaji wa chakula umekuwa mzuri sana. Niishukuru pia na Ofisi ya Waziri Mkuu, inayoshughulikia maafa na sera, wamefanya kazi nzuri, kilio kimepungua lakini tusiwaweke wananchi waendelee kuwa ombaomba, tuwatayarishe ili waweze kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Edward Lowassa, jana alitueleza kwamba, aliwahi kukataa kondoo wa bure, alikataa kwa sababu aligundua kwamba wana matatizo. Sasa mimi nina wasiwasi, kwa sababu mtu akiwa na njaa hawezi kukataa misaada kwa sababu ya njaa. Kwa hiyo, tunaweza kuletewa chakula

ambacho ni kibovu watu wakakipanda, wakafanya kama mbegu, matokeo yake chakula kile kikaleta wadudu na kikileta wadudu maana yake sasa kilimo kile kinazidi kuharibika. Sasa tumejiandaa vipi? Hili ndiyo swali kubwa la kujiuliza hapa. Isije kuwa Tanzania tukawa kituo cha majaribio ya nchi nyingine za nje na kama walivyozungumza wachangiaji waliopita ni kwamba, lazima iundwe Bodi Maalum ya kudhibiti hiki kitu, kama tukienda tu kuweka Kamati tu madhara yake yatakuja kuwa makubwa sana kwa sababu tutaathirika hata kiafya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize tu kwa kusema kwamba, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia. *(Makofi)*

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba ku-*declare my interest* kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo na Chakula. Kwa hiyo, ni miongoni mwa tuliopitisha mapendekezo yetu juu ya hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, naanza kwa kutamka kuwa naunga mkono hoja hii. Mchango wangu katika hoja hii ni kwamba, kwa kuwa Wizara ya Kilimo imetamka mashamba makubwa ya mbegu yataendelea kuendeshwa na Wizara, hilo ni jambo zuri sana. Nashauri katika uendeshaji huo wafikirie sana kupanda mbegu ambazo zitaweza kununulika vizuri na wakulima maana kuna aina ya mbegu zinazoitwa *open pollinated seeds* na kuna aina ya mbegu zinazoitwa *hybrids.* Kwa hiyo, kama haya mashamba makubwa ya Serikali yatapanda mbegu za aina ya *hybrids,* upo uwezekano mkubwa wa maelezo aliyotoa Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha Muswada huu kwamba, wakulima wadogo wadogo wataendelea kuzalisha mbegu. Uwezekano huo utakuwa mdogo sana kwa sababu hawa wakulima wadogo wadogo wanazalisha mbegu kwa njia inayoitwa *informal method, quality declared seeds*.

Kwa hiyo, ili wakulima wapande mbegu hizi, kwa sasa hivi hizi *quality declared seeds* zinapata msaada mkubwa sana kutoka kwa wahisani. Nilikuwa namshauri Mheshimiwa Waziri kwamba, awe na utaratibu wa kuhakikisha kwamba, utaratibu huu kwa kuwa ni mzuri, unasambaza vizuri mbegu kwa wakulima, basi *funding* yake lazima iwe na uhakika wa kuwawezesha wakulima hawa kuendelea kupanda hizo mbegu, vinginevyo tutakuwa tumeshindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ningependa kuzungumzia suala la kilimo cha umwagiliaji. Napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa jitihada zake za kuwezesha mashamba makubwa ya mbegu sasa kuwa yanalimwa kwa kilimo cha umwagilialiji kwa sababu kwa njia hiyo tutakuwa na uhakika wa kupata mbegu zilizo bora. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mengi yamekwishasemwa na Kamati yangu na mimi ni sehemu ya Kamati hiyo, nimesimama hapa kuipongeza tu Wizara, kwa jitihada zake kubwa za kuhakikisha mashamba makubwa ya mbegu yanaendelea kubaki chini yao. Lakini vile vile ningependa nitofautiane kimawazo na wachangiaji wenzangu wanaopenda *genetically modified organism* ziendelezwe nchini kwa sababu tayari nchi kama Mexico sasa hivi hawana mbegu za mahindi kwa kuwa walitegemea mahindi

kutoka Marekani, mahindi hayo yalipofika pale walipoyapanda hayakuota wala hayakufaa hata kuliwa na ng'ombe. Kwa hiyo na sisi tukitaka kuiga mambo haya tunaweza kupata hasara ya maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada ulio mbele yetu, ambao kwa kichwa cha habari kilichopo kwenye *Order Paper* kinasema *The Seeds.* Nadhani nianze kwanza kwa kumshukuru na vile vile kumwambia Waziri kwamba, anatekeleza ahadi yake ya wakati anatusomea Bajeti hapa ya mwaka 2003/2004, ukurasa wa 33, ibara ya 70, alisema: "Sheria Mpya ya Mbegu". Sasa pale siwezi kunukuu yote kwa sababu ya muda. Alisema kwamba: "Muswada wa Sheria Mpya ya Mbegu unaandaliwa na unatarajiwa kuwasilishwa na kujadiliwa katika Bunge lako Tukufu la mwezi Oktoba". Hujakosea sana, huu ni mwezi Novemba, hapa ulisema Oktoba, lakini sasa umetekeleza wajibu wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kwamba, pamoja na wajibu uliokuwa umetekeleza, lakini vile vile katika Sera za Chama cha Mapinduzi, mwelekeo mwaka 2000 - 2010, naomba ninukuu ukurasa wa 15, mikakati ya mapinduzi ya kilimo uwe na malengo makubwa yafuatayo: "Kuweza kuwaongezea wakulima tija katika uzalishaji wa mazao kwa kila eka kulingana na viwango vya kisasa kwa zao linalohusika". Vipo vipengele vingi lakini hiki nimechukua kama ni changamoto tu kwamba, Chama kiliona hili mapema katika kuliangalia na kuweka makada katika maeneo ya Wizara hiyo ili kutekeleza mambo haya haya, yalikuwa sera sasa inakuja Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, kuna *definition* hapa wamesema *Minister, means Minister responsible for agriculture.* Sasa nilikuwa naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mbunge wa Kisarawe ya kusema jinsi unavyoweza kukasimu madaraka. Kuna maeneo ambayo yanaweza kukasimiwa. Kwa mfano, mdomo unaweza kunyamaza ukakasimu madaraka kwenye mkono, ukakataa kusema sitaki au ukasema ndiyo, ukakasimu kwenye kichwa au mdomo au kwa kutumia kichwa au mkono. Ukakataa ukasema hivi au ukakataa kwa kichwa. Huo ni ukasimu mzuri, lakini ukasimu wa Waziri, yapo mambo mengine ambayo hayakasimiwi. Mdomo huo huo niliosema unakasimu madaraka kwa viungo vya mwili umeshindwa kukasimu madaraka kwa kucheka. Huwezi kutumia sehemu yoyote lazima ucheke mdomo wenyewe, kwa hiyo, hapo hauwezi kukasimu madaraka au kwa kula na kununa. Huwezi kutumia eneo lolote la mwili wako kukasimu madaraka kwa mambo hayo. Kwa hiyo, Waziri umetajwa usikwepe madaraka katika Muswada huu ni ya kwako. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ukurasa wa 25 ibara ya (5), *functions of the National Committee,* mmesema kwamba, *to advise Minister formulation and the implementation of the seed industrial policy.* Hivi Sheria ya Mbegu imeshatoka? Hebu naomba tupate nakala zake tuione hiyo sera ya mbegu, tunaomba tuipate kama pengine nilikuwa nimei-*misplace* kwenye Maktaba yangu, nimetafuta mpaka kwenye tovuti sijaiona, kama ipo labda imekuja mwaka 1989 *before* Pawa. Mimi nilikuja mwaka 1990.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika orodha ya *definition* kuna sehemu inaitwa *analyst,* ambayo mmemtumia *analyst* huyu kwenda kufanya *analysis* ya mbegu. Sasa mbegu sidhani kama zinafanyiwa *analysis,* zinafanyiwa *physical test,* kwa hiyo, ni *inspection* kwa sababu *analysis* ni lazima utumie *chemical test to analyse* kujua *contents* zilizomo mle ndani na kuona vitu vingine vingine, hiyo ni *taxonomy* ambayo inaweza ikafanya mambo kama hayo. Sasa hapa *analyst* kwa kweli kwanza, ingawa hamkumweka kule, huku msimtaje kama *analyst,* mbegu zinachunguzwa kwa rangi, wajihi, kwa hiyo inaitwa *inspection* kwenye ibara ya 24 kifungu cha (1) ukurasa wa 31, kwa hiyo, yule aitwe *inspector* siyo *analyst, analyst* ni *chemist,* ni fani moja nzito kweli ambayo mimi ni mmoja wapo ambaye nimeiacha kule. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ni kwamba, wakati umefika vyombo vya udhibiti viundwe katika nchi hii kwa sababu tumetoka katika mfumo hodhi uliohodhiwa kwenda mfumo ulio huria. Sasa binadamu ana matatizo yake kwa sababu Mungu kamwumbia giza ambalo halina sauti lakini analiona, akamwumbia upepo anausikia lakini hauoni. Anatumia maeneo hayo ambayo ni ya kudra kuweza kuficha na kufichama baadhi ya mambo ili kuweza kupata mambo yake binafsi na kuharibu umma ambao umemzunguka. Kwa sababu ya ubinafsi huo basi ndiyo maana tukiambiwa twende mbele, viongozi wanakatisha mkato wanasema twendeni mbele. Maana ya mbele ni *definition* mbele ya Taifa siyo mbele yako binafsi. Nikisema twende mbele, najua Mawaziri mtakwenda kule pamoja na mimi na wale watakuja huku, kwa hiyo, ni mbele ya Taifa siyo mbele yetu binafsi. Kwa hiyo, Muswada huu unalenga mbele ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *scheme* ya mipango husishi katika jedwali namba mbili ukurasa wa 33, inabainishwa moja kwa moja na Muswada huu. Lakini sehemu hizo ambazo zinaitwa Nzega, Shinyanga, Kwimba, katika Wilaya sita za Tanzania, ekari karibu 4,666 zililimwa na walengwa walikuwa 6,312, sheria mpya itawasaidia watu hao katika maeneo hayo na kupanua wigo wa kilimo cha umwagiliaji kama alivyoshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *seeds regulations standard,* kwa mfano, *Act* ya mwaka 1973, tuone vipengele vinavyohusika upande wa *plant cross-section* kama kuna maingiliano ya baadhi ya vipengele kadhaa. Kwa hiyo, pale kifungu kinachohusu mambo ya *pestcide* na masuala mengine, kwenye ile *plant cross-section,* kwa hiyo, kile kingeona kwa sababu kimekuwa kimechukuliwa vizuri sana kwenye *plant cross-section bill.* Halafu kwenye *definition* ya *seeds* ilikuwa *too general* ilipokuwa inakuja lakini mlirekebisha hapa angalau mmeingiza vitu kama *barley* na vitu vingine vingine. Mimi nilidhani mbegu, maana yake ninyi mmeweka mbegu na miche na zile mbaazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwachekeshe, siku moja kulitokea kituko kimoja kwamba mbegu kama za mihogo lazima uelekeze upande ambako mhogo unaonyesha. Sasa mtaalam mmoja alikwenda kusomea kilimo cha mihogo, aliambiwa awaeleze wapanda mihogo kule sehemu za Morogoro kwa kipaza sauti. Sasa alikuwa mvivu kweli kweli, vile vimihogo akaita vijicho. Kwa hiyo, akasema tafadhali wakulima naomba wakati mnapanda miche ya mihogo macho muangalie juu, kumbe yalikuwa ni macho ya

mbegu siyo ya wakulima. Kwa hiyo, lazima zile *regulations* ambazo mnazitoa ziwe zinaelekeza wakulima na vile vile mbegu zielekeze kwa taaluma zilizokuwa zimetarajiwa. Katika kuhimiza ni kwamba mbegu za nafaka, mbegu zile za *barley,* unafanyaje kuzichambua kuzipeleka kwenye *store,*kwa mfano *barley* ya mchungwa na maeneo mengine ya mmea kama mkonge, embe, siyo mbegu ya embe bali zile *barley* za mbegu kuzichambua kama hii ni sahihi kweli, lazima kuna utaalam wa aina yake, hiyo ni *taxonomies,* ni taaluma maalum ambayo inahusu *taxonomy.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kilimo nchini iliendelea, napenda kuwapongeza Mawaziri wote waliokuwa wameshika Wizara hiyo, ikiwa ni pamoja na wewe Mheshimiwa Keenja, ni kwamba, mwaka 1999 kilimo chetu cha Tanzania kiliongezeka kwa asilimia 4.1, mwaka 2000 asilimia 3.4, mwaka 2001 asilimia 5.1, mwaka 2002 asilimia 5.0. Lakini kilimo ambacho ni cha manufaa kinatakiwa kikue kwa asilimia kumi, kwa hiyo, Tanzania hatujiandai kwa njaa kutokana na uwezo wetu mdogo wa teknolojia, vifaa vinavyotumika na maeneo mengine.

Sasa wito, Serikali inatoa wito kwa sababu sasa hivi tunasikia usambazaji wa vyakula vya njaa, hamsambazi mbegu kwa maeneo ambayo yameathirika. Tungeomba zoezi hilo liendelee vile vile la usambazaji wa mbegu kwenye maeneo ambayo yameathirika. Najua kabisa kwamba, hawawezi wakakosa chakula halafu wakawa na mbegu. Kwa hiyo, kuna maeneo ambayo nilitembelea kama vile Mkulazi, Luholole, Ngerengere, Kidugaro, Tununguo na maeneo mengine ya Mikese, Kinonko na Furwe, wana matatizo ya mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuanze mbegu hizo ambazo mnazifanyia majaribio kwenye maeneo yale ya Jimbo langu ili wananchi wale waweze kufanikiwa. Serikali ipeleke mbegu za mahindi, mtama na mihogo, tuna uwezo wa kupandikiza sehemu za Mikese lakini tunaepuka, tunataka mbegu za mihogo ambazo zinahimili ule ukinzani, ambazo zinaweza kupambana na aina fulani ya wadudu wanaweza kushambulia.

Kwa hiyo, maeneo muhimu yabainiwe siyo kila Mkoa upande kila zao na kila Kijiji kipande kila zao, kwa hiyo, hivi Vijiji vinatambulishwa kabisa kwamba, mbegu hata ikiwa bora lakini ardhi na hali ya hewa iliyoko hapo kama haikidhi basi mnawaambia Kijiji hiki msipande mahindi, mnapanda kitu fulani, siyo kutangaza redioni kwamba, pandeni mazao yanayostahimili ukame. Fika *site,* tusiwe na utaratibu wa kupenda kukaa maofisini kama mizimu waje kutuangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naona wachangiaji wawili hawapo hapa lakini walisisitiza wangetaka kuchangia, sasa tutawapa nafasi mchana, Mheshimiwa Malangalila na Mheshimiwa Dr. William Shija, halafu nitampa nafasi mtoa hoja, tutaendelea na taratibu za kawaida na Muswada mwingine unaoishia mchana leo. Hadi sasa hivi wachangiaji wa Muswada unaokuja ni watano tu na ndiyo majina tunayokwenda kuchapisha sasa, nadhani hatutaongeza majina mengine.

Waheshimiwa Wabunge baada ya hapo, naahirisha Bunge mpaka hapo saa 10.00 jioni.

*(Saa 6.27 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Bunge linaendelea. Tuna wachangiaji wawili kama nilivyowatangazia kusema, tuna Mheshimiwa Dr. William Shija, atafuatiwa na Mheshimiwa Benito Malangalila, halafu tutaendelea na taratibu nyingine.

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika Muswada wa utaratibu mpya na madhubuti wa kudhibiti viwango vya mbegu, ambao umewasilishwa na Waziri wa Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono Muswada huu kwa sababu za msingi kabisa kwamba, madhumuni na sababu zilizowekwa kwenye Muswada ni sahihi licha ya kwamba, Muswada wenyewe ni wa kuboresha sheria ambayo tulikuwa nayo ya mwaka 1973. Lakini jambo lingine la msingi ambalo naunga mkono ni kwamba, kilimo ni mbegu, kilimo ni maji, kilimo ni pembejeo na kilimo ni utafiti.

Kwa hiyo, madhumuni yanayoonyeshwa kwenye Muswada huu, ni madhumuni ambayo yanatuelekeza kuwa na matumaini kwamba, suala la kilimo ni mbegu litaweza kuzingatiwa kitaalamu, kisayansi na kwa usimamizi mzuri na wa kisasa.

Lakini sababu nyingine ambayo nimeiona kwenye Muswada ni kwamba, sasa tunalenga katika kushirikisha zaidi sekta binafsi, ambayo wengi tunajitahidi kwenda sambamba nayo jinsi inavyozidi kukua katika nchi yetu. Kwa sababu historia ya nchi yetu ilikuwa ni ile ya vyombo vya umma vinavyosimamia mambo mbalimbali ya sekta zetu za uzalishaji na huduma. Kwa hiyo, naunga mkono sana hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mimi ninavyoona, tatizo letu si katika kutunga sheria, tunajitahidi kutunga sheria nzuri. Lakini kama sheria hii au Muswada huu unavyoonyesha, kazi kubwa itakuwa ni ya usimamizi na udhibiti na kwa hiyo kazi kubwa itakuwa ni ya kutafuta utaratibu uliowekwa ufuatwe ili sekta ndogo nzima ya kilimo kwenye eneo la mbegu iweze kufanywa vizuri. Kwa hiyo, napenda nishauri tu kwamba, taratibu hizi ambazo zimeelezwa kwamba zitatolewa na Mheshimiwa Waziri, mbali na vifungu vya sheria vitakavyokuwepo, ni vizuri vikawekwa vizuri ili kweli viweze kufuatwa na Mheshimiwa Waziri aweze kuwa na utaratibu wa kufuatilia kama je, kile alichoelekeza kinafuatwa kweli au la. Ni vema vyombo tunavyoviunda katika usimamizi huu vipate fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi tunatengeneza vyombo vya usimamizi na udhibiti, lakini hatukuweza kuvipa fedha za kutosha ili vyombo hivyo viweze kufanya kazi ipasavyo. Suala hilo ni gumu na si zuri katika mambo ya kusimamia uchumi. Lakini vilevile natarajia kwamba, kutakuwa na eneo la namna ya kusimamia dharura inayotokana na upungufu au jambo baya ambalo litatokana na tatizo la mbegu. Dharura ambayo Mheshimiwa Waziri, ataiona yeye mwenyewe au kwa kushauriwa na chombo kinachohusika kuweza kuchukua hatua za dharura kadri itakavyowezekana. Kushindwa kushughulikia dharura katika suala la mbegu maana yake ni kuwapotezea kabisa wakulima na wananchi kwa ujumla, mapato na hata chakula ambacho wanakitegemea kutokana na kilimo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, napenda niseme mfano wa mbegu ya pamba ambayo ilishindwa kuota katika msimu wa 2002 na mara tu tulipotoa taarifa katika Bunge hili, kupitia swali langu ambalo nilimwuliza Mheshimiwa Waziri, basi mimi nashukuru kwamba, aliweza kuchukua hatua za haraka, akaweza kutuma vyombo vyake vikafanya utafiti na yeye mwenyewe alifika katika maeneo mengi ya Mkoa wa Mwanza, Mkoa wa Shinyanga, Mkoa wa Mara na hata Mkoa wa Tabora. Napenda nimpongeze sana kwa jinsi alivyolichukua kwa kasi na kulitazama tatizo hilo lilikuwaje. Bila ya kufanya hivyo, inawezekana angeweza kutuona sisi kama wabaya, tunasema tu jambo ambalo liko hewani, lakini nashukuru kwamba, alikwenda kupata ukweli huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbegu hizo zilizoshindwa kuota ni mbegu ambazo zilipita katika mfumo wa sekta binafsi, kama ambavyo tunapendekeza sasa. Ni vyema basi tukawa makini zaidi kwamba, pamoja na kuwa na sekta binafsi, lakini bado Serikali kupitia vyombo vyake, vinavyopendekezwa katika Muswada huu na sheria hii, viwe makini na viwe na uwezo ili kuweza kusimamia mambo ambayo yatatokana na mbegu. Kwa sababu mimi nafahamu katika Wilaya yangu ya Sengerema, wakulima walipata hasara kubwa ya kukosa fedha kwa sababu pamba yao haikuota na kwa mwaka huu wanaendelea kuathirika na kushindwa kununua chakula, kwa sababu hawana fedha kutokana na ukosefu wa mapato kutokana na mbegu ya pamba ambayo haikuota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile ningependa Mheshimiwa Waziri, atumie fursa ya leo kuweza kufafanua ahadi alizozitoa za kuwafidia wananchi ambao walipata mbegu mbovu zimekamilishwa namna gani, pamoja na kuwapa mbegu bure kama maandalizi ya kilimo hiki cha mwaka 2003. Hilo litakuwa jambo zuri kwa sababu Waswahili wanasema, ahadi ni deni na sisi tunajua kabisa kwamba, Mheshimiwa Waziri alikwenda kule kwa dhati na wananchi wa Sengerema wanaodai bado wanadai na orodha zipo. Ni vizuri jambo hilo kama lingekamilishwa ili Serikali ionekane kwamba inaheshimu madai ya wananchi kutokana na hasara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, nilikuwa napenda niseme kwa ujumla tu kwamba, mara nyingi tumeona miaka hii inayojitokeza kuwa ya ukame, Serikali na sisi sote kwa ujumla, tunawahimiza wakulima na tunawahimiza wananchi kwamba, basi walime mazao yanayostahimili ukame. Wito huo unatoka vizuri kwenye vyombo vya habari na kwenye vyombo vyetu mbalimbali, lakini wito huo huwa hauambatani na kupatikana kwa mbegu husika, unasikia tu kuna wito lakini mbegu husika hazipatikani.

Ni bora basi pamoja na utaratibu unaopendekezwa na sheria hii ukawekwa kwamba, unapoona hali ya hewa si nzuri, kama vile ambavyo imetokea mwaka jana na mwaka huu inaendelea kutokea, kama kuna ukame basi ni vyema mbegu ambazo tunawashauri wananchi waweze kuzitumia ziweze kupatikana. Hilo ni jambo kubwa sana ambalo mimi kiutendaji nimeliona na nimewahi kutafuta mbegu Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, wakajaribu kunisaidia, lakini hatukupata mbegu za mtama na uwele ambazo tulizihitaji ili tuweze kudhibiti hali ya njaa iliyokuwa imejionyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, nilikuwa napenda niunganishe makusudio ya Muswada huu na yale ambayo tunaona ni mambo muhimu kuhusu utafiti wa mazao na utafiti wa mbegu na kwa maana hiyo tutafanyaje ili tuweze kuimarisha Taasisi zetu za utafiti katika kilimo, ikiwa pamoja na kutaka kutekeleza sheria hii. Ni mambo ambayo nashauri yangejitokeza waziwazi katika ufafanuzi na baadaye katika utekelezaji ili utafiti wa Tanzania uweze kujionyesha kwamba unakuwa madhubuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Kenya najua wako mbele zaidi kupitia Taasisi yao ya *KABRI* na utafiti wanaofanya wao katika kilimo kwa mwaka nadhani uko karibu mara tatu ya tunaoufanya kwetu. Ni vyema basi kwa kuwa Kenya na sehemu zingine ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wenzetu wanafanya utafiti ambao ni imara zaidi na sisi tukajifunza kutokana na wao. Je, wanatoa fedha kiasi gani, je wanatoa wataalamu kiasi gani, Taasisi zao zinapewa vifaa gani ili kuweza kutimiza utafiti huo? Tafiti hizi za kilimo tukaweza basi kuziunganisha na tafiti za aina nyingine ili kilimo kiweze kuwa imara kutokana na matokeo ya utafiti na hii ni pamoja na mambo ya mbegu za kisasa ambazo ziko katika mfumo wa *GMO*. Ni vizuri haya mambo tukayapanua siyo kwa sura ya Muswada huu tu, lakini kwa sura ya tafiti mbalimbali ikiwa ni pamoja na wadudu, kupotea kwa mazao baada ya mavuno au baada ya msimu wa mavuno kufika na ni mazao kiasi gani tunapoteza. Utafiti huo nao tungeweza kuuweka ukawa imara zaidi na tukaweza kushirikiana na wenzetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

La mwisho, Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda niseme kwa ujumla tu, nimesema pale mwanzoni kwamba, kilimo ni maji na kilimo ni mbegu, kwa hiyo, Muswada huu ningependa tuuone katika sura nzima la kutaka kuinua kilimo, tukiwa tunajua kwamba, lazima tupate maji. Kwa hiyo, sehemu zote ambazo zina maji ni vema tukajitahidi kuzitumia. Juhudi za Wizara tunazifahamu na juhudi za Serikali zilizopo tunazifahamu. Lakini bado nashauri kwamba, kilimo ni ugani. Sehemu ya ugani ina upungufu mkubwa sana katika sekta nzima ya kilimo na bila kuwa na ugani mzuri au huduma za ugani nzuri, basi haiwezekani hata mfumo wa mbegu huu ukaweza kuutekeleza vizuri. Sasa hivi ugani kwa kweli katika Wilaya zetu na Mikoa yetu, nilivyouangalia kwa ujumla bado ni hafifu sana karibu umekufa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, tutafanya nini basi kutekeleza au kuweka mfumo madhubuti zaidi wa ugani ili hata mbegu hizi ambazo zitawekwa kwenye mkondo wa kuuzwa, wa kupatikana, wa utafiti, ziweze kupitia kwa washauri wakuu wetu katika kilimo, ambao ni Maafisa wa Ugani katika sehemu mbalimbali. Miaka ya nyuma, pamoja na miaka ya ukoloni kwa

kweli huduma hizi zilikuwepo na wakulima walikuwa wanaweza wakashauriwa kwa namna mbalimbali kwamba, hapana usitumie mbegu hii sasa, tumia mbegu ambayo imepatikana na yeye mwenyewe Afisa Ugani anafanya majaribio na kuonekana ufanisi mzuri zaidi kuliko hapo awali. Kwa hiyo, yote haya ya kilimo ni maji, kilimo ni mbegu, kilimo ni pembejeo, kilimo ni utafiti na kilimo ni ugani, ni dhana moja ambayo inategemeana. Huwezi ukazungumza tu kwamba, tunatarajia kuwa na mfumo wa mbegu bila kushughulika na kilimo kwa ujumla. Huyo atakayekuwa kwenye Kamati ya Taifa ya Mbegu atakuwa kwa kweli anafanya kazi ndogo sana au kazi bure kwa sababu atakuwa hajapata msaada kutoka kwenye sehemu nyingine zinazohusika na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda niseme tena kwamba, naunga mkono hoja hii na kwamba sheria hii itusaidie katika kutekeleza na kuimarisha kilimo chetu nchini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Muswada huu muhimu uliopo mbele yetu. Naipongeza Wizara ya Kilimo na Chakula na Serikali kwa ujumla, kwa kuleta Muswada huu katika kipindi hiki. Nasema hivi kwa sababu yapo matukio muhimu yanayohusu mbegu katika nchi yetu yaliyokwishajitokeza na yametupa mafunzo. Kulikuwa na tukio lile la mbegu za minazi mifupi, kama tunavyokumbuka, katika nchi lililetwa kwa maelezo mazuri sana. Lakini hatimaye halikuweza kuzaa matunda na likaleta madhara kwa wakulima. Pia tukio lililotokea mwaka jana la madhara ya mbegu za pamba katika Mikoa ya Ziwa, ambapo nazo hazikuweza kuota. Kwa hiyo, kwa kweli tuna kila sababu ya kuuangalia Muswada huu kwa kina na kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ingawa Muswada wenyewe hauonyeshi matumaini makubwa ya kupungua kwa bei za mbegu ambazo ni aghali sana katika nchi hii na wakulima wengi wanashindwa kumudu. Lakini basi yapo mambo ambayo tunadhani ni muhimu kwa nchi yetu. Kwanza kabisa niipongeze Kamati iliyoupitia Muswada huu, imefanya kazi kubwa. Kwa sababu ukiangalia mabadiliko na marekebisho yaliyofanyika ni Muswada mwingine. Kwa hiyo, nasema kwa mabadiliko haya kungelikuwa na Miswada miwili hapa ambapo kwa kweli Serikali ingetakiwa kuuchapisha Muswada huu upya ili uweze kusomeka na uweze kupata *contribution* ya kutosha kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi nikiuangalia Muswada wenyewe, nianze kwanza na Muundo wa Kamati itakayosimamia shughuli hizi za usimamizi wa mbegu katika nchi. Sasa Kamati yenyewe ina wajumbe 9, kati ya wajumbe hao 9, wajumbe 6 wanatoka Serikalini na wajumbe 3 ndiyo watateuliwa na Mheshimiwa Waziri kutoka katika Taasisi mbalimbali zinazojihusisha na masuala ya mbegu. Sasa kwa mtazamo wangu sioni namna ambayo nitashindwa kuamini kwamba, Kamati hii itafanya mambo ambayo yataangalia sana maslahi ya Serikali kuliko ya wadau kwa muundo wa Kamati yenyewe. Hiyo ni *observation* yangu ya kwanza. Kwa muundo wa Kamati yenyewe, sioni kama ina uwezo wa kusimamia soko huria la mbegu katika nchi hii, kwa sababu wajumbe wenyewe wa Kamati ni watu ambao wanatoka katika Serikali na Serikali

inasema kwamba, inajitoa katika biashara inaachia biashara katika soko huria. Lakini bado Kamati hii kwa muundo wake haionyeshi picha hiyo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia inaonekana kwamba, Kamati hii katika Ibara ya 4 sehemu ya pili, itakuwa na uwezo wa kupiga kura. Sasa sielewi kati ya wajumbe hao 9 kama 6 wanatoka Serikalini na 3 wanatoka katika maeneo mengine. Kwanza sielewi hata hiyo kura itakuwa na maana gani. Mimi nadhani kipengele hiki cha kusema Kamati itakuwa na uwezo wa kupiga kura, basi kura hizo zote zitaelekeza maslahi kwa mtu aliyewapeleka pale na izingatiwe kwamba, katika hao watu 6 wote ni watumishi wa Serikali. Kwa hiyo, kimsingi uwezo wa Kamati yenyewe mimi nautilia shaka.

Lakini pamoja na jambo hilo, Kamati hiyo itakuwa na wajumbe 9, kama nilivyosema na Mwenyekiti wa Kamati hii ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Chakula na moja ya kazi zake kama ilivyoelekezwa katika Ibara ya 5 kutoka sehemu (a) mpaka (e) kazi ya Kamati hii ni kuishauri Wizara. Sasa sielewi kama Mwenyekiti wa Kamati ni Katibu Mkuu wa Wizara na wajumbe wake ni watendaji wa Serikali. Sasa hii Kamati ikienda Wizarani inakutana na Mtendaji Mkuu wa Wizara, ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara, sasa sijui Katibu Mkuu anakaa kiti gani? Ina ugumu sheria hii katika utekelezaji wake. Ina ugumu sana kwa sababu wewe Mwenyekiti wa Kamati, unapokwenda kukaa katika kiti ukashauriwa na Kamati ambayo wewe mwenyewe ulikuwa ni Mwenyekiti, ni jambo ambalo kwa kweli haliwezekani katika utendaji mzima wa sheria hii, ni dhahiri kwamba, utendaji wake una *contradiction* nyingi na hauwezekani. Mimi natafsiri kwamba, maamuzi ya Kamati hii ndiyo maamuzi ya Serikali au ndiyo maamuzi ya Wizara, kwa sababu haiwezi kwenda kujipinga yenyewe, ni kitu ambacho kitashindikana kabisa. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Lakini la pili, nikiingia katika sheria yenyewe, kwa bahati mbaya hakuna *definition* au tafsiri ya neno *quality seed* maana yake nini? Sasa kutokana na kutokuwa na tafsiri ya neno hili ambalo ni muhimu katika sheria hii, naona kama ni mapungufu makubwa ya sheria yenyewe. Uzoefu wetu unaonyesha kwamba, mbegu zinaweza kujaribiwa katika maabara ya nchi za nje, lakini zikafika hapa kwetu zikashindwa kufanya kazi. Mimi ningeridhika sana kama ningepata tafsiri sahihi ya neno hili mbegu ndiyo bora. Lakini moja ya sifa zake iwe ni mbegu ambayo imejaribiwa katika mazingira ya Tanzania na kuonyesha mafanikio makubwa. Mimi naona hii ni moja ya sifa kubwa za mbegu na hii ingetokea katika Sheria. Kwa sababu kama tunavyojua, leo watu wote wanataka kufanya biashara hata kama bidhaa zao siyo nzuri sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa nasema kwamba, *quality seed* imepata *definition* na baada ya kupata *definition*, moja ya sifa za mbegu zingekuwa mbegu ambazo zimefanyiwa majaribio katika mazingira ya Tanzania na kuonyesha mafanikio makubwa. Siku zilizopita, tumekuwa na Taasisi zetu zilizofanya kazi nzuri sana na kwa kweli zilifanya utafiti na zilitoa matokeo ambayo matatizo ya mbegu hatukuwa nayo katika nchi. Lakini hivi sasa tunaanza kupata uzoefu kwamba, nchi yetu inakuwa ni dampo la mbegu katika nchi hii na bila kuwa na uzoefu wa mbegu inayoota katika Tanzania, mimi naona hili ni mapungufu makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nilikuwa na maoni ya jumla kuhusu sheria yenyewe. Naiona sheria hii kama imekaa kimya mno juu ya mbegu za asili. Sheria hii kwa ujumla ni kama haizitambui kama zipo mbegu za asili. Sasa hatujui kwa nini iko kimya? Kwa sababu huko tunakotoka vijijini kwetu, wako wakulima wadogo wadogo, ambao kwa utaratibu wao wa asili wanasambaziana mbegu. Sasa sheria inatoa tamko gani juu ya hali hii ya mbegu za asili?

Lakini pia naiona sheria hii kama inafunga mlango mno kwa mbegu za nje ambazo hazijafanyiwa utafiti wa kutosha katika mazingira yetu, naona sheria hii pia ni moja ya mapungufu ambayo yamo ndani ya Sheria. Ziko baadhi ya mbegu ambazo kwa utaratibu inabidi ununue mbegu kila mwaka, kwa sababu huwezi ukapanda mbegu, ukavuna, ukatumia mazao yale kwa ajili ya kupanda mbegu mwaka unaofuata. *(Makofi)*

Sasa tukiangalia mazingira ya nchi yetu, hali za wakulima wetu ni kwamba, kama mbegu za namna hii zitaenea kwa wingi ni dhahiri wakulima wetu watapata matatizo makubwa. Kwa hiyo, sheria hii ni lazima iwaangalie wadau ambao ni wakulima wadogo wadogo katika nchi kuhakikisha kwamba kutakuwa na mbegu endelevu siyo lazima mkulima anunue mbegu kila mwaka. Ni dhahiri kwamba, ukinunua mbegu iliyotoka mwaka huu, ukaipanda mwaka unaofuata, kutakuwa na upungufu wa mazao, lakini itazaa. Sasa mbegu za namna hiyo ndiyo lazima zielekezwe katika nchi badala ya kutegemea mbegu ambazo ukilima mwaka huu ukavuna, mwakani huwezi kuipanda tena shambani. Mbegu za namna hii zitaendelea kuwafanya wakulima wetu wawe maskini zaidi na ni mbegu ambazo kwa kweli hazistahili kuruhusiwa kuuzwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ibara ya 11 inatoa mwanya wa sheria hii nzima kuchezewa. Ibara hii inampa Mheshimiwa Waziri, mamlaka ya kukasimu sehemu ya madaraka au madaraka yote ya masuala ya mbolea kwa mtu au kwa Taasisi. Mnajua Wazungu wana neno wanaita *delegation* na wanalipenda sana. Lakini *excessive delegation* huwa wanaita *relegation,* maana yake unakasimu kupita kiasi na huo ni uzembe, yaani ukasimu kila kitu, sasa jambo hili kwa kweli halitapendeza. Nadhani Mamlaka ya ibara ya 11 yabaki kwa Mheshimiwa Waziri. Suala la mbegu katika nchi limekuwa ni suala gumu na limekuwa ni suala nyeti na limeisumbua sana Serikali. Suala hili awepo mwajibikaji na mwajibikaji mmoja wa suala hili ni lazima awe Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengi ambayo tumeachia achia kwa kutunga sheria hizi, sasa leo zinageuka kuonyesha kwamba, Bunge ndiyo lilifanya. Mtu anauza nyumba za Serikali, anasema aah lakini haya mambo yote yalifanywa na Bunge. Sasa mambo haya tunavyojifunza hatuwezi tena kuruhusu mianya kama hiyo. Ni lazima tuwe makini kabisa kuhakikisha kwamba, tunatunga sheria ambayo haitoi mwanya kwa mtu kuichezea na baada ya yeye kuichezea na kuiharibu, anairudisha tena kwa chombo kilichotunga sheria. Jambo hili nadhani hatuwezi tukalikubali, kwa hiyo ibara ya 11 lazima madaraka na mamlaka yabaki kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna *issue* inazungumzwa duniani leo, hizi *Genetically Engineered Seeds* au *GMO* ni jambo linalozungumzwa. Hili jambo bado tata na sheria hii kwa bahati mbaya haitamki chochote juu ya mbegu ambazo hazijakubalika Kimataifa, iko kimya, nadhani ni mapungufu haya, lazima ndani ya Sheria iwepo *clause* inayosema kwamba, mbegu ambayo haijakubalika Kimataifa, isiruhusiwe kuingia ndani ya nchi ili kuilinda nchi yetu isiwe dampo la mbegu. Hili ni jambo kubwa na muhimu, lazima tuendelee kuwalinda wakulima wetu kwa mambo kama haya. Mimi naona kutokuwa na *clause* inayofunga, maana yake hii Kamati sawa ipo, lakini imepewa madaraka yasiyo na mwisho juu ya uwezo wa kuagiza au uwezo wa kuruhusu mbegu ziingie katika nchi. Kwa hiyo, nasema kuwepo na *clause* inayotamka wazi kwamba, mbegu ambayo itakuwa haikubaliki Kimataifa, isiruhusiwe kuingia ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nilikuwa na mawazo kwamba, kutokana na uzoefu, wako waagizaji wakubwa wa mbegu katika nchi. Mimi nilikuwa nafikiri waagizaji wakubwa lazima wakate Bima ambazo zitawasaidia kuwarudishia wakulima waliopata hasara kwa mbegu ambazo hazikuota, hili ni jambo muhimu. Lakini kuwe na Bima, maana yake tukisema wao wenyewe watarudisha uwezekano huo inawezekana haupo. Lakini wakiwa na Bima, Bima zile ndizo zitakazo *compensate* wakulima ambao imedhihirika kabisa kwamba, mbegu zao hazikuweza kuota kutokana na ubora wa mbegu zenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hili kwa sababu tunajua vyombo vyetu hivi *TBS* na vinavyosimamia masuala haya, tunajua *how passive,* tunajua. Mimi nikisema vinachukua rushwa nitakuwa nasema uongo kwa sababu sina uhakika. Lakini ninachosema ni kwamba, vipo tu *passive* haviwezi kuaminika kwamba, vikitoa leseni, mtu akaleta mbegu katika nchi akauza, watu wakapanda mbegu zisiote wapate hasara tuseme ndiyo mwisho,hapana. Lazima makampuni makubwa yanayoingiza mbegu kutoka nje yawekewe Bima.

Pale wakulima wanapokuwa wamepata hasara, lazima Bima hizo ziweze kuwarejeshea gharama zao na hii ndiyo itakuwa kuwalinda wakulima. Kwa sababu kwa kweli kwa hali ya sasa, mkulima hana mlinzi kabisa, akienda kununua jembe bovu basi ni hasara yake, akienda kununua mbolea haikuweza kutoa mazao hiyo ni hasara yake. Hatuwezi kuendelea namna hii wakati asilimia 80 ya wananchi wetu ni wakulima wadogo na wakulima maskini sana, lazima tufike mahali tuweze kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kengele inigongee tena, bado dakika moja, basi hii dakika moja nikupe uweze kutengeneza mambo yako vizuri. Lakini nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na kwa kawaida kama nilivyosema, naunga mkono Muswada huu. Mambo haya niliyosema basi Serikali iyaangalie kwa karibu sana kwa sababu ni mambo muhimu ambayo kwa kweli ni ya msingi katika ujenzi wa uchumi na kuwasaidia wakulima wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza kabisa, nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu na mimi vilevile nichangie kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, kuhusu Muswada huu wa Sheria ya Udhibiti wa Viwango vya Mbegu ya mwaka 2003. Naanza kwa kusema bayana kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, waliochangia kwa kauli na kwa maandishi. Michango yenu ni mizuri sana na imesaidia sana kuboresha hoja iliyoko mbele yetu, kwa maanufa ya kuendeleza kilimo chetu nchini, kwa lengo la kujitosheleza kwa chakula na kupambana na umaskini miongoni mwa wananchi na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kwa kutoa maelezo mafupi kwa baadhi ya yale yaliyoulizwa wakati Waheshimiwa Wabunge walipochangia. Moja ya kitu kilichozungumzwa ilikuwa elimu kuhusu maudhui ya Muswada. Baada ya sheria hii kupitishwa na Bunge hili Tukufu, Maafisa Kilimo katika Vyuo watafundishwa mabadiliko yote yaliyomo kwenye Muswada, kwa hiyo, watakuwa wameelewa Muswada huu unazungumzia nini. Hoja nyingine ambayo natakiwa kuchangia ni watumishi kuwa chini ya *DED.* Kutokana na sheria tuliyoipitisha katika Bunge hili Tukufu ya mwaka 1988, Watumishi wa Kilimo kama Watumishi wengine Wilayani, wataendelea kuwa chini ya Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya husika, lakini kitaaluma huwa pia na mahusiano ya moja kwa moja na Wizara Mama yaani Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni matokeo ya utafiti kuwafikia wakulima. Kutokana na Muswada huu, jitihada ya Wizara hii ni kuzalisha mbegu kwenye mashamba ya wakulima kwa mfumo wa *Quality Declared Seeds,* yaani mbegu zilizothibitishwa na *TOSCI* chini ya Wasimamizi na Wataalam wa Utafiti wakishirikiana na Maafisa Ugani kule Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine lilihusu mbegu za jamii ya mikunde. Ilivyo sasa hivi, Makampuni binafsi yanakuwa yanashughulikia zaidi mbegu ya jamii ya nafaka mfano mahindi, lakini Makampuni hayashughuliki zaidi na mbegu kama choroko, kunde, mbaazi, fiwi, karanga au ufuta na kadhalika. Hivyo, uzalishaji wa mbegu za aina hii kutokuwa shughuli zaidi ya Wataalam wa Ugani na Utafiti huko Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine lililozungumziwa ni kwamba, Tanzania hatuhitaji kukabiliwa na njaa kwa sababu kuna mito mingi yenye maji mwaka mzima, pia maziwa makubwa sana kama Victoria, Tanganyika na Nyasa na mabonde yenye rutuba nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana nao Waheshimiwa Wabunge na hii ndiyo maana Wizara iliainisha upya kuwako kwa hekta 29 milioni zinazofaa kwa umwagiliaji wa maji mashambani. Aidha, mwaka huu wa 2003/2004 imetengwa kwenye bajeti shilingi zaidi ya bilioni 3 kwa shughuli za umwagiliaji na mnaweza kuelewa jinsi tulivyoshughulikia miradi mbalimbali, angalau katika kila Mkoa uko mradi na tunaendelea kufuatilia kila Wilaya tupate miradi kupitia Halmashauri za Wilaya husika.

Aidha, Wizara imeandaa *Irrigation Master Plan*, hivyo siku za usoni tatizo halitakuwa kubwa kama lilivyo leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine lililozungumziwa ni kwamba, tusiletewe chakula chenye wadudu, ninakubaliana na mtoa hoja hiyo. Kutokana na kupitisha *Plant Protection Act* ya mwaka 1997, tatizo la kupewa chakula chenye wadudu limepungua kwa kiasi kikubwa sana kuliko ilivyokuwa kabla ya sheria hii. Tatizo la nzige huko Kilolo linafuatiliwa kwa makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni juu ya umuhimu wa kusambaza mbegu kwenye maeneo yenye njaa. Ilivyo sasa hivi, Kitengo cha Maafa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu mara zote hutoa chakula cha njaa, lakini vile vile hutoa fedha au pengine mbegu zenyewe za kupanda mazao ya muda mfupi kukidhi njaa baada ya chakula cha msaada kwisha *(family leaf),* ikimalizika watu wanaweza kujitegemea. Hii ndiyo sera ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine lilikuwa ni kwamba, tukisambaza mbegu tuhakikishe kuwa mbegu hizo zina ukinzani. Ninakubaliana kabisa na hoja hiyo, karibu aina zote za mbegu za mazao zinazozalishwa na utafiti zina ukinzani wa magonjwa au wadudu waharibifu muhimu, mfano *Uyole hybrid* namba 615 ina ukinzani dhidi ya ukungu wa majani ya mahindi *(grey leaf spot)* na hiyo imeandaliwa na watafiti wetu wa humu humu nchini.

Mwisho, mafanikio ya utafiti ya miaka 40 toka uhuru ni yapi? Nafikiri yako mengi sana. Katika kipindi cha utafiti wa miaka 40 tumeweza kutoa aina nyingi za mbegu za mazao ya jamii ya nafaka. Mfano mahindi, tumetoa mbegu za Staha, Kilima, Kito, *Ukiriguru composite, Uyole hybrid* niliyoitaja namba 615 na kadha wa kadha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpunga tumetoa *Saro 5, TXD 85, TXD 88*. Hata ngano tumetoa mbegu za ukinzani, mbegu bora iitwayo Chiriku, Mbayuwayu na Mware na siyo hivyo tu hata mtama una mbegu zilizozalishwa na utafiti. Mbegu aina ya Masiha, Patu na Wahi. Uwele nao ziko mbegu hizo Okoa, nyingine inaitwa Shibe, mikunde na kadha wa kadha. Ziko mbegu za pamba zinazoitwa Ukiriguru 95 au *IL 85, UK 92* na *IL 85,* kahawa vile vile. Ndugu zangu wanaotoka Kusini, watakumbuka kuwa korosho zilikuwa zinashambuliwa sana na ukungu. Watafiti wetu wazalendo walibuni dawa yake na wakatafuta dawa ikapatikana inaitwa *sulphur.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na haya yote, ningeweza kueleza kwa saa kadhaa, lakini muda ni mchache nataka kusema hivi, hakika watafiti wetu wanastahili pongezi kubwa kwa haya yote niliyoyataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sasa napenda tena kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa maelezo mafupi kwa baadhi ya hoja ambazo zimetokea hapa. Lakini nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na kwa kweli wametoa maelezo ambayo ningekuwa nimeyasikia mapema, nafikiri ningeyatumia katika maelezo yangu.

Mheshimiwa Richard Ndassa, anasifu anasema: "Mbegu ni uhai." Mheshimiwa Dr. William F. Shija amesema: "Kilimo ni mbegu", maana bila kuwa na mbegu zinazofaa ni matatizo kabisa. Mheshimiwa Musa Lupatu anazungumzia msingi wa kilimo ni mbegu. Kwa hiyo, sote tunakubaliana kwamba, mbegu ni muhimu sana katika kilimo na wale ambao mmekutana na baadhi ya hizi mbegu ambazo zina sifa nzuri za uzalishaji na ukinzani na kadhalika, mtakubaliana nami kwamba, mbegu zinaweza kufanya tofauti kubwa sana katika uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hizi aina za mbegu za mpunga alizozungumzia Mheshimiwa Prof. Pius P. Mbawala, zina uwezo wa kutoa mpaka magunia 40 kwa eka au magunia zaidi ya 100 kwa eka, lakini mbegu ya kienyeji inaweza ikatoa magunia 5 - 10 kwa eneo lile lile. Kwa hiyo, mbegu inafanya tofauti kubwa sana katika uzalishaji. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao kwa kweli wameunga mkono nia ya kuwa na utaratibu wa kusimamia na kudhibiti mbegu katika nchi ili kuhakikisha kwamba, kazi hii muhimu haiingizwi katika matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo waliochangia kwa kutoa hoja hapa Bungeni, ningeomba kwa ruhusa yako niwataje nikianza na Mheshimiwa Musa A. Lupatu, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, ambaye ndiye Mwenyekiti wa kikao hiki, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, wakati mwingine anapenda kujiita kivuli, Mheshimiwa Athumani S. M. Janguo, Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Venance M. Mwamoto, Mheshimiwa Prof. Juma M. Mikidadi, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Semindu K. Pawa, Mheshimiwa Dr. William F. Shija, Mheshimiwa Benito W. Malangalila na mwisho Mheshimiwa Prof. Pius P. Mbawala, Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, naomba niwataje pia wale waliochangia kwa maandishi, nao ni Mheshimiwa Athumani S. M. Janguo, Mheshimiwa Prof. Phillemon M. Sarungi, Mheshimiwa Janeth B. Kahama, Mheshimiwa Abu T. Kiwanga na Mheshimiwa Richard M. Ndassa. Wote naomba niwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mambo mengi yaliyozungumzwa ni ya kuunga mkono, nitazungumzia tu yale ambayo yanahitaji ufafanuzi kidogo, maana naweza nikachafua mambo mazuri yaliyozungumzwa hapa kwa kujaribu kuyapamba bila sababu. Niombe tu kueleza kwamba, Muswada huu lengo lake ni kuweka utaratibu wa kudhibiti biashara ya mbegu katika nchi, ndiyo kazi yake. Huu Muswada hauna kipengele chochote kinachohusiana na uzalishaji wa mbegu.

Suala la uzalishaji litashughulikiwa kwa utaratibu tofauti, Muswada huu unataka kudhibiti tu, unafanya nini na mbegu na unahakikishaje kwamba mbegu unayotumia ina sifa hizo zilizokubalika. Kwa hiyo, kama ukisema umezalisha mbegu inayotoa magunia 40 kwa eka, ni lazima hiyo mbegu itoe magunia 40 kwa eka. Ikitoa chini ya hapo umefanya kosa kwa sababu unasema uongo na mkulima akichukua ile mbegu akaipanda ikatoa chini ya magunia 40 katika mazingira yaliyoelezwa, basi ana haki hata ya kukupeleka Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baya zaidi ni uingizaji wa mbegu kutoka nje. Tangu mwaka 1993 tulifungua milango na mbegu zikaingia huku nchini kiholela kabisa. Mfano mwaka jana katika Maonyesho ya Nane Nane, Morogoro, tulikuta watu wa Kenya wanaonyesha aina mbalimbali ya mbegu walizoleta na moja haiku-*perform* kabisa. Kwa hiyo, ilibidi tuchukue nafasi ile ile kuwaambia hii mbegu isije ikaonekana tena hapa nchini vinginevyo tutatafuta jinsi ya kuwashughulikia, lakini wakati ule hatukuwa na sheria ya kuweza kuwashughulikia, kwa sababu sheria yetu ilikuwa imetoa ukiritimba kwa *TANSEED* ambayo *TANSEED* yenyewe haikuwa tena inashughulikia mbegu. Hawa wameleta mbegu zao mbovu kwa kuruhusiwa tu kwa utaratibu ambao haukutawaliwa na sheria, hivyo ikatupa matatizo. Kwa hiyo, kazi ya Muswada huu ni kudhibiti haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, tunatarajia kwamba, mtu atakayeleta mbegu humu nchini sasa atapambana na *TOSCI,* ambayo itahakikisha kwamba, anaijaribu ile mbegu na kuridhika nayo kwamba ina hizo sifa zinazosemekana kabla ya kuiruhusu na hapa ndipo penye jibu la *GMO.* Hatukuizungumzia *GMO* katika Muswada huu kwa sababu kuna kazi ambayo haijakamilika juu ya *GMO* na itabidi tulete Muswada hapa Bungeni utakaohusu *GMO*. Huwezi kushughulikia *GMO* kama *general issue* katika Muswada mwingine, inahitaji kwa kweli ifafanuliwe katika Muswada wake pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tumefikiri tungeweza kufanya semina ya Wabunge na Viongozi wengine katika mwezi huu ili tujieleweshe juu ya hizi *GMOs* ni nini, zinatengenezwaje, athari zake ni nini na kadhalika. Hivi sasa wenzangu wanatafuta fedha, kama zitapatikana, nina hakika hiyo semina itafanyika na kama hazikupatikana kipindi hiki itafanyika mapema iwezekanavyo ili baadaye twende katika hatua inayofuata kutunga kanuni za kuingiza *GMOs* huku nchini na hatua inayofuata ya kutunga sheria ya kusimamia uingizaji wa *GMOs* humu nchini. Ndiyo maana *GMO* haikuzungumzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuingiza *GMO* kwa sababu utaratibu uliowekwa ni lazima uwe *registered,* ni lazima upewe leseni. Sasa, ukiomba kwamba unataka kuleta *GMOs* utakataliwa maana utaratibu huo haupo ni mpaka utakapokuwepo. Kwa hiyo, kwa sasa hatujaweka utaratibu na haitawezekana kuingiza *GMOs* mpaka utaratibu utakapokuwa umewekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona Mheshimiwa Prof. Maghembe anatikisa kichwa kidogo. Nina hakika Wabunge karibu wote wanaamini kwamba, *GMOs* zina madhara kama hazikuwa *handled properly* na kwa hiyo lazima tuweke *system* kwanza mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya uzalishaji wa mbegu, tunaandaa *Executive Agency* itakayoshughulikia masuala ya mbegu na hiyo *Executive Agency* inayoandaliwa

itaunganisha watafiti, mashamba ya kilimo na wazalishaji wa mbegu ili kuhakikisha kwamba, tuna mtiririko. Huko nyuma miaka iliyopita watafiti walikuwa hawasimamii uzalishaji wa mbegu zao na kwa hiyo haikuwepo njia ya kuhakikisha kwamba, ubora wa zile mbegu zilizotoka kwa watafiti unabaki ule ule.

Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, alisema kwamba, utafiti haujawa na manufaa. Mheshimiwa Mbunge, naomba utakapopata nafasi uje nikutembeze ili uone baadhi ya kazi nzuri sana zilizofanywa na watafiti. Tukichukua kwa mfano mpunga, kuna *varieties* sasa ambazo zina-*combine* sifa za mpunga wa Kyela na uzalishaji kwa wingi wa mpunga tuliopata wakati mmoja ulikuwa unaitwa kitumbo, nafikiri kutoka Uchina. Kwa hiyo, ukila ladha ni ile ile, harufu ni ile ile, lakini unapata magunia 40 kwa eka.

**MBUNGE FULANI:** Japan.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Ilikuwa Japan eeh, walaji wa wali wanajua umetoka wapi. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, unapata sifa zile zile, lakini sasa unapata magunia 40 kwa eka badala ya magunia matano. Kwa hiyo, kuna kazi nzuri sana kwa kweli ambazo zimefanywa na watafiti, isipokuwa nikubali kwamba, baadhi ya matokeo, *actually* matokeo mengi sana ya watafiti wetu hayajawafikia wakulima kwa sababu ile *chain* ya kuwaunganisha ilikuwa haipo na kwa ajili hiyo katika Wizara sasa hivi tumeunganisha mafunzo na utafiti ili yaende pamoja. Mwanafunzi anayetoka chuoni anajua tangu mwanzo utafiti gani unafanyika katika eneo gani ili aweze kwenda kwenye vile vituo na vile vile awe na kiungo cha kumwezesha kupeleka huo utafiti huko kunakohusika.

Mheshimiwa Malangalila amesema, *Quality Declared Seed* siyo *defined. Quality Declared Seed* ni *defined*, tena iko *defined* katika sheria wala haikuwa *amended.* Ningeomba atazame tena *Quality Declared Seed means seed produced by registered smallholder farmer which conforms to the specified standards of crops, fishes* na kadhalika na hata utaratibu wake wa kuitengeneza katika hii *definition* umeelezwa. Lakini zaidi ku-*define Quality Declared Seed* tulirudi tuka-*define seed* kwa sababu katika sheria ilikuwa imekuwa *defined as a true seed.* Sasa, ukiniambia kwamba, Mwanri ni Mwanri hujaniambia lolote juu yake.

Kwa hiyo, tumerudi ku-*define* katika hii *Schedule of Amendments,* tumerudi ku-*define* mbegu ni nini, ni sehemu yoyote ya mmea ambayo inaweza kutumika kwa *propagation* na tumetoa mifano mingi sana inayoeleza hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lupatu, alipendekeza kwamba, wakaguzi wa mbegu waende mpaka Wilayani. Kwanza, Chombo kitakachotusaidia kusimamia na ku-*certify* mbegu ni *TOSCI* na ni Chombo ambacho ni cha Kiserikali, lakini ambacho kimepewa *independence* kubwa sana, ndiyo maana hakipo Dar es Salaam, kiko Morogoro na kina matawi katika maeneo yale yanayozalisha mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kwamba, mbegu itakuwa *stratified at the entry* ama *production point.* Kama unaingiza mbegu kutoka nje, kwa mfano, hawa watengenezaji wa mbegu *Cargil, Monsanto* ama wengine, anaingiza mbegu kutoka nje atapambana na *TOSCI* mpakani ambao wata-*certify* hiyo mbegu yake na *actually* anatakiwa awe ameshaleta hiyo mbegu imejaribiwa na kuwa *certified* ndipo aweze kuiingiza humu nchini.

Hivyo hivyo, wazalishaji wa mbegu ambao watakuwa wanazalisha mbegu zitakazotupa tabu, ni wazalishaji wakubwa siyo wazalishaji wadogo wadogo. Hawa wazalishaji wadogo watazalisha *Quality Declared Seed* ambayo itasimamiwa na Afisa Kilimo na mwaka jana Tumeanza kuwa-*train* hawa jinsi ya kusimamia uzalishaji wa *Quality Declared Seed.* Mwaka 2002 tuli-*train* 20 na mwaka huu tutaendelea ku-*train* ili kila Wilaya baadaye iwe na watu ambao wanaweza wakasimamia *production* ya *Quality Declared Seed.* Kwa hiyo, kwa hawa wa kusimamia wazalishaji wakubwa na uzalishaji mkubwa wa mbegu hakuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarajia pia kwamba, katika miaka inayokuja wauzaji wengi wa mbegu watazalisha mbegu hizo hapa nchini. Tunatumia *billions of shillings* kila mwaka kuagiza mbegu kutoka nje sasa hivi. Hizi mbegu mnazosema tunatumia asilimia 10 zinatugharimu mabilioni ya shilingi. Isitoshe ndiyo mbegu zenye gharama kubwa kwa sababu inabidi ununue kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbegu tunazozalisha katika mashamba yetu nyingi ndiyo zile alizozungumzia Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah kwamba, ni *Open Pollinated.* Kwa hiyo, unaweza ukapanda, uka-*select,* ukapanda tena na zikaota zikakupa sifa zile zile *over and over again.* Hizi zinazotoka nje nyingi ni *hybrids*, ukipanda mwaka huu ni lazima mwaka kesho ununue tena. Mfanyabiashara hana sababu ya kuzalisha *Open Pollinated Seed* kwa sababu akishakupa ndiyo basi tena yeye biashara imekwisha, lakini sisi tunazalisha *Open Pollinated Seed* kwa sababu tunataka mkulima wetu ajitegemee kwa mbegu. Anaweza akazalisha *Saro* mwaka huu, aka-*select* mbegu yake nzuri mwaka kesho akaipanda *Saro* ile ile na ikampa sifa zile zile alizopata mwanzo.

Kama tunataka kuzitumia kama mbegu ndipo sasa tunapozisimamia na kuhakikisha kwamba, inakuwa ni *Quality Declared Seed* ambayo inakuwa na zile sifa zinazotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu mashamba yetu yamelima eka 648 ambazo tulikuwa tunatarajia kwamba zingetoa zaidi ya tani 1,500, lakini kutokana na hali ya hewa tunafikiri zitateremka mpaka tani 900 hivi ya mbegu tuliyozalisha katika mashamba yetu. Mwaka kesho zitakuwa *multiplied* tena na kwa hiyo tutafika mahali ambapo tutazalisha kwa wingi na kuwa na mbegu sasa zitakazotuwezesha kuajiri mawakala wa kuzalisha mbegu. Kwa hiyo, wale wenye mashamba makubwa wanaweza wakaingia katika mkataba na Serikali wakazalisha mbegu zile kama wakala kwa ajili ya ku-*distribute* kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ruzuku limezungumzwa sana, ruzuku kwa wakulima hasa kuhusiana na mbegu. Sasa, kwa mbegu tunazozalisha wenyewe na *Quality Declared Seed,* tunatarajia bei itakuwa ndogo sana, lakini kwa mbegu zinazotoka nje bei itaendelea kuwa juu kwa sababu hao wanaozileta kutoka nje wanazileta ili waziuze na wapate faida. Tutakachoweza kufanya ni kudhibiti utaratibu wa kuleta hizo mbegu na kama nilivyosema, kuhakikisha kwamba, wanahimizwa kuzalisha hizo mbegu humu humu nchini badala ya kutuletea mbegu walizozalisha nje na tumeshawapa *notice* kwamba, kwa kweli mtu akitaka kuuza mbegu kwa wingi hapa nchini atazalisha hapa hapa, lakini kama anataka azalishe nje alete mbegu, auze hapa itabidi tuzungumze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda niseme kwamba, *quality* ya mbegu zilizozalishwa na watafiti wetu ni bora kuliko mbegu nyingi sana tunazoagiza kutoka nje, ni nzuri sana, zina sifa bora sana. Kwa mfano, kuna kitu kinachoitwa *Quality Protein Maize* ambayo mtoto akila hata asipokula *protein* hatashikwa na utapiamlo kwa sababu ina *protein* nyingi. Ukilisha mifugo hivyo hivyo, hiyo mifugo yako hata kama haikupata *another source of protein* haitakuwa na matatizo. Ni mbegu zilizozalishwa na watafiti wetu, ni nzuri sana na nyingi sana hazina *competitor* kutoka nje. Sasa hivi wamezalisha mbegu ambayo inastahimili ukame ambayo watu wa Dodoma wanaopenda kulima mahindi wangeweza wakazitumia kwa sababu zinastahimili ukame kwa mazingira ya nchi yetu. Kwa hiyo, tuna hakika kwamba, mbegu tunazozalisha tutakapozi-*multiply* kwa wingi zita-*compete* katika soko na mbegu zozote zitakazoletwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ile Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Mbegu ambayo imekuwa na matatizo, imezungumzwa kuwa na matatizo makuu mawili. Naomba tukubaliane kwamba, suala la mbegu ni suala la kitaalam. Hii ni Kamati ambayo kwa kweli ni *technical, it is a Technical Committee*, si Kamati tu inayokwenda kuzungumzia mbegu bila kuweza ku-*follow up* ile *science* ya mbegu inavyozalishwa na ndiyo maana ukiangalia Wajumbe wake tisa wanatokana na *scientists.* Katibu Mkuu ni Mwenyekiti, anaongoza kikao kile, lakini Wajumbe wake wote ni *scientists* na hiyo ni makusudi kwa sababu wanazungumzia suala la kitaalam, si suala tu la kugawa mbegu.

*Actually,* sidhani kama kuna wakati pengine watakapozungumzia maslahi ya mkulima, lakini watazungumzia maslahi ya mkulima kwa kuzungumzia *quality* ya mbegu zilizozalishwa. Kwa hiyo, ni tofauti kidogo na zile Kamati nyingine ambazo ni za Biashara, hii siyo Kamati ya Biashara. Hata hawa watu binafsi tunaotarajia kwamba, watateuliwa ni lazima wawe ni watu wenye taaluma ya mbegu. Kama ni mtu asiyekuwa na taaluma ya mbegu, atakaa pale watu watakuwa wanazungumza, lakini juu ya kichwa chake hataelewa wanazungumza nini. Maana watakuwa wanazungumza juu ya sijui manasaba na *breeding methods* na nini, ambazo zinaweza zikatoa matatizo. Ndiyo maana wengi wa Wajumbe hawa ni *scientists,* ambao wanatoka kwenye Taasisi za Utafiti, wanatoka kwenye Vyuo Vikuu kama Sokoine ambavyo vinashughulikia masuala ya uzalishaji wa mbegu, ndiyo sababu ya wao kuwa wengi kiasi hiki katika hii Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kumshauri Katibu Mkuu, Katibu Mkuu kweli ni Mtendaji Mkuu wa Wizara, lakini ndiyo mshauri wa Wizara pia na tunapozungumzia kushauri Wizara ni pamoja na kumshauri huyo Waziri na kushauri Viongozi wengine

walioko katika Wizara ambao baadhi yao nao watakuwa katika hii Kamati. Hii ndiyo sababu tu ya hii Kamati kuwa na muundo huo, hakuna sababu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 22 (4) (b) Mheshimiwa Janguo ali-*point out* kwamba, kuzuia mbegu kwa miezi sita ni kipindi kirefu mno. Nitamwomba tutakapokuja kwenye Kamati tu-*amend* kifungu hicho kwa kukubaliana naye ili tupunguze ule muda uwe miezi mitatu badala ya miezi sita. Ni kweli kabisa ukiweka mbegu kwa miezi sita ukija kuiotesha si ajabu isiote tena. Kwa hiyo, tunakubaliana naye na tutarekebisha hilo *accordingly*. *(Makofi)*

Nimezungumzia mambo mengi. Mheshimiwa Malangalila hapa mwisho amezungumzia mambo mengi sana. Sasa, kuna suala la kulinda mbegu asilia ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Janeth Kahama na wamelizungumzia Wajumbe wengi sana, hata Mheshimiwa Malangalila amelizungumzia sasa hivi. Kwanza, nieleze kwamba, tuna vituo ambavyo kazi yake ni kuhifadhi nasaba za mbegu zilizopo hapa nchini.

Mheshimiwa Janeth Kahama, anazungumzia kwa mfano, aina za mpunga uliokuwa unapatikana Shinyanga, ambao sasa hivi haupatikani. Kama akitueleza kikamilifu ni mpunga wa namna gani, tukienda kwenye vituo vyetu tutakuta umehifadhiwa, tunaweza tukauotesha ukaanza tena kupatikana kama kweli una sifa nzuri kiasi hicho. Kwa hiyo, mbegu zote hizi ambazo zimepata kutumika katika kilimo hapa nchini zinahifadhiwa katika vituo hivi. Kituo kinachoongoza ni *TPRI*, lakini vituo vyetu vyote vya utafiti vina jukumu hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeulizwa na Mheshimiwa Pawa kwamba, hivi kwa mfano migomba au mihogo utahifadhije nasaba zake? Kuna *open fields*, kwa mfano, tuna shamba la michungwa liko Handeni, kwa hiyo kama unataka aina ya michungwa iliyoko humu nchini ipo katika shamba imeoteshwa na hivyo ndivyo tunavyofanya kwa migomba. Ukienda pale Tengeru, kuna shamba la migomba lenye migomba mingi tu ambapo ukitaka mbegu ndipo utapata na kadhalika. Lakini kuna Vituo vya Kimataifa pia vinavyohifadhi nasaba hizi na ukizihitaji unaweza kuagiza na wanaweza kukuletea kwa *tissue culture.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubaliana na Mheshimiwa Prof. Maghembe, juu ya kutumia teknolojia za kisasa za kuzalisha ili kuzalisha kwa wingi. Kwa mfano, tuna aina sita za kahawa ambazo zina ukinzani dhidi ya *CBD* na *leaf rust* na kama ukizitumia zile unapunguza sana matumizi yako ya madawa ya kupambana na magonjwa haya. Sasa, kama tukiweza kuzi-*multiply* zile kwa wingi na tukazifanya *available* kwa mkulima, tutakuwa tumempunguzia sana gharama. Lakini utaratibu uliokuwa unatumika kuzizalisha ulikuwa unakwenda pole pale sana.

Juzi nikiwa Mbinga nimeshangaa kukuta kumbe utaratibu ule unaweza ukatumiwa na mkulima akazalisha miche yake mwenyewe kwa utaratibu wa vipando. Kwa hiyo, tunataka sasa tuhakikishe kwamba, kwenye kila Wilaya tuna miche ya miti ile ya kahawa na tuwafundishe wakulima jinsi ya kupanda miche yao wenyewe ili waweze

kui-*multiply* haraka zaidi. Lakini njia ya haraka zaidi ni *tissue culture,* ameiita *micro systems of production,* ni *tissue culture*. Kwa *tissue culture* unaweza uka-*produce millions of seedlings* katika muda mfupi tu na kwa hiyo ukasambaza kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi njia zote zitatumika na vituo vyetu vya utafiti karibu vyote sasa hivi vimekuwa vinaweka hizi *systems* za *tissue culture* na *TPR.* Kituo cha Lyamungo bado hakijaweka, lakini kitaweka kwa fedha walizopata kutokana na utaratibu ule wa *STABEX.* Kwa hiyo, itafika siku tutakuta vituo vyetu vyote vina uwezo wa kuzalisha *tissue culture* na tuta-*multiply* haraka sana uzalishaji. Kwa hiyo, suala la kulinda mbegu zetu za asili ni suala la msingi na huu Muswada unatupa nafasi ya kuweza kulinda mbegu hizo za asili kwa sababu tunaweza kukataza kuingizwa kwa mbegu zozote zitakazoingiliana na mbegu tunazozalisha humu nchini.

Suala lingine ambalo limejitokeza na ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Prof. Mikidadi, ambalo amelizungumzia vile vile Mheshimiwa Lupatu, ni fidia kwa wakulima. Muswada unatambua na kuweka utaratibu wa makusudi wa mkulima kulipwa fidia itakapotokea amepewa *planting material* ambayo haiku-*conform* na mategemeo yake ama na makubaliano yake na mtu aliyemwuzia. Sasa ni nani atakayelipa fidia?

Mheshimiwa Janguo, alisema kwamba, yule mfanyabiashara mdogo wa Kariakoo hataweza kulipa fidia hiyo na sisi hatumtarajii yule alipe hiyo fidia kwa sababu yeye siyo mzalishaji wa mbegu wala siyo mwagizaji wa mbegu, yeye ni *distributor,* yeye ni wakala, ni *outlet* tu ya zile mbegu kumfikia mkulima, kuna mtu nyuma yake ambaye ndiye atakayekuwa ameleta hizo mbegu. Aidha, ni *Monsanto*, ni *Cargil* ama ni Kampuni ya Uzalishaji wa Mbegu hapa nchini.

Sasa hiyo ndiyo itakayowajibika kwa kusambaza *materials* ambazo hazilingani na matakwa ya mkulima na kumsababishia mkulima hasara. Kwa hiyo, sasa hivi kwa kuwa tunakwenda kwenye soko huria, basi biashara yenyewe inafanyika kihuria pia, kwamba kama ukimsababishia mkulima hasara utawajibika kwa hiyo hasara uliyosababisha. Kwa hiyo, ni lazima uhakikishe kwamba, *quality* ya mbegu unayosambaza inalingana na ulivyoeleza.

Vile vile Mheshimiwa Benito Malangalila, amesema kwenye sheria pengine tungeweka kifungu ambacho kinamtaka huyu akate Bima lakini nafikiri ni *automatically,* mfanyabiashara yeyote atakuwa na Bima inayowezesha kufanya hiyo biashara, lakini tutaangalia vile vile katika kanuni ni jinsi gani tunavyoweza kumbana kuhakikisha anaweka utaratibu utakaomwezesha kulipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo limeleta mtafaruku mkubwa sana hapa ni hili la Waziri kukasimu madaraka yake chini ya kifungu cha 11. Mheshimiwa Musa Lupatu amelizungumzia, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Benito Malangalila, wote hawa wamelizungumzia kwamba Waziri asikasimu madaraka yake. Kwamba kila kifungu kinasema *"may",* kinamruhusu tu kinasema *you may do this*, hakisemi *"shall"*, kingesema *"shall"* ingekuwa ni maana tofauti kabisa kwamba, ni lazima akasimu

madaraka yake. Katika kifungu kile mngesoma vile vile mngeona kwamba, *actually* hata ukikasimu madaraka yale bado unaweza ukatekeleza madaraka yale, kuyakasimu haikunyang'anyi uwezo wa kutekeleza yale madaraka uliyokasimu.

Kwa hiyo, kama hungependa kukasimu kutangaza hii sheria ianze lini, basi unatangaza mwenyewe hii sheria ianze lini na hata kama kuna mtu mwingine angekasimu madaraka hayo hatayatumia. Mimi sioni tatizo la hili kwa sababu kukasimu madaraka haya ni utashi wa mtu kama akitaka kukasimu atakasimu, lakini akiona kwamba jambo lenyewe halifai kukasimu, hatakasimu. Kuna mambo mengine unafanya *only once* kwa mfano, ukishatangaza kwamba hii sheria ni *effective,* basi *it becomes effective* kuanzia siku hiyo ulipotangaza na kuendelea mpaka itakapobadilishwa tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishatunga kanuni ndiyo umetunga kanuni na imemalizika. Kinachofanya inasema ni *may, you may, you may not,* kwa hiyo, hiki kifungu hakina matatizo. Kifungu kinachonipa matatizo na tumeshauriana na *Attorney General* haraka haraka hapa ni kile kifungu cha ku-*detain* mbegu kwa kipindi kirefu, jambo ambalo lingeweza kusababisha hizo mbegu zisifae, kwa hiyo kutuletea matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze hapa kwamba, baada ya soko huria kuanza kufanya kazi katika nchi yetu, tumejikuta kwamba *systems* za kufanya kazi na soko huria hazikuwepo. Mkiangalia ile Miswada tuliyopitisha jana ya kusajiri Maafisa Mifugo na vile vile ya kudhibiti magonjwa ya mifugo, ni sheria zinazojaribu kuweka mazingira katika nchi ya kutuwezesha kufanya shughuli za kilimo katika mazingira hayo ya soko huria.

Tunaendelea kuzirekebisha moja baada ya nyingine ili tufike mahali tuwe tumejenga mazingira ambayo yatamwezesha huyu mkulima kuzalisha kwa ufanisi na bila kuathiriwa sana na vitendo ambavyo vinaweza vikafanywa na wafanyabiashara binafsi.

Wafanyabiashara binafsi ni *efficient* katika kufanya mambo fulani fulani, mradi kuna faida na wakati mwingine wanaweza wakaifuata hiyo faida wakasahau maslahi ya mkulima. Kazi ya Serikali ni kuhakikisha kwamba, tunaweka utaratibu wa kulinda hayo maslahi ya mkulima.

Ni kuweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba, kilimo chetu kinaendelea kukua na kuzalisha kiasi cha chakula cha kutosha na hata kuuza nje. Ili tuweze kufanya mambo haya, ni lazima tuunde mazingira haya na tuweke utaratibu wa kuyalinda ili yasiweze kuingiliwa bila kudhibitiwa kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, kwa kweli jukumu langu lilikuwa ni kuzungumzia haya mambo machache tu. Waheshimiwa Wabunge, wametoa michango mizuri sana, wameielewa sheria hii vizuri hata kuliko walioi-*draft* nafikiri, naomba niwashukuru sana kwa michango yenu ambayo imetufumbua macho hata sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo naomba kutoa hoja. Ahsante sana.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kudhibiti wa Viwango vya Mbegu wa Mwaka 2003**
***(The Seeds Bill, 2003)***

Kifungu cha 1

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ohoo! Kumbe tuko kifungu cha kwanza siyo cha pili nilikuwa naongea juu ya *definitions* kumbe hatujafika huko. Ahsante. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu, kama mimi nilivyojieleza pale awali, bado nadhani kwamba, Muswada haukidhi mahitaji ya sekta hii ya mbegu. Lakini sina tatizo na kusisitiza sana kwamba, turudishe Muswada huu, isipokuwa katika *definition* maana ya mbegu lazima ibadilike iwe *brooder* na nilikuwa napendekeza hapa kwamba, *seed means true seed* na nilikuwa napendekeza tubadilishe sehemu hiyo iwe *or other plant proper guise including vegetative propagated materials, tissue culture, GMO offered for sale and so on. I think it is important* kwamba, hii inakuwa inatamkwa wazi.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *definition* ya *seed* imekuwa *amended* katika hii *schedule of amendments* tuliyosambaza, *seed means that part of a plant which is or indented to be used for propagation and include any true seed, any vegetative material including seedling, corm, cutting, bulb, pulbil, layer, marcott, root, runner, scion, set, split, stem, stock, stumpe, sucker or tuber so used or intended to be so used.* Kwa hiyo, utakuta kwamba, hata hivi vidudu vingine kwa mfano, *tissue culture* inakuwa *covered* katika mchanganuo huu. Sisi tulifika mahali tukakwama kama Mheshimiwa Profesa Maghembe alivyokwama kwamba, hii *definition* haikuwa *all impressing* na kuna vitu ambavyo vingeweza vika-*escape* kama haikupanuliwa ikafikia hapa na kamati yetu utakumbuka ili-*note* hili pia.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 3

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 4
Kifungu cha 5

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 6
Kifungu cha 7

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 8

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 9

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 10

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 11

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 12

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Hiki kifungu cha 12 kinasema: *"The Ministry may make orders".* Sasa katika suala la hoja ya ruzuku Waziri alivyotueleza hapa nilitaka ufafanuzi kwa sababu amesema itajileta yenyewe kutokana na *production,* lakini ana uwezo wa kusema kwamba angalau tutafikiria basi, tunaomba ufafanuzi zaidi kuhusu suala la ruzuku.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa vizuri sana Mheshimiwa Thomas Ngawaiya. Analozungumzia ni kwamba, chini ya kifungu cha 12 ambacho *The Ministry may make orders* basi kiwepo kifungu cha (e) pengine ambacho kinasema *make orders* ambazo zinatoa ruzuku kwa mkulima. Sasa hili haliwezekani kwa sababu fedha hizo itabidi ziwe *voted* na *Parliament* ndipo ziweze kutumika kutolea ruzuku. Itategemea uwezo wa Serikali katika mazingira yatakayokuwepo kwa wakati huo. Sasa ukisema itatoa ruzuku, isipotolewa tutakuwa tunavunja sheria. Kwa hiyo, nilikuwa naomba *systems* hizo za uzalishaji wa mbegu ambazo zinakuwa *put in place* zitatuhakikishia kwamba tunapata mbegu kwa bei nafuu na hilo ni muhimu zaidi kuliko kuandika sheria ambayo haitatekelezeka.

Kifungu cha 13
Kifungu cha 14

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 18
Kifungu cha 19

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 20

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 21

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 22

**MWASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, wakati anahitimisha hoja yake kwenye kifungu hiki cha 22 (4) (b), kulikuwa na hoja ilitolewa na Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Athumani

Janguo, kuhusiana na muda huo kwamba ni mrefu sana. Serikali imetafakari na Waziri tumeshauriana naye, nadhani badala ya kusomeka 6 tunapendekeza kwa kufanya kufuta neno 6 na badala yake tuweke 3. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 33

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Viwango vya Mbegu wa Mwaka 2003 *(The Seeds Bill, 2003)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima, imeupitia Muswada wa Mbegu *(The Seeds Act, 2003)* kifungu kwa kifungu, pamoja na marekebisho yaliyopendekezwa na kuukubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada uitwao *The Seeds Acts, 2003* kama ulivyobadilishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukulibaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Hatua za kupitisha Muswada kuwa Sheria zimemalizika, muda uliobaki siyo mwingi sana na taarifa niliyonayo ni kwamba, Muswada ule uliokuwepo leo umeahirishwa utasomwa kesho na tutaujadili kesho.

Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 11.18 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi*
*Tarehe 6 Novemba, 2003 Saa 3.00 Asubuhi)*